


Sauti *ya* Sheria

TOLEO NA. 2 — MACHI - SEPTEMBER, 2026

Jarida



UTEKELEZAJI WA DIRA 2050 MCHANGO WA SEKTA YA SHERIA KATIKA KUJENGA TANZANIA MPYA



ISBN-13: 978-2820268600



www.oag.go.tz

www.nps.go.tz

www.osg.go.tz

www.ocpd.go.tz

DIRA

Kuwa Taasisi yenye Ufanisi, Kitaaluma na Kuaminika katika kutoa Huduma Bora za Kisheria kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**DHIMA**

Kutoa Huduma za Kisheria zenye Ubora kwa njia ya Kuandaa Sheria, Upekuzi na Majadiliano ya Mikataba pamoja na Ushauri wa Kisheria kwa Maendeleo ya Kijamii, Kiuchumi na Kisiaa.

DIRA

Huduma Bora za Mashtaka kwa Wakati na Usawa kwa wote.

DHIMA

Kuhakikisha Huduma za Mashtaka Zinazotolewa kwa Ufanisi, Tija kwa kuzingatia Weledi, Uadilifu na Ushirikishaji wa Wadau.

**DIRA**

Kuwa Ofisi Mahiri ya Umma ya Kusimamia na Kuendesha Mashauri ya Madai na Usuluhishi yanayohusu Serikali.

DHIMA

Kuratibu, Kusimamia na Kuendesha Mashauri ya Madai na Usuluhishi kwa niaba ya Serikali kwa Ufanisi na Weledi wa hali ya juu

**DIRA**

Kuwa Kitovu cha Ubora katika Uandishi wa Sheria

DHIMA

Kutoa Sheria Bora na zinazopatikana kwa urahisi kwa ajili ya Maendeleo Endelevu





Mhe. Hamza S. Johari
Mwanasheria Mkuu wa Serikali



Mhe. Samwel M. Maneno
Naibu Mwanasheria Mkuu wa
Serikali



Bw. Sylvester Mwakitalu
Mkurugenzi wa Mashtaka



Dkt. Ally Possi
Wakili Mkuu wa Serikali



Bw. Onorius Njole
Mwandishi Mkuu wa Sheria

YALIYOMO

- | | |
|----|--|
| 01 | RAIS SAMIA AFUNGUA MKUTANO WA MAWAKILI WA SERIKALI, ASISITIZA WELEDI, UADILIFU NA ULINZI WA RASILIMALI ZA TAIFA |
| 04 | WAZIRI MKUU ASISITIZA USHIRIKIANO WA KIKANDA NA MATUMIZI YA TEKNOLOJIA KUPAMBANA NA UHALIFU |
| 06 | WAZIRI HOMERA AIPA KONGOLE OWMS KWA UTENDAJI KAZI KWA WELEDI |
| 08 | RAIS DKT. SAMIA AAGIZA SHERIA ZILIZOTAFSIRIWA KWA LUGHA YA KISWAHILI KUWAFIKIA WANANCHI |
| 09 | SERIKALI YASAINI MKATABA WA UBIA WA UCHIMBAJI WA GESI YA HELIUM SONGWE |
| 11 | WATUMISHI WAPYA NPS WATAKIWA KUZINGATIA MAADILI YA UTUMISHI WA UMMA |
| 13 | WAKILI MKUU WA SERIKALI AKUTANA NA RAIS WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU |
| 15 | SERIKALI KUIMARISHA UPATIKANAJI WA HAKI KUPITIA KAMPENI YA MSAADA WA KISHERIA - AWAMU YA PILI |
| 17 | MAWAKILI WA SERIKALI WAHITIMU MAFUNZO YA AWALI YA PROPRAMU CP3P |
| 19 | MAGARI 21 KUONGEZA KASI YA UTENDAJI NPS |
| 21 | JAJI AHIMIZA MABORESHO YA MIFUMO YA KISHERIA KUWAVUTIA WANAWAKE SEKTA YA USULUHISHI |
| 23 | OCPD KUFANYA MAPITIO YA SHERIA ILI ZIENDANE NA DIRA 2050 |
| 25 | “CHAMA BORA CHA KITAALUMA NI KILE KINACHOISAIIDIA SERIKALI KUFIKIA MALENGO YAKE” – MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI |
| 28 | DKT. HOMERA APONGEZA USIMAMIZI MZURI WA UJENZI WA JENGO LA NPS MKOA WA SINGIDA |
| 30 | SEKTA YA SHERIA NI MSINGI WA UCHUMI WA NCHI |
| 32 | SERIKALI KUONGEZA WIGO WA UPATIKANAJI WA MIKOPO KWA WANANCHI |
| 34 | KUFIKIA MALENGO YA DIRA YA 2050 TAIFA LINAHITAJI ZAIDI YA UTAALAMU WETU WA SHERIA”– MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI |

- 36** KUELEKEA DIRA 2050 SERIKALI YAIMARISHA ULINZI WA WATOTO
- 38** OSG YAJIPANGA UENDESHAJI WA MAJUKUMU YA KISHERIA
- 40** TANZANIA YANG'ARA CALC: BI REHEMA KATUGA AIBUKA MSHINDI WA AFRICA
- 42** SERIKALI YAJIPANGA KUREKEBISHA SHERIA ILI ZIENDE SAMBAMBA NA DIRA 2050
- 45** DPP AWAPONGEZA MAWAKILI WA SERIKALI KWA KUFIKIA ASILIMIA 88 YA USHINDI WA MASHAURI
- 47** DKT. POSSI: VIONGOZI NI TASWIRA YA TAASISI NA SERIKALI KWA JAMII
- 49** OCPD YAUNGA MKONO KAMPENI YA TANZANIA 27 YA KIJANI
- 50** NAIBU MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AKAGUA MRADI WA UJENZI WA JENGO LA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI MTUMBA
- 52** NAIBU DPP AHIMIZA USHIRIKIANO KATIKA KUDHIBITI UHALIFU WA KIFEDHA
- 54** OWMS YAWASILISHA TAARIFA YA UTEKELEZAJI KWA KAMATI YA BUNGE
- 56** OCPD NA AFISI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR ZAJENGEANA UWEZO MASUALA YA UANDISHI WA SHERIA
- 57** “KATIKA UTEKELEZAJI WA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2050, TUNA MATARAJIO MAKUBWA NA MAWAKILI WA SERIKALI” – NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA
- 59** MIONGOZO YA MAAMUZI YA KUSHTAKI NA UTAIFISHAJI MALI ILETE TIJA KATIKA UTOAJI HAKI – NAIBU DPP
- 60** WAKILI MKUU WA SERIKALI ASHIRIKI UZINDUZI WA KAMATI ZA USHAURI WA KISHERIA NGAZI YA MKOA NA WILAYA
- 63** OCPD NA MIKAKATI YA MATUMIZI YA TEKNOLOJIA KATIKA UANDISHI WA SHERIA
- 67** “SHERIA INA THAMANI PALE INAPOBADILISHA MAISHA YA WATU” – MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI
- 69** UENDESHAJI WA MASHAURI YA JINAI MAHAKAMANI KWA MFUMO WA KIFICHO
- 73** SG AKAGUA UJENZI WA JENGO LA OFISI MTUMBA, DODOMA

73 SERIKALI NA MIKAKATI YA KUPAMBANA
NA UTAKATISHAJI FEDHA

75 BUNGE LAPITISHA MUSWADA WA SHERIA
NA 2 WA MWAKA 2026

76 “LENGO LETU NI KUREJESHA TABASAMU KWA WANANCHI”-
MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

79 SEKTA YA SHERIA NI MIUNDOMBINU LAINI KUFIKIA
DIRA 2050

82 OFISI YA AG NA NDOTO YA KUWA CHACHU YA
KUFIKIA MALENGO YA DIRA 2050

85 MCHANGO WA OCPD KATIKA MCHAKATO WA KUTUNGA
SHERIA NCHINI

88 MAWAKILI WA SERIKALI SIMAMIENI UTAWALA WA
SHERIA ILI KUFIKIA MALENGO YA DIRA YA TAIFA 2050

TAHARIRI YA WAHARIRI



LELA O. MUHAJI
Mhariri

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI



PRISCA ULOMI
Mhariri

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI



REBECCA KWANDU
Mhariri

OFISI YA TAIFA YA MASHTAKA



CARINE SENGUJI
Mhariri

OFISI YA MWANDISHI MKUU WA SHERIA
SHERIA

Tanzania imeingia katika kipindi kipya cha utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Dira inayoweka mwelekeo wa kujenga Taifa lenye uchumi shindani, utawala bora, na maendeleo endelevu.

Ni muhimu kufahamu kuwa, dira hii si waraka tu wa Serikali pekee, bali ni mwongozo wa pamoja unaowahusu Watanzania wote na taasisi mbalimbali katika kutimiza matarajio ya Taifa kwa kipindi hadi mwaka 2050.

Katika hotuba yake wakati wa uzinduzi wa Dira mnamo tarehe 17 Julai, 2025 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alisema ni lazima kufanyika kwa mapitio ya Sheria mbalimbali ili ziweze kuendana na mwelekeo wa Dira 2050 na hii inatokana na ukweli kuwa Sheria ni nguzo kubwa na muhimu inayoweza kuwezesha Dira hii kufikiwa na kufanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Utekelezaji wa Dira 2050 unahitaji zaidi ya kuwa na mipango na mikakati, inahitajika nyenzo madhubuti za utekelezaji, mifumo imara ya kisheria, taasisi zenye uwezo, ubunifu, uwajibikaji na kubwa ushiriki wa kila Mtanzania. Kwa mantiki hiyo,

Sheria ni kiungo cha kuyaunganisha haya yote katika mnyororo mmoja.

Sekta ya Sheria ina nafasi ya kipekee sana katika safari hii tuliyoianza ya utekelezaji wa Dira, kwani Sheria huweka misingi ya utekelezaji wa sera na mipango ya Taifa, hulinda haki za wananchi, inawezesha mazingira bora zaidi ya uwekezaji na biashara na zaidi inaimarisha utawala wa sheria.

Hapa tunamaanisha kuwa utekelezaji wa Dira 2050 kwa mafanikio makubwa hauwezi kabisa kutenganishwa na uwepo wa mfumo wa sheria unaoendana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kiteknolojia na kimazingira yanayoendelea kote duniani.

Hivi karibuni, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika hotuba yake wakati wa uzinduzi wa nyenzo za utekelezaji wa Dira alisisitiza kuwa, Taasisi za Kisheria zifanye maboresho ya Sheria ili Sheria hizo ziendane na malengo ya maendeleo kufikia uchumi wa dola trilioni moja ifikapo mwaka 2050.

Kwa upande wa Sekta ya Sheria, kama alivyoelekeza Mhe. Rais Dkt. Samia kuwa,

ni muhimu kuhakikisha kuwa mfumo wetu wa kisheria unaendelea kwenda sambamba na mahitaji ya Taifa linalolenga kuwa na uchumi wa kisasa na shindani, uchumi wa kidijitali, matumizi ya teknolojia na akili mnemba (AI), uwekezaji, biashara, rasilimali za Taifa, na huduma za umma zote hizi zinahitaji mfumo wa kisheria unaokidhi mahitaji ya wakati.

Kwa muktadha huo, utekelezaji wa Dira 2050 unatupa fursa ya kutafakari upya nafasi ya sheria katika kujenga Tanzania tunayoitaka. Sheria si tu chombo cha kudhibiti mwenendo wa jamii, pia ni nyenzo ya kuleta maendeleo ya kweli.

Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria (OCPD), kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na

Tume ya Kurekebisha Sheria, imeanza zoezi la mapitio ya sheria mbalimbali zinazohitaji marekebisho au uandishi mpya ili ziwezekwenda sambamba na mahitaji ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050.

Katika kuunga mkono utekelezaji wa Dira hiyo, OCPD imeendelea kuwekeza katika kuwajengea uwezo watumishi wake kupitia mafunzo mbalimbali, hususan katika maeneo ya kimkakati yanayohusiana na uandishi, urekebu na tafsiri ya sheria, hatua inayolenga kuhakikisha Ofisi inaendelea kuwa na wataalamu wenye ujuzi na uwezo unaohitajika katika kuandaa mifumo ya sheria inayokidhi mahitaji ya maendeleo ya Taifa.

“Ninyi ni walinzi wa kalamu na siyo walinzi wa bunduki. Ni walinzi wa kalamu na sheria zenu. Kwa hiyo mwende mkalinde uchumi wetu, kwa haki na uadilifu ili nchi hii iweze kupokea wawekezaji wengi zaidi, tuwekeze zaidi, tukuze uchumi, masilahi yapatikane.” Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 29 Septemba 2022.



RAIS SAMIA AFUNGUA MKUTANO WA MAWAKILI WA SERIKALI, ASISITIZA WELEDI, UADILIFU NA ULINZI WA RASILIMALI ZA TAIFA

- Na Lela Muhaji -



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza wakati wa Ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania (TPBA), Jijini Arusha.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, amewataka Mawakili wa Serikali kuendelea kufanya kazi kwa uadilifu, weledi, uzalendo mkubwa na kuwa walinzi wa rasilimali za taifa kwa kutumia kalamu ya Sheria.

Rais Samia aliyasema hayo, wakati akifungua rasmi Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Chama cha Mawakili wa Serikali tarehe 13 Julai, 2026 Jijini Arusha.

"Nataka nilisisitize hilo, Kalamu ya Mwanasheria ikitumika vizuri inaweza kuzuia hasara kabla haijatokea, inaweza kulinda mkataba kabla haujawa mzigo kwa serikali, na inaweza kuiongoza Serikali kufanya maamuzi bora na yenye maslahi kwa taifa." Alisema Dkt. Samia

Aidha, Dkt. Samia aliwataka Mawakili wa Serikali kuendelea kuwa walinzi wa rasilimali za taifa kwa kutoa ushauri wa kisheria kwa usahihi, uzalendo, uaminifu na kutanguliza mbele maslahi ya taifa ambapo

Serikali itaendelea kuwawezesha Mawakili wa Serikali kwa kuwajengea uwezo wa kitaaluma na Mazingira wezeshi ya kazi zao.

Katika hatua nyingine, Mhe. Rais aliipongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hatua mbalimbali ambazo Ofisi inaendelea kuzichukua katika kuimarisha mifumo ya upekuzi wa mikataba, urekebu wa tafsiri ya sheria, msaada wa kisheria, Kliniki ya Sheria na mafunzo na elimu ya Sheria kwa Wananchi.

“Nawapongeza sana kwa hatua hizi za kuimarisha mifumo ya mikataba, urekebu wa tafsiri za sheria, Msaada wa kisheria na Kliniki za sheria, hatua hizi kwa njia moja au nyingine zimesaidia kuimarisha utekelezaji wa shughuli za maendeleo na ustawi wa wananchi wetu.” Alisema Mhe. Rais

Vilevile. Dkt. Samia aliipongeza jitihada za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuendeleza huduma za msaada wa kisheria ikiwezo kazi ya kutafsiri sheria kwa lugha ya Kiswahili ambayo iko mbioni kakamilika.

“Hatua hii mliyoichukua ni muhimu na ya kupongezwa kwani mwananchi anapoelewa sheria anaelewa haki zake, wajibu wake, mipaka ya uhuru wake na mipaka ya mamlaka ya Serikali hii ndio maana halisi ya utawala wa Sheria”. Alisema Mhe. Rais.

Dkt. Samia alieleza kuwa, ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya 2050 ni lazima kuwa na mfumo wa Sheria unaoshawishi wananchi kujielekeza na kuchangia kwenye Uchumi imara, Shindani, umuishi na unaongozwa na maarifa na ubunifu.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akipokea Kitabu cha Falsafa ya Sheria ya “Mama Samia” kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari wakati wa Ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa TPBA uliofanyika Jijini Arusha.

“Mwelekeo wa Taifa hili kwa miaka 25 ijayo ni kuona mfumo wetu wa sheria na utoaji wa haki unashawishi watu kujielekeza na kuchangia kwenye Uchumi imara, shindani, jumuishi na unaongozwa na maarifa na ubunifu, hili litawezekana tukiwa na sheria bora.” Alisema Dkt. Samia

Kwa upande wake, Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera alieleza kuwa Wizara ya Katiba na Sheria inaendelea kufanya kazi kwa ushirikiano na Chama cha Mawakili wa Serikali kupitia mlezi wa Chama hicho, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambapo Wizara imeweza kukipatia chama hicho Ofisi katika jengo la Wizara lililoko Mtumba Jijini, Dodoma.

Naye, Rais wa Chama cha Mawakili wa Serikali anayemaliza muda wake, Bw. Bavoo Junus alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali yake ya Awamu Sita kwa kukiwezesha

Chama cha Mawakili wa Serikali kutekeleza majukumu yake kwa usahihi, na kukifanya chama hicho kuendelea kukua na kuimarika huku kikitoa mchango chanya, wenye tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Mawakili wa Serikali.

Aidha, Bw. Bavoo alieleza kuwa chama hicho kitaendelea kushiriki katika programu za utoaji wa huduma za msaada wa kisheria katika mikoa mbalimbali na kuhakikisha wananchi wanapata elimu kuhusiana na masuala mbalimbali ya kisheria.

Mkutano Mkuu wa Chama cha Mawakili wa Serikali uliofunguliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 13 Julai, 2026, Pamoja na mambo mengine ulihusisha Uchaguzi wa nafasi mbalimbali za uongozi katika chama hicho uliofanyika tarehe 14 Julai, 2026.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa huduma za Sheria, Bi. Neema Ringo wakati wa Mkutano wa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania (TPBA) Jijini Arusha.

WAZIRI MKUU ASISITIZA USHIRIKIANO WA KIKANDA NA MATUMIZI YA TEKNOLOJIA KUPAMBANA NA UHALIFU

- Na Rebecca Kwandu -



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba akifungua Mkutano Mkuu wa 11 wa Umoja wa Waendesha Mashtaka Ukanda wa Afrika Mashariki uliofanyika Jijini Dar es salaam.

Katika dunia inayozidi kuunganishwa kwa kasi kupitia maendeleo ya sayansi na teknolojia, changamoto za uhalifu wa kimataifa nazo zimekuwa zikibadilika kwa sura mpya na mbinu za kisasa zaidi. Uhalifu unaovuka mipaka, unaopangwa kwa ustadi mkubwa na unaotumia mianya ya teknolojia, umeendelea kuwa tishio kwa usalama, uchumi na mifumo ya haki jinai katika mataifa mbalimbali duniani. Kutokana na hali hiyo, Serikali ya Tanzania imeendelea kusisitiza umuhimu wa ushirikiano wa kikanda na matumizi ya teknolojia kama silaha muhimu katika kukabiliana na changamoto hizo.

Akifungua Mkutano Mkuu wa 11 wa Umoja wa Waendesha Mashtaka Ukanda wa Afrika Mashariki (EAAP-AGM) tarehe 14 Mei 2026 Jijini Dar es Salaam, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck

Nchemba, alisema kuwa mafanikio katika mapambano dhidi ya uhalifu wa kimataifa hayawezi kupatikana bila ushirikiano madhubuti baina ya nchi na nchi pamoja na matumizi sahihi ya teknolojia.

Aidha, Waziri Mkuu alisisitiza umuhimu wa nchi wanachama kubadilishana taarifa kwa wakati, kushirikiana katika uchunguzi wa makosa ya jinai pamoja na kutumia teknolojia kwa ufanisi zaidi ili kuzuia na kudhibiti uhalifu unaovuka mipaka, hususan makosa dhidi ya wanyamapori ambayo yameendelea kuathiri uchumi na rasilimali za mataifa mengi ya Afrika.

Dkt. Mwigulu alieleza kuwa maendeleo ya teknolojia yameleta manufaa makubwa katika sekta mbalimbali, lakini kwa upande mwingine baadhi ya wahalifu wamekuwa wakiyatumia maendeleo hayo kufanya uhalifu kwa urahisi zaidi, jambo linalozifanya

nchi wanacha ma kuwa na wajibu wa kuimarisha mifumo ya pamoja ya kukabiliana na changamoto hiyo.

“Kama ambavyo uhalifu unaovuka mipaka na kupangwa unaongezeka bila kujali mipaka ya nchi, vivyo hivyo vyombo vya dola na mifumo ya haki ya jinai haviwezi kukabiliana nao kwa ufanisi bila kuwa na mifumo madhubuti ya ushirikiano wa kimataifa, hususan katika maeneo ya msaada wa kisheria na urejeshaji wa watuhumiwa,” alisema Dkt. Mwigulu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Bw. Sylvester Mwakitalu, alisema kuwa mapinduzi ya sayansi na teknolojia yamebadilisha taswira ya uhalifu wa kisasa ambapo wahalifu wanaweza kutenda makosa katika nchi moja huku

madhara yake yakionekana katika nchi nyingine. Alisema hali hiyo imeongeza umuhimu wa ushirikiano baina ya waendesha mashtaka katika ukanda wa Afrika Mashariki ili kuweka mikakati ya pamoja ya kukabiliana na changamoto hizo.

“Mkutano huu umekuwa jukwaa muhimu kwa waendesha mashtaka kubadilishana uzoefu, kujifunza mbinu mpya za uendeshaji mashauri ya jinai pamoja na kujadili namna

bora ya kutumia teknolojia katika kuimarisha utoaji wa haki miongoni mwa nchi wanachama” alieleza Bw. Mwakitalu.

Sambamba na hayo, tarehe 15 Mei 2026, siku ya pili ya mkutano huo, Umoja wa Waendesha Mashtaka Ukanda wa Afrika Mashariki (EAAP) ulizindua Mpango Mkakati wa Umoja huo unaolenga kuimarisha mapambano dhidi ya uhalifu mpya unaovuka mipaka unaochochewa na maendeleo ya teknolojia.

Mkutano huo pia ulitoa mapendekezo mbalimbali yatakayosaidia kuimarisha mifumo ya haki jinai na kuongeza ufanisi wa waendesha mashtaka katika ukanda wa Afrika Mashariki kupitia matumizi ya eknolojia na ushirikiano wa kitaalamu.

Mkutano huo uliofanyika tarehe 4 hadi 6 Mei, 2026 uliwakutanisha washiriki kutoka nchi wanachama 14 za Ukanda wa Afrika Mashariki ambazo ni Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Malawi, Sudan Kusini, Sudan, Somalia, Zambia, Msumbiji, Shelisheli na Ethiopia, huku ukitoa taswira ya dhamira ya pamoja ya nchi hizo katika kuimarisha usalama, haki na ushirikiano wa kikanda kupitia mifumo ya kisasa ya haki jinai.



Washiriki wa Mkutano Mkuu wa 11 wa Umoja wa Waendesha Mashtaka Ukanda wa Afrika Mashariki wakifuatilia kwa makini mada mbalimbali zilizowasilishwa kwenye mkutano huo uliofanyika Jijini Dar es salaam.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba akiwa katika picha na washiriki wa Mkutano Mkuu wa 11 wa Umoja wa Waendesha Mashtaka Ukanda wa Afrika Mashariki uliofanyika Jijini Dar es salaam.

WAZIRI HOMERA AIPA KONGOLE OWMS KWA UTENDAJI KAZI KWA WELEDI

- Na Prisca Ulomi -



Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera (Mb) akizungumza na watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mara baada ya kuwasili katika Ofisi hiyo wakati wa ziara ya kikazi iliyofanyika Jijini Dar es Salaam.

Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera (Mb), aliwapongeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa utendaji kazi kwa weledi wa usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya madai, katiba, haki za binadamu na usuluhishi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake ndani na nje ya nchi.

"Hongereni kwa kazi kubwa, muendeleo kuifanya kwa weledi, uzalendo, nasi Wizarani tutaendelea kuwapa ushirikiano ili muweze kutekeleza majukumu yenu kwa ufanisi zaidi, milango ya Ofisi ipo wazi, tutafanya kazi usiku na mchana, tufanye kazi kwa kujitoa na tutangulize maslahi ya taifa mbele" alisisitiza Mhe. Waziri Dkt. Homera.

Mhe. Dkt. Homera aliyasema hayo alipofanya ziara yake ya kwanza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya kuteuliwa kuongoza Wizara hiyo kwa lengo la kujitambulisha, kufahamiana na menejimenti ya OWMS na kufahamu majukumu ya Ofisi hiyo.

Katika ziara hiyo, Mhe. Waziri Dkt. Homera aliambatana na Naibu Waziri wake, Mhe. Zainab Katimba (Mb) ambaye aliwasihi wajumbe wa menejimenti na watumishi wa OWMS kuwa waendeleo kutumia mifumo ya TEHAMA katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku. Mifumo hii inahitajika kwenye Sekta ya Sheria ambapo pamoja na kutumia mifumo hii pia tunatekeleza azma ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan

ya kuhakikisha kuwa Serikali inatumia mifumo ya TEHAMA inayosomana.

Wakati akimkaribisha Mhe. Waziri Dkt. Homera kuzungumza na menejimenti na wafanyakazi wa OWMS, Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi alisema kuwa OWMS ni lango la uchumi na maslahi ya taifa. Hivyo, OWMS itaendesha mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake kwa kuhakikisha kuwa maslahi mapana ya taifa yanalindwa.

Akiwasilisha taarifa ya OWMS kwa niaba ya menejimenti, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo aliwaarifu viongozi hao kuwa hadi kufikia mwezi disemba, 2025 OWMS imeendesha jumla ya mashauri

10,576 ya madai na kati ya hayo imemaliza mashauri 1,715 na imeendesha mashauri 258 ya usuluhishi na imemaliza 35 kati ya hayo.

Pia, Bi. Mtulo aliongeza kuwa OWMS inakwenda sambamba na maelekezo ya Serikali ambapo tayari inatumia mfumo wa CIMS wa kupokea, kusajili, kupanga, kupata takwimu sahihi za mashauri na kwa wakati na kutunza taarifa na idadi za mwenendo wa mashauri hayo.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dkt. Franklin Rwezimula, baadhi ya watumishi kutoka Wizara hiyo, wajumbe wa menejimenti na watumishi wa OWMS.



Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akitoa salamu za utangulizi wakati wa ziara ya Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Juma Zuberi Homera (Mb) (hayupo pichani) alipotembelea ofisi hiyo Jijini Dar es Salaam.



Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera (Mb) akiwa pamoja na viongozi Wizara na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya kuzungumza na Watumishi wa Ofisi hiyo alipotembelea Ofisi hiyo wakati wa ziara yake Jijini Dar es Salaam.

DKT. SAMIA AAGIZA SHERIA ZILIZOTAFSIRIWA KWA LUGHA YA KISWAHILI KUFIKIA WANANCHI

- Na Carine Senguji -



Mwandishi Mkuu wa Sheria, Bw. Onorius Njole akimuelezea Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan kazi na majukumu yanayotekelezwa na Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria (OCPD) wakati wa ufunguzi wa mkutano wa Chama cha Mawakili wa Serikali kinachoendelea Jijini Arusha.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amepongeza na kutambua jitihada za kuendeleza huduma za kisheria ikiwemo kazi ya kutafsiri sheria katika lugha ya kiswahili kwani hatua hii itasaidia mwananchi kuelewa sheria na haki zake.

Mhe. Rais aliyasema hayo wakati wa ufunguzi wa kikao cha Mawakili wa Serikali kilichofanyika tarehe 13, Julai 2026, jijini Arusha.

Natambua jitihada zenu za kuendeleza huduma za msaada wa kisheria ikiwemo kazi ya kutafsiri sheria katika lugha ya kiswahili na nimeambiwa kazi inakaribia kumalizika na sasa wameniomba kuja kuzindua sheria hizi kwa lugha ya kiswahili

na mimi nasema nipo tayari alisema Rais Samia kufanya hivyo," alisema Rais Samia.

Rais Samia alieleza kuwa zoezi la tafsiri ya sheria litamsaidia mwananchi kuelewa haki zake, sheria na mipaka yake.

"Hatua hii mliyochukua ni muhimu na ya kupongezwa kwani mwananchi anapo ielewa sheria anaelewa haki zake, wajibu wake, mipaka ya uhuru wake na mipaka ya mamlaka ya serikali na hii ndio maana halisi ya utawala wa sheria," aliongeza Rais Samia.

Mhe. Rais Samia alielekeza zoezi hilo lisiishie kwenye kutafsiri sheria tu bali kuhakikisha watu wanaelewa sheria hizo kwa kuwafuata walipo.

"Kazi yenu isiishie tu kuzitafsiri lakini pia muingie njiani kwenda kuzifundisha kwa watu ili wazielewe, wazifahamu na wajue mipaka ya serikali, mipaka yao na sheria za nchi yao zinasema nini, kwahiyo ni matumaini yangu kuwa hatua hizi zote mlizozichukua zitakua chachu ya kuongeza ubora, ufanisi, nidhamu na weledi katika kutoa huduma za kisheria ndani ya serikali na kwa wananchi kwa ujumla," alielekeza Mhe. Rais Samia.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliendelea kwa kusema kuwa hatua hizi pamoja na nyingine zinapaswa kuendana na malengo nchi iliyojiwekea katika dira ya taifa ya maendeleo ya 2050 ambayo utekelezaji wake umeanza mwaka huu.

Kwa upande wake Rais wa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania, Bw. Bavoo Junus alisema kuwa jumla ya sheria kuu 444 zimetafsiriwa kwa lugha ya kiswahili na zimetangazwa rasmi kupitia gazeti la serikali namba 659 la mwaka 2025.

"Kukamilika kwa zoezi hili la tafsiri kutaongeza wigo wa upatikanaji wa haki, utaongeza uwezo wa serikali kusimamia na kutekeleza sheria zake kwa ufanisi zaidi, kutaimarisha utawala wa sheria na kuongeza ufanisi wa taasisi za umma na kutekeleza kwa vitendo malengo ya dira ya taifa ya maendeleo 2050," alisema Bw. Bavoo.

SERIKALI YASAINI MKATABA WA UBIA WA UCHIMBAJI WA GESI YA HELIUM SONGWE

- Ally Masaninga -

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepiga hatua nyingine kubwa ya kihistoria katika sekta ya madini na nishati kufuatia utiaji saina wa Mkataba wa Ubia wa Uchimbaji wa Gesi ya Helium baina ya Serikali na Kampuni ya Helium One Global Limited, kupitia Kampuni ya Ubia ya Songwe Helium Limited.

Naibu Waziri wa Madini Mhe. Dkt. Steven Kiruswa aliiongoza timu ya wataalamu wa Serikali katika hafla hiyo ambayo ni mwendelezo wa sera na juhudi za Serikali ya Awamu ya SITA wa kuweka mazingira wezeshi, salama na ya kuvutia kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, huku ikilinda maslahi ya taifa na wananchi wake

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Samwel M. Maneno alishiriki hafla hiyo ya utiaji Saina kwa Mkataba huo baina ya

Serikali na Kampuni ya Helium One Global Limited iliyofanyika tarehe 2 Mei, 2026 Mkoani Songwe, ambapo kupitia Mkataba huo Serikali itamiliki asilimia 17 ya Hisa katika Kampuni ya Ubia ya Songwe Helium Limited.

Helium ni gesi ya kipekee duniani kwasababu Haina mbadala na matumizi yake ni ya kimkakati kwa maisha ya sasa ya binadamu na hutumika katika vifaa vya tiba kama MRI, uzalishaji wa vifaa vya kielektroniki na teknolojia za kidijitali, Sekta ya anga, ulinzi na tafiti za kisayansi.

Kusainiwa kwa mkataba huu kuliifanya Tanzania kuanza rasmi safari mpya ya kihistoria ya kuingia kwenye ramani ya dunia kama mzalishaji na msambazaji mkuu wa kimkakati wa gesi ya Helium, hali inayotarajiwa kuongeza fursa za kiuchumi, ajira, na mapato ya kigeni kwa taifa.



Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Samwel M. Maneno (Kushoto) akitia Saini mkataba wa Ubia kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kampuni ya Helium One Global Limited, (Kulia) ni Naibu Waziri wa Madini Mhe. Dkt. Steven Kiruswa, hafla ya utiaji saini Mkataba huo ilifanyika Mkoani Songwe.

Mradi huu mkubwa unatarajiwa kutekelezwa katika eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 480, ambapo sehemu kubwa ya mradi huo ipo katika Mkoa wa Songwe, Wilaya ya Momba, huku eneo dogo likiingia

katika Mkoa wa Rukwa. Utendaji wa mradi huu unatarajiwa kuchochea maendeleo ya miundombinu na uchumi wa kijamii kwa wananchi wa maeneo husika na nchi kwa ujumla.



Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Samwel M. Maneno (Kushoto), Naibu Waziri wa Madini Mhe. Dkt. Steven Kiruswa (wa pili kutoka kushoto), pamoja na wawakilishi kutoka Kampuni ya Helium One Global Limited, wakionyesha Mkataba wa Ubia uliosainiwa kati ya Serikali na Kampuni, Mkoani Songwe.

WATUMISHI WAPYA NPS WATAKIWA KUZINGATIA MAADILI YA UTUMISHI WA UMMA

- Na Rebecca Kwandu -



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera (Mb) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa Mafunzo elekezi ya awali kwa waajiriwa wapya wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka yaliyofanyika Jijini Arusha.

Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera aliwataka watumishi wapya wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS) kuzingatia maadili, weledi na misingi ya utumishi wa umma wanapotekeleza majukumu yao ya kila siku.

Dkt. Homera alisema hayo tarehe 19 Aprili, 2026 Jijini Arusha wakati akifunga mafunzo elekezi kwa watumishi wapya wa NPS na kuwataka kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya Serikali sambamba na kutunza siri za Serikali na kuwajibika ipasavyo katika nafasi walizopewa.

Alieleza kuwa Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika kuimarisha taasisi za haki jinai kwa kuongeza nguvu kazi ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) Sylvester Mwakitalu alisema baada ya mafunzo ya siku tano (5) yaliyohusu majukumu ya kazi, kanuni na taratibu za utumishi wa umma, waajiriwa hao wako tayari kwenda kutoa huduma za kimashtaka kwa Alisema Serikali ina matarajio makubwa kwa watumishi hao katika kuimarisha utoaji wa haki jinai nchini kupitia majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, huku akisisitiza umuhimu wa kufanya kazi kwa ushirikiano, ubunifu na nidhamu.

"Nina imani mafunzo haya yamewajengea uwezo wa kutosha kwenda kutekeleza majukumu yenu kwa bidii, weledi na kwa kuzingatia misingi ya haki na utumishi wa umma," alisema Mkurugenzi Mwakitalu.

Aidha, aliwapongeza washiriki kwa kuchaguliwa kujiunga na utumishi wa umma na kupata nafasi ya kulitumikia Taifa.

DPP Mwakitalu alieleza kuwa mafunzo hayo yalijumuisha watumishi wapya 162 wakiwemo Mawakili wa Serikali, Makatibu Sheria, Madereva, Wahasibu, Wasaidizi wa Hesabu, Watakwimu, Maafisa TEHAMA, Watunza Kumbukumbu, Waandishi Waendesha Ofisi na Afisa Habari.

katika Mkoa wa Rukwa. Utendaji wa mradi huu unatarajiwa kuchochea maendeleo ya miundombinu na uchumi wa kijamii kwa wananchi wa maeneo husika na nchi kwa ujumla.



Washiriki wa Mafunzo elekezi ya awali kwa waajiriwa wapya wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wakifuatilia kwa umakini mada mbalimbali zilizowasilishwa kwenye mafunzo hayo yaliyofanyika Jijini Arusha.

WAKILI MKUU WA SERIKALI AKUTANA NA RAIS WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU - Na Prisca Ulomi -



Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (kushoto) akisalimiana na Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Mhe. Jaji Blaise Tchikaya alipowasili Ofisini kwake kwa ajili ya kujitambulisha na kuona namna Mahakama hiyo inavyofanya kazi Jijini Arusha.

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi alikutana na Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Mhe. Jaji Blaise Tchikaya na kufanya mazungumzo nae Ofisini kwake jijini Arusha kwa lengo la kujitambulisha kwa Rais huyo ili kuendeleza ushirikiano uliopo baina ya Ofisi hizo mbili.

Dkt. Possi alifika Ofisini kwa Mhe. Jaji Tchikaya baada ya ufunguzi wa mwaka wa Mahakama hiyo uliofanyika kwenye ukumbi wa Mahakama hiyo jijini Arusha na uzinduzi wa maadhimisho ya miaka 20 ya Mahakama hiyo.

Dkt. Possi alisema kuwa Tanzania kama nchi mwenyeji na kwa kuzingatia majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeona ni muhimu kufika na kujitambulisha, pamoja na kuona namna Mahakama hiyo inavyofanya kazi.

“Ofisi ina jukumu la kuendesha mashauri ya Serikali, utakutana na Ofisi hii katika kuendesha mashauri na Tanzania imekuwa na idadi ya mashauri ambayo yanaendeshwa na Mahakama hii na nimeona nifike tuzungumze ili kukuhakikishia ushirikiano na Ofisi hii kwa niaba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika uendeshaji wa mashauri kwenye Mahakama hii,” alisisitiza Dkt. Possi.

Pia, Dkt. Possi aliongeza kuwa kama nchi mwenyeji yuko tayari kupokea ujumbe kwa niaba ya Serikali ili kuweza kuwasilisha kwa kuwa Ofisi imekuwa ikishirikiana na Mahakama hiyo.

Naye, Mhe. Jaji Tchikaya, alisema kuwa ni kweli mashauri mengi yanayoendeshwa na Mahakama hiyo yanatokea Tanzania na hii inaonesha kuwa uwepo wa Mahakama hii Tanzania inawapa fursa wadau kutumia Mahakama hii baada yakupita kwenye Mahakama za ndani.

Mhe. Jaji Tchikaya aliongeza kuwa hii inaonesha Tanzania inaruhusu u wananchi

wake kutafuta na kupata haki kupitia kwenye vyombo vya kimataifa ikiwemo Mahakama hii ambapo ni ushahidi wa utekelezaji wa Mkataba na Itifaki ya Haki za Binadamu wa Umoja wa Afrika.

Katika hatua nyingine, Mhe. Jaji Tchikaya aliomba ushirikiano wa Dkt. Possi na msukumo katika ujenzi wa Ofisi ya Mahakama hiyo ili uweze kukamilika na aliishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanikisha kuanza kwa ujenzi wa Ofisi ya Mahakama hiyo jijini Arusha.

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (kushoto), akimkabidhi Jarida la Wakili Mkuu Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Mhe. Jaji Blaise Tchikaya alipotembelea Mahakama hiyo Jijini Arusha



Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akiwa kwenye picha ya pamoja na baadhi ya Watumishi wa Ofisi hiyo baada ya kutembelea Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kwa lengo la kujitambulisha na kujionea namna Mahakama hiyo inavyotekeleza majukumu yake Jijini Arusha.

SERIKALI KUIMARISHA UPATIKANAJI WA HAKI KUPITIA KAMPENI YA MSAADA WA HUDUMA YA KISHERIA - AWAMU YA PILI

- Na Michael Mhina -



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi akisikiliza maelezo kuhusiana na majukumu ya OCPD alipotembelea banda la Ofisi hiyo wakati wa uzinduzi wa awamu ya pili ya kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia, uliofanyika Zanzibar.

Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria (OCPD) ni miongoni mwa taasisi zinazoshiriki kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi katika Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia Awamu ya Pili ambayo ilizinduliwa tarehe 20 Juni 2026 katika Uwanja wa Dole, Kizimbani Zanzibar, ambapo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mh. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, alimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika uzinduzi huo rasmi.

Katika hafla hiyo, Mh. Dkt. Mwinyi alitembelea banda la OCPD na kupata maelezo kuhusu huduma mbalimbali za

kisheria zinazotolewa na ofisi hiyo kwa wananchi, ikiwa ni sehemu ya mchango wake katika kuhakikisha wananchi wanapata elimu na usaidizi wa kisheria kwa urahisi na kwa wakati.

Katika uzinduzi huo, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali, Bw. Onorius Njole, alishiriki pamoja na viongozi wengine wa Serikali na taasisi mbalimbali za Sekta ya Sheria ikiwa ni pamoja na kutembelea mabanda ya taasisi mbalimbali zinazoshiriki Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia ili kujionea huduma zinazotolewa kwa wananchi na kuimarisha ushirikiano katika utoaji wa huduma za msaada wa kisheria nchini.

Akisoma hotuba kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mhe. Dkt. Mwinyi alisema Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuhakikisha huduma za msaada wa kisheria zinawafikia wananchi wengi zaidi nchini.

"Serikali imechukua hatua za makusudi za kuimarisha huduma za msaada wa kisheria, kwa kutunga sera itakayotoa mwongozo wa usimamizi na uendeshaji wa huduma za msaada wa kisheria nchini, hatua itakayoleta mabadiliko makubwa ya kimtazamo na kimfumo katika utoaji wa huduma za msaada wa kisheria," alisema Mh. Dkt. Mwinyi.

Aliongeza kuwa hatua hiyo itawezesha wananchi kupata huduma za kisheria kwa urahisi zaidi huku ikichangia kuimarisha upatikanaji wa haki, kuimarisha utawala bora na kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu haki na wajibu wao kwa mujibu wa sheria.

Kwa upande wake, Waziri wa Katiba na Sheria, Mh. Dkt. Juma Zuberi Homera, alisema Wizara itaendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali ili kuhakikisha huduma za msaada wa kisheria zinawafikia wananchi katika maeneo yote ya nchi.

Mhe. Jaji Tchikaya aliongeza kuwa hii inaonesha Tanzania inaruhusu u wananchi wake kutafuta na kupata haki kupitia kwenye vyombo vya kimataifa ikiwemo Mahakama hii ambapo ni ushahidi wa utekelezaji wa Mkataba na Itifaki ya Haki za Binadamu wa Umoja wa Afrika.

Mwananchi akipokea elimu ya Uandishi wa Sheria kutoka kwa Watumishi wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria (OCPD), alipotembelea banda la Ofisi hiyo katika kliniki ya awamu wa pili ya Msaada wa kisheria ya Mama Samia, iliyofanyika Jijini Dodoma.

Katika hatua nyingine, Mhe. Jaji Tchikaya aliomba ushirikiano wa Dkt. Possi na msukumo katika ujenzi wa Ofisi ya Mahakama hiyo ili uweze kukamilika na ameishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanikisha kuanza kwa ujenzi wa Ofisi ya Mahakama hiyo jijini Arusha.

"Wizara kwa kushirikiana na taasisi zingine katika utekelezaji wa kampeni, itahakikisha huduma zinasogezwa karibu katika maeneo mbalimbali nchini," alisema Mh. Dkt. Homera.

Alisema kampeni hiyo ni sehemu ya jitihada za Serikali za kuongeza upatikanaji wa haki kwa wananchi kwa kuwafikisha huduma za kisheria moja kwa moja katika maeneo wanayoishi na kufanyia shughuli zao za kila siku.

Uzinduzi wa Awamu ya Pili ya Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia ulizikutanisha taasisi mbalimbali za sekta ya sheria kutoka Tanzania Bara na Zanzibar zikiwa na lengo la kutoa elimu ya sheria, ushauri wa kisheria na huduma nyingine zinazochangia kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wananchi.

Kupitia ushiriki wake katika kampeni hiyo, OCPD imeendelea kutekeleza wajibu wake wa kusogeza huduma za kisheria karibu na wananchi kwa kutoa elimu kuhusu masuala mbalimbali ya sheria pamoja na ushauri wa kisheria unaowasaidia wananchi kuelewa na kulinda haki zao kwa mujibu wa sheria.



MAWAKILI WA SERIKALI WAHITIMU MAFUNZO YA AWALI YA PROGRAMU YA CP3P

- Na Lela Muhaji -



Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Samwel M. Maneno akizungumza wakati wa kufunga mafunzo kwa Mawakili wa Serikali kuhusu utoaji wa Ithibati ya Kimataifa katika miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, yaliyofanyika Jijini Dodoma.

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Samwel M. Maneno, alifunga mafunzo ya awali ya Programu ya CP3P ambao ni mpango wa Uthibitishaji wa APMG PPP yaliyotolewa kwa Mawakili wa Serikali katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mafunzo hayo yalilenga kuongeza ujuzi na kutoa ithibati ya Kimataifa kwa Mawakili hao kuhusu miradi ya ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Mpango wa Uthibitishaji wa APMG PPP-CP3P ni uvumbuzi wa Benki ya Maendeleo ya Asia (ADB), Benki ya Ulaya ya Ujenzi na Maendeleo (EBRD), Jumuiya ya Kimataifa Benki ya Maendeleo ya Marekani (IDB), Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IsDB), Mfuko wa

Uwekezaji wa Kimataifa (MIF) na Benki ya Dunia (WBG).

Akizungumza wakati akihitimisha mafunzo hayo, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema mafunzo hayo yalilenga kuwaongezea ujuzi mawakili katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuimarisha utendaji wa ubia hapa nchini utakaoendana na Utekelezaji wa DIRA, 2050.

Alifafanua kuwa Uhitimu na Ufaulu wa hatua zote 3 za Mafunzo hayo ni uthibitisho na kitambulisho dhahiri cha kuonyesha uwezo wa Mawakili hao katika Miradi ya Ubia kwa viwango vya kimataifa.

"Kwa ujuzi huu, Mwakili hawa wataweza kutoa ushauri wa kisheria ipasavyo katika hatua za maandalizi ya mradi na hasa uandaaji wa nyaraka mbalimbali ukiwemo mikataba ya ubia na hivyo kuhakikisha Miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi inakuwa na tija na kufikia malengo yaliyokusudiwa." Alisema Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Aidha, Mhe. Maneno alieleza kuwa mafunzo hayo ni muhimu kwa Mwakili wa Serikali na umma kwa ujumla katika kipindi hiki ambacho Serikali imeanza rasmi utekelezaji wa Dira 2050; kuvutia uwekezaji na ubia katika miradi mbalimbali ya maendeleo.

"Kupitia lthibati na mafunzo haya tunaamini kuwa mchango wa OAG na uwezo wa Serikali katika kuchakata, kununua na kusimamia miradi ya ubia hapa nchini utaimarika zaidi." Alisema Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kwa upande wake, Wakili wa Serikali Bi. Mwamini Kilongola kwa niaba ya washiriki wa mafunzo hayo aliushukuru uongozi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuwezesha kufanyika kwa mafunzo hayo ambayo yatafanya wahitimu kutambulika na jumuiya ya kimataifa kama wataalam wa PPP, kuongeza ujuzi katika Upekuzi wa Mikataba ya Ubia na hivyo kusaidia katika utekelezaji wa Dira, 2050.

Mafunzo hayo ni mwendelezo wa mikakati ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakikisha kuwa Watumishi wake wanaongeza ujuzi utakaowasaidia katika utekelezaji wa majukumu yao.



Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Samwel M. Maneno (katikati walioketi) katika picha ya pamoja na Mwakili wa Serikali na Mkufunzi wa mafunzo ya Utoaji wa lthibati ya Kimataifa kwa Mwakili wa Serikali kuhusu miradi ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, yaliyofanyika Jijini, Dodoma.

MAGARI 21 KUONGEZA KASI YA UTENDAJI NPS

- Na Rebecca Kwandu -



Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera (Mb) akikabidhi magari 21 ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwenye hafla ya makabidhiano ya magari hayo iliyofanyika Jijini Dar es salaam.

Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera, amekabidhi magari 21 yatakayosaidia kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika Ofisi za Mashtaka za Wilaya nchini.

Akizungumza wakati wa hafla ya makabidhiano iliyofanyika tarehe 03 Mei, 2026 Jijini Dar es Salaam, Mhe. Dkt. Homera alisema kuwa magari hayo ni nyenzo muhimu zitakazorahisisha utekelezaji wa majukumu ya kila siku, hususan katika uendeshaji wa mashauri ya jinai.

“Ni imani yangu kuwa upatikanaji wa vitendea kazi hivi utaongeza ufanisi na kasi ya utendaji wa kazi za mashtaka. Hivyo, ni wajibu wetu kufanya kazi kwa bidii, kwa

ushirikiano, na kuhakikisha mashauri yote ya jinai yanakamilika kwa wakati,” alisema Mhe. Dkt. Homera.

Alieleza kuwa katika kipindi cha miaka nane, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS) imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hatua iliyochangia kupunguza mlundikano wa mashauri mahakamani pamoja na malalamiko kutoka kwa wananchi. Aidha, juhudi hizo zimepelekea kupungua kwa idadi ya mahabusi na wafungwa magerezani.


Vilevile, Waziri Homera alibainisha kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anatambua na kuthamini mchango wa NPS

katika kuchochea maendeleo ya nchi hivyo upatikanaji wa magari hayo 21 ni sehemu ya juhudi za kuhakikisha huduma za mashtaka zinawafikia wananchi kwa wakati.

“Katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali inatarajia kununua magari mengine 30 kwa ajili ya Ofisi za Mashtaka za Wilaya 30 ambazo bado hazijapatiwa magari ili kuendelea kuboresha mazingira ya kazi na utoaji wa huduma za kimashtaka,” alisema Dkt. Homera.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mashtaka, Bw. Sylvester Mwakitalu, alisema kuwa ujio wa magari hayo 21 utapunguza kwa kiasi kikubwa changamoto ya uhaba wa vitendea kazi katika ofisi za mashtaka za wilaya, hususan kwa zile zilizokuwa hazina magari.

Pia aliwataka madereva watakaokabidhiwa magari hayo kuyatunza na kuyatumia kwa uangalifu ili yaweze kudumu na kuleta tija ya utoaji huduma bora za mashtaka kwa wakati kama ilivyokusudiwa.



Magari mapya ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka yaliyokabidhiwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera (Mb) kwenye hafla ya makabidhiano iliyofanyika Jijini Dar es salaam.

JAJI MARUMA AHIMIZA MABORESHO YA MIFUMO YA KISHERIA KUWAVUTIA WANAWAKE SEKTA YA USULUHISHI

- Na Prisca Ulomi -



Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kituo cha Usuluhishi, Mhe. Zahra Maruma akizungumza na washiriki wa kongamano la ushirikishwaji wa wanawake kwenye utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala lililofanyika Jijini Dar es Salaam.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kituo cha Usuluhishi, Mhe. Zahra Maruma alisema kuboreshwa kwa mifumo ya kisheria na kisera itakayowawezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala (ADR) kutachangia kujenga jamii yenye misingi imara na ustawi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam akiwa mgeni rasmi kwenye uzinduzi wa Wiki ya Kongamano la Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro, Jaji Maruma, alisema ukosefu wa maboresho katika mifumo hiyo umechangia kuwepo kwa pengo kubwa la ushiriki wa wanawake ikilinganishwa na wanaume wanaoshika nafasi nyingi za uamuzi.

"Wanawake ni wazuri katika usuluhishi kwa sababu ni wavumilivu na wasikivu; tukiboresha mifumo ya kisheria na kisera, wataweza kutumia fursa zilizopo na kusaidia kujenga jamii yenye misingi imara na ustawi," alisema Jaji Maruma.

Alisema hatua hiyo ya maboresho haitawanufaisha wanawake pekee, bali pia ni utekelezaji wa Dira ya Taifa 2050, inayolenga kuimarisha usawa wa kijinsia nchini.

Mhe. Jaji Maruma aliongeza kuwa, utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala ni rafiki zaidi kuliko mfumo wa kawaida wa mahakamani, kwani huokoa muda, hupunguza gharama na kujenga maelewano kwa kuwa migogoro inapojitokeza huacha nyufa katika jamii,

lakini usuluhishi hujenga maelewano hivyo mwanamke akiwezesha ana nafasi kubwa ya kufanikisha hilo.

Tanzania ina fursa ya kuwa kinara barani Afrika katika matumizi ya usuluhishi, akieleza kuwa takribani sheria 12 zinatatambua na kuruhusu matumizi ya njia hizo ambapo mwaka 2025, zaidi ya mashauri 386 yalimalizwa kupitia usuluhishi mahakamani na zaidi ya mashauri 500 yakamalizwa nje ya mahakama kupitia mabaraza.

Kwa upande wake, Makamu wa Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Bi. Laetitia Ntagazwa alisema chama hicho kimeanzisha Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

"Moja ya jukumu letu ni kulinda umma wa Watanzania. Kupitia kongamano hili tunalenga kuongeza ushiriki wa wanawake, kwani bado kuna pengo kubwa; Afrika, wanawake ni asilimia 28 tu katika sekta hii," alisema Wakili Ntagazwa.

Alisema, wanawake waliothibitishwa kama wasuluhishi ni 82 pekee, ikilinganishwa na wanaume 444, hali inayoonyesha umuhimu wa kuongeza juhudi za kuwawezesha wanawake.



Mkurugenzi wa Idara ya Usuluhishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bw. Saddy Sevingi akitoa salamu za Ofisi hiyo wakati wa ufunguzi wa kongamano la ushirikishwaji wa wanawake kwenye utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala lililofanyika Jijini Dar es Salaam.

Naye, Mwenyekiti wa Bodi ya Kituo cha Kimataifa Cha Usuluhishi kwa Njia Mbadala, Wakili Godson Nyange alisema elimu, makongamano na ushirikiano kati ya Serikali na wadau ni muhimu katika kuongeza ushiriki wa wanawake.

"Tumeandaa kongamano hili kuwajengea uwezo wanawake na kuujulisha umma kuhusu huduma za usuluhishi ili wananchi wenye changamoto wajitokeze kupata suluhisho," alisema Godson Nyange.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Usuluhishi kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bw. Saddy Sevingi alisema Ofisi hiyo inaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuboresha Sekta hiyo kupitia mafunzo na kubadilishana uzoefu.

"Tuna idara maalumu cha usuluhishi na tunaendelea kushirikiana na wadau ili kuongeza ufanisi katika utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala," alisema Sevingi.

Kongamano hilo lilijumuisha watunga sera, wanasheria na viongozi wa biashara liliandaliwa na Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi wa Migogoro Tanzania (TIAC), kwa kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria liliongozwa na kaulimbiu isemayo **Kutoka Majadiliano hadi Hatua: Kuendeleza Ushirikishwaji wa Wanawake katika Utatuzi Migogoro kwa Njia Mbadala.**



Baadhi ya washiriki wa kongamano la ushirikishwaji wa wanawake kwenye utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala wakimsikiliza Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mhe. Zahra Maruma (hayupo pichani) wakati akifungua kongamano hilo lililofanyika Jijini Dar es Salaam.

OCPD NA MIKAKATI YA UTEKELEZAJI WA DIRA 2050

- Na Michael Mhina -



Mkurugenzi wa Divisheni ya Urekebu wa Sheria, Tafiti na Mafunzo, Bi. Rehema Katuga, pamoja na Menejimenti ya Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria (OCPD) wakitoa mafunzo ya kuimarisha uelewa kwa wanahabari kuhusiana na majukumu ya Ofisi ya OCPD.

Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria inaendelea kuwajengea uwezo Watumishi wake kwenye maeneo mbalimbali ya kimkakati ili kuwezesha kufanya uchambuzi na mapitio ya sheria mbalimbali zinazohitaji maboresho au kuandikwa upya ili kurahisisha na kuwezesha utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Mkurugenzi wa Divisheni ya Urekebu wa Sheria, Tafiti na Mafunzo, Bi. Rehema Katuga alibainisha hayo wakati akimwakilisha Mwandishi Mkuu wa Sheria, kwenye mafunzo yaliyoandaliwa na ofisi hiyo kwa ajili ya kuwajengea uelewa wanahabari kuhusu majukumu yake Jijini Dodoma.

“Moja ya majukumu yetu ni kuhakikisha kuwa sheria zinazoandikwa zinaakisi na kusaidia utekelezaji wa sera na mipango ya serikali, ikiwemo Dira ya 2050,” alisema.

Kutokana na Dira ya 2050 kulenga uchumi wa kidijitali, Bi. Katuga aliongeza kuwa katika kipindi cha miaka 25 ijayo, shughuli nyingi za biashara na uendeshaji wa shughuli za kiuchumi zitafanyika kidijitali, ikiwemo matumizi ya akili bandia (AI).

Kwa sababu hiyo, OCPD imeweka kipaumbele katika kujenga uwezo wa watumishi wake ili waweze kumudu majukumu yanayohusiana na maeneo haya mapya.

“Iwapo mifumo ya kidijitali itatumika kwa wingi, ni lazima kuwe na maandalizi ya kutosha ya kushughulikia kazi za kisheria kutoka wizara zinazohitaji mapitio au uandishi wa sheria,” alisema.

Pia alieleza kuwa Ofisi imekamilisha zoezi la kutafsiri sheria zote 444 kwa Kiswahili, hatua inayolenga kuimarisha upatikanaji wa haki, usawa na maendeleo kwa Watanzania.

Bi. Katuga alisema OCPD ndiyo taasisi yenye dhamana ya kuandaa, kupitia na kuchapisha miswada ya serikali, kanuni na nyaraka nyingine za kisheria, ambapo pia hufanya kazi kwa kushirikiana na Bunge na Mahakama ili kuhakikisha sheria zinapatikana kwa lugha rahisi, kulingana na lengo la kutoa sheria bora kwa wote.

Alisema zoezi la tafsiri limekamilika na sheria zote 444 zimewasilishwa kwa mamlaka husika, na zinatarajiwa kuanza kutumika hivi karibuni.

“Moja ya mafanikio yetu makubwa ni kutafsiri sheria zetu kwa Kiswahili. Hii itarahisisha Watanzania kusoma na kuelewa sheria mbalimbali,” alisema.

Aliongeza kuwa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria ina jukumu muhimu katika kubadilisha sera kuwa sheria zinazokuza upatikanaji wa haki, usawa na maendeleo.

Awali, Mkurugenzi wa Divisheni ya Tafsiri, Bw. Said Nzori, alisema Ofisi imefanikiwa kuandaa miongozo itakayosaidia uandaaji wa kamusi ya kisheria ya Kiswahili pamoja na kusaidia utekelezaji wa maelekezo ya kutafsiri sheria zote kwa Kiswahili.

Akizindua Dira ya 2050 mwaka jana, Rais Samia Suluhu Hassan alitoa maelekezo mbalimbali kwa taasisi za umma ili kuimari- sha jitihada za kufikia uchumi wa dola trilion moja katika kipindi cha miaka 25 ijayo.

Rais aliagiza wizara zote kupitia na kusasisha sera zao ili ziendane na Dira ya 2050, Pamoja na kuielekeza Tume ya Mipango, kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, kuandaa mpango wa muda mrefu wa utekelezaji kabla ya uzinduzi rasmi unaotarajiwa kufanyika Julai 2026.

Aidha, Tume ya Mipango imepewa jukumu la kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha unaendana na malengo ya muda mrefu ya maendeleo ya nchi.

Rais Samia pia alielekeza Tume ya Kurekebisha Sheria pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kufanya mapitio na kupendekeza maboresho ya kisheria yatakayoweza utekelezaji mzuri wa Dira hiyo.

**“CHAMA BORA CHA KITAALUMA NI KILE
KINACHOSAIDIA SERIKALI KUFIKIA
MALENGO YAKE”
– MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI
- Na Lela Muhaji -**



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari akizungumza wakati wa Ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa TPBA uliofanyika Jijini Arusha.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye ni Mlezi wa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania (TPBA) Mhe. Hamza S. Johari alisema kuwa Chama cha Mawakili wa Serikali, kitaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuisaidia Serikali kufikia malengo mbalimbali ambayo Serikali imejiwekea.

Mhe. Johari aliyasema hayo wakati wa Ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Chama cha Mawakili wa Serikali wa Tanzania (TPBA), Jijini Arusha tarehe 13 Julai, 2026.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema kuwa, Chama cha Mawakili wa Serikali nchini, kimeendelea kukua, kuimarika na kuwa jukwaa muhimu la kubadilishana uzoefu wa kitaaluma, kujenga uwezo wa

wanachama wake, kuimarisha maadili ya kazi, na kukuza ushirikiano miongoni mwa Wanasheria wa Serikali wanaotekeleza majukumu yao katika taasisi mbalimbali za umma.

“Chama Bora cha Kitaaluma ni kile kinachosaidia Serikali katika kufikia malengo yake na sio kuitikisa au kuiyumbisha Serikali.” Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Akieleza juu ya malengo ya Mkutano huo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema kuwa Mkutano huo unalenga kutoa fursa kwa wanachama kujadili masuala mbalimbali yanayohusu chama hicho, maendeleo ya Sekta ya Sheria kwa ujumla pamoja na kufanya uchaguzi wa viongozi wa Chama cha Mawakili wa Serikali.

Aidha, Mhe. Johari alisema kuwa pamoja na mafanikio mengine mengi yaliyofikiwa, Chama hicho kimeweza kuzindua Kitabu cha Falsafa ya Sheria ya Mama Samia ambacho kinaeleza kwa kina namna maboresho mbalimbali yaliyofanyika katika Sekta ya Sheria yalivyoleta mabadiliko katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Alieleza kuwa, Kitabu hicho kinaelezea mwelekeo ulioonekana katika Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutumia sheria, sera, taasisi na mifumo ya utekelezaji kujenga mazingira ya maridhiano, uwekezaji, uwazi, huduma, haki, na maendeleo ya wananchi.

“Mwelekeo huu haukuonekana katika sekta moja tu. Umeonekana katika kodi na mapato, uwekezaji, nishati, ardhi, TEHAMA, utalii, elimu, msaada wa kisheria, hifadhi ya jamii, utawala bora, PPP na maeneo mengine mengi.” Alisema Mhe. Johari

Katika hatua nyingine, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ina wajibu wa kuishauri Serikali kuhusu masuala ya sheria, mikataba, utungaji wa sheria, tafsiri ya sheria, na kulinda maslahi ya umma.

“Ushauri wa sheria una thamani zaidi pale unaposaidia Serikali kufanya maamuzi yanayolinda maslahi ya taifa, yanayoleta maendeleo, yanayopunguza migogoro, yanayovutia uwekezaji na yanayowezesha wananchi kupata haki kwa wakati na kupata huduma bora.” Alisema Mhe. Johari.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, alisema kuwa utekelezaji wa Dira ya Taifa 2050 unahitaji uwepo wa sheria bora zinazoshabihiana na Dira na nguvu za

kiuchumi, ambapo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea kutekeleza maelekezo ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kushabihisha sheria mbalimbali na Dira 2050.

Mhe. Johari alieleza kuwa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kuratibu na kushirikiana na wadau wote katika kuboresha sheria, kusimamia upatikanaji wa haki kwa wakati, kuimarisha ushauri wa kisheria kwa Serikali, kusimamia mikataba, na kuhakikisha kuwa sheria zinaendelea kuwa chombo cha maendeleo ili hatimaye malengo ya Dira 2050 yaweze kufikiwa.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali alimshukuru, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyoendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi katika Sekta ya Sheria hususan Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

“Mhe. Rais tunaendelea kukushukuru kwa namna ambavyo unaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kweli tunakushukuru sana sasa hivi mazingira yetu yameboreshwa sana.” Alisema Mhe. Johari.

Mkutano Mkuu wa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania (TPBA) uliofunguliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ulifanyika kwa siku mbili kuanzia tarehe 13 hadi 14 Julai, 2026 na ulibeba Kauli Mbiu isemayo *“Haki, Wajibu na Utawala wa Sheria ni Msingi wa Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050”*.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari (kushoto) na Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera wakati wa Ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania (TPBA), uliofanyika Jijini Arusha.



Mawakili wa Serikali wakifuatilia mada mbalimbali wakati wa Mkutano wa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania (TPBA), uliofanyika Jijini Arusha.

DKT. HOMERA APONGEZA USIMAMIZI MZURI WA UJENZI WA JENGO LA NPS MKOA WA SINGIDA

- Na Rebecca Kwandu -



Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera (Mb) akikagua hatua mbalimbali za maendeleo ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Mkoani wa Singida.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dkt. Juma Zuberi Homera, alifanya ziara ya kikazi katika mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS) Mkoa wa Singida, kwa lengo la kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo muhimu unaotekelezwa na Serikali.

Katika ziara hiyo Waziri Dkt. Homera alipata fursa ya kukagua hatua mbalimbali za ujenzi wa jengo hilo na kujionea maendeleo yaliyofikiwa hadi sasa.

Akizungumza mara baada ya kufanya ukaguzi huo, Dkt. Homera alimpongeza Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Bw. Sylvester Mwakitalu, pamoja na uongozi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa usimamizi mzuri wa mradi huo unaolenga kuboresha utoaji wa haki kwa wakati.

Dkt. Homera alisema kukamilika kwa jengo hilo kutaboresha kwa kiasi kikubwa mazingira ya kazi kwa Waendesha Mashtaka mkoani Singida, hatua itakayoongeza ufanisi, uwajibikaji na kasi ya utoaji wa huduma za mashtaka kwa wananchi.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati na kwa ubora unaostahili, kwa kuzingatia thamani ya fedha za umma zilizotolewa na Serikali chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Bw. Sylvester Mwakitalu, alimshukuru Dkt. Juma Homera kwa ushirikiano unaotolewa na Wizara ya Katiba na Sheria katika kuboresha miundombinu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

Mwakitalu alieleza kuwa ujenzi wa jengo hilo ni sehemu ya mkakati wa Serikali wa kuimarisha utendaji wa taasisi za haki jinai na kuhakikisha huduma za mashtaka zinawafikia wananchi kwa karibu zaidi.

Bw. Mwakitalu aliongeza kuwa mara baada ya kukamilika, jengo hilo litasaidia kupunguza changamoto ya uhaba wa ofisi, kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi pamoja na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za mashtaka kwa wananchi mkoani Singida.



Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Juma Homera (Mb) akikagua hatua mbalimbali za maendeleo ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Mkoani Singida.

SEKTA YA SHERIA NI MSINGI WA UCHUMI WA NCHI

- Na Prisca Ulomi -



Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera (Mb) akizungumza na Mawakili wa Serikali wakati akifungua mafunzo kwa Mawakili hao yaliyofanyika Jijini Arusha.

Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera (Mb) alifungua mafunzo ya Mawakili wa Serikali yaliyohusisha Mawakili wa Serikali wa kutoka katika Wizara, Idara, taasisi za Serikali, Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa wa Tanzania Bara na Zanzibar ambayo yalifanyika jijini Arusha. Mafunzo hayo yaliandaliwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na yalifanyika kwa siku tatu kuanzia tarehe 18 hadi tarehe 20 Mei, 2026. Mafunzo hayo yaliongozwa na kauli mbiu isemayo, *"Kulitumikia Taifa katika uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi ili kulinda maslahi mapana ya taifa kwa ajili ya kesho."*

Mhe. Dkt. Homera alisema kuwa Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria inaamini

kwamba hakuna maendeleo endelevu bila mfumo imara wa kisheria na wala hakuna uchumi shindani bila utawala bora. Wizara inaamini kuwa Sekta ya Sheria siyo tu ni mhimili wa utawala bora bali ni miongoni mwa miundombinu isiyoonkana inayoshikilia misingi ya kiuchumi ya nchi.

Aliongeza kuwa Dira 2050 imeweka misingi yake katika Sekta ya Sheria ambayo ni utawala, amani, usalama na utulivu. Kwa kuzingatia kuwa katika kipindi hiki cha ushindani wa kimataifa na kiuchumi, pamoja na mambo mengine taifa linahitaji watu wake walio imara katika kusimamia sheria zitakazoleta amani, utulivu, maendeleo ya kiuchumi kwa jamii na taifa kwa ujumla.

"Hivyo, ni lazima kwa Mawakili wa Serikali ambao ndio watekelezaji namba moja wa Dira 2050 kuwa imara katika kushauri, kutetea na kulinda rasilimali na maslahi ya Taifa hili. Niipongeze Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuandaa mafunzo haya kwa Mawakili ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Sheria inashikilia misingi ya kiuchumi ya nchi," alifafanua Mhe. Dkt. Homera.

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi alisema kuwa lengo la Ofisi kutoa mafunzo hayo ni kuendelea kuwanoa Mawakili ili kuwa askari wa kalamu mahiri katika kulinda maslahi ya taifa tangu hatua ya awali ya uandaaji wa mikataba, usimamizi wa mikataba na usuluhishi wa migogoro kabla na baada ya kuwasilisha shauri katika Mahakama na Mabaraza.

Dkt. Possi alisema kuwa katika kipindi cha mwezi Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imepata mafanikio mbali mbali ikiwemo uendeshaji wa mashauri 641 ya madai yaliyohitimishwa na kushinda mashauri 565 ambayo ni sawa na asilimia 88.1 ya mashauri yaliyomalizika na kuokoa jumla ya shilingi bilioni 316.28 ambazo Serikali ingelipa endapo ingeshindwa mashauri hayo.



Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akizungumza na Mawakili wa Serikali wakati wa Mafunzo kwa Mawakili hao yaliyofanyika Jijini Arusha.

Pia, Ofisi ilihitimisha mashauri 18 ya usuluhishi na kuiwezesha Serikali kuokoa shilingi bilioni 6.8 na dola za Marekani milioni 418.17 ambazo ni sawa na shilingi triloni 1.09 ambazo Serikali ingelipa endapo ingeshindwa mashauri hayo. *"Hivyo, jumla ya shilingi triloni 1.35 zimeokolewa katika uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi katika kipindi tajwa hapo juu ambapo Serikali ingeshindwa tungelipa pesa hizo,"* alifafanua Dkt. Possi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb) alitoa wito kwa Mawakili wa Serikali wasome na kuzingatia utekelezaji wa Dira 2050 ili kuhakikisha nchi inakuwa na amani, utulivu na misingi thabiti ya utawala wa sheria na watumie fursa ya mafunzo haya kujadiliana namna ya kutetea na kulinda maslahi ya taifa nje ya mahakama.

Naye Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo alisema kuwa Mawakili hao watapatiwa mafunzo na wataalam wabobezi wa Sheria za Usafiri wa Anga, Uandishi wa Sheria, Sheria za Kodi katika Gesi, Madini na Mafuta, Usimamizi wa Mikataba na Mamlaka ya Usikilizaji wa Rufaa za Zabuni ; pamoja na Uendeshaji na Usikilizaji wa Mashauri ya Madai na Usuluhishi.



Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera (Mb) akiwa kwenye picha ya pamoja na Wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya kufungua mafunzo kwa Mawakili hao yaliyofanyika Jijini Arusha.

SERIKALI KUONGEZA WIGO WA UPATIKANAJI WA MIKOPO KWA WANANCHI

- Na Michael Mhina -



Kaimu Mkurugenzi wa Divisheni ya Uandishi wa Sheria, Bw. Nicodemus Chuwa akizungumza kuhusiana na Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana ya Mali Zinazohamishika wa Mwaka 2026.

Serikali imewasilisha Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana ya Mali Zinazohamishika wa mwaka 2026, unaolenga kurahisisha upatikanaji wa mikopo kwa wananchi, hususan wafanyabiashara wadogo na wa kati, wakulima na wajasiriamali ambao mara nyingi hukosa dhamana za mali zisizohamishika kama ardhi au nyumba.

Akizungumza kuhusu umuhimu wa Muswada huo, Kaimu Mkurugenzi wa Divisheni ya Uandishi wa Sheria, Bw. Nicodemus Chuwa, alisema kuwa hatua hiyo ni sehemu ya jitihada za Serikali za kuboresha mfumo wa kifedha na kuongeza ushiriki wa wananchi katika shughuli za kiuchumi. Alisema Muswada huo

utawezesha matumizi ya mali zinazohamishika kama dhamana ya mikopo katika taasisi za kifedha.

“Muswada wa kisheria utawezesha wananchi kutumia mali zinazohamishika kama dhamana ya mikopo na hivyo kupanua fursa za upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya kukuza biashara na shughuli za uzalishaji,” alisema Bw. Chuwa.

Kwa mujibu wa Muswada huo, mali zinazohamishika ni zile zinazoweza kuhamishwa kutoka sehemu moja kwenda nyingine bila kuharibu asili yake. Mali hizo zinajumuisha magari, mitambo, samani, vifaa vya kielektroniki, mifugo, mazao ya kilimo, hisa pamoja na mali nyingine

zitakazotambuliwa rasmi kupitia notisi itakayotangazwa na Benki Kuu ya Tanzania.

Aidha, Muswada unapendekeza kuanzishwa kwa Masijala Maalumu ya Usajili wa Dhamana za Mali Zinazohamishika itakayokuwa chini ya Benki Kuu ya Tanzania. Mfumo huu utawezesha usajili na uhifadhi wa taarifa za dhamana, kuthibitisha umiliki wa mali, pamoja na kuondoa hatari ya mali moja kutumika kama dhamana mara mbili au zaidi bila taarifa rasmi.

Bw. Chuwa aliongeza kuwa uwepo wa sheria hiyo utaimarisha imani ya taasisi za fedha katika utoaji wa mikopo kwa kutumia mali zinazohamishika, hatua itakayoweze- sha wananchi wengi zaidi kupata mitaji ya kuendeleza shughuli zao za kiuchumi.

“Kupitia mfumo huu mpya, wafanyabiashara wadogo, wakulima na wajasiriamali watakata nafasi ya kupata mikopo bila vikwazo vya dhamana za mali zisizohamishika,” alisisitiza.

Hata hivyo, wataalamu wa masuala ya uchumi wanaamini kuwa muswada huo ukipitishwa na kutekelezwa ipasavyo utaongeza uwekezaji, kukuza biashara ndogo na za kati, pamoja na kuimarisha mzunguko wa fedha katika uchumi wa nchi. Walisisitiza umuhimu wa utoaji wa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya mali zinazohamishika kama dhamana ili kuhakikisha fursa hiyo inawanufaisha wananchi wengi zaidi.



Kaimu Mkurugenzi wa Divisheni ya Uandishi wa Sheria, Bw. Nicodemus Chuwa akifuatilia Majadiliano kuhusu Miswada ya Sheria Bungeni, Jijini Dodoma.

“KUFIKIA MALENGO YA DIRA 2050 TAIFA LINAHITAJI ZAIDI YA UTAALAMU WETU WA SHERIA”

- Na Lela Muhaji -



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari akifungua mafunzo ya tatu ya Bespoke kwa Mawakili wa Serikali, yaliyofanyika Jijini Arusha.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari alifungua mafunzo ya Bespoke kwa Mawakili wa Serikali, yalioandaliwa na kuratibiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuanzia tarehe 15 hadi 17 Julai, 2026 katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano Arusha (AICC) Jijini Arusha.

Mhe. Johari aliwasisitiza Mawakili wa Serikali kuhakikisha wanasimamia vyema Utawala wa Sheria katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na kuishauri Serikali ipasavyo kuendelea kuzingatia sheria ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa 2050.

“Nitumie fursa hii kuwakumbusha washiriki wote kuwa tunapoendelea katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa 2050 ni muhimu kufahamu kuwa, Taifa linahitaji zaidi ya utaalamu wetu wa sheria.” Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Aidha, Mhe. Johari aliwakumbusha Mawakili wa Serikali kutambua nafasi yao katika utekelezaji wa Dira ya Taifa 2050, ambapo alieleza kuwa utekelezaji wa malengo yake unategema kwa kiwango kikubwa uwezo wa Mawakili wa Serikali, pamoja na kuwa na mifumo ya kisheria itakayokwenda sambamba na kasi ya maendeleo na mabadiliko yanayoendelea nchini na duniani kote.

“Ni imani yetu kuwa, Dira hii itatekelezwa kwa kiwango kilichokusudiwa kwa kupitia Sheria bora, Sera madhubuti, Mikataba yenye tija, Mifumo bora ya utawala wa kisheria sambamba na taasisi zenye uwezo wa kutafsiri malengo ya maendeleo kuwa na matokeo yanayoonekana kwa manufaa ya Taifa lote kwa ujumla.” Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Katika hatua nyingine, Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliwahimiza Mawakili wa Serikali kuzingatia matumizi ya teknolojia ambayo yamebadilisha kwa kiasi kikubwa utoaji wa huduma za kisheria ikiwemo matumizi ya Akili Mnemba na utoaji wa matumizi ya Ushahidi wa Kielektroniki.

"Mapinduzi ya teknolojia yamebadilisha kwa kiasi kikubwa, namna ambavyo huduma za kisheria zinazoendelea kutolewa nchini na duniani kote kwa ujumla, hivyo katika mazingira haya, Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria hawawezi kuendelea kutekeleza majukumu yao ya kazi kwa kutumia mazoea ya zamani". Alisema Mhe. Johari.

Vilevile, Mhe. Johari aliwataka Mawakili wa Serikali kuendelea kufanya kazi kwa kuzingatia Uadilifu, Weledi, Uwajibikaji, Uzalendo na Nidhamu ili waweze kutoa ushauri wenye ubora na tija na Mikataba yenye manufaa kwa Taifa.

"Wananchi wanatarajia kuona rasilimali za umma zikilindwa kwa wivu mkubwa. Wananchi wanatarajia kuona Sheria zikitumika kama nyenzo ya maendeleo ya kufikia malengo ya Dira ya Taifa 2050." Alisema Mhe. Johari.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali alitoa wito kwa Mawakili wa Serikali kuendelea kuyatumia mafunzo haya kama fursa ya kujifunza, kubadilishana uzoefu, kujenga mitandao ya kitaaluma, kuibua suluhisho za changamoto zinazowakabili Mawakili hao.

Kwa upande wake, Gavana Mstaafu wa Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Prof. Florens Luoga akitoa mada kuhusu *"Nafasi ya Kimkakati ya Mawakili wa Serikali katika kufikia Dira ya Taifa 2050,"* ambapo alieleza nafasi waliyonayo Mawakili wa Serikali katika kufanya maboresho mbalimbali ya Kisheria ili kuweza kutimiza malengo ya Dira 2050.

"Wakili wa Serikali ana nafasi kubwa katika kuchangia maendeleo ya nchi na kulinda maslahi ya Taifa, kwakuwa ushauri wa kisheria anaoutoa ni kichocheo katika mageuzi ya kiuchumi." Alisema Prof. Luoga.

Awali, akimkaribisha Mgeni Rasmi, Mwandishi Mkuu wa Sheria Bw. Onorius Njole alimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuwezesha kufanyika kwa mafunzo haya muhimu kwa Mawakili wa Serikali ambayo yataleta mabadiliko katika utekelezaji wa majukumu yao.

Akiwakaribisha washiriki katika mafunzo ya tatu Bespoke, Mkurugenzi wa Uratibu na Huduma za Sheria, Bi. Neema Ringo alieleza mafunzo haya yatasaidia kuwezesha Mawakili wa Serikali kupata uzoefu katika nyanja mbalimbali za kisheria, ambapo alieleza kuwa wakufunzi mahiri watawasilisha mada mbalimbali kwa Washiriki wa Mafunzo ya Bespoke.

Msimu wa tatu wa Mafunzo ya Bespoke kwa Mawakili wa Serikali ulifunguliwa tarehe 15 hadi 17 Julai, 2026 Jijini Arusha ambapo Mawakili wa Serikali walijifunza masuala mbalimbali ya kisheria na kiuchumi kutoka kwa Wakufunzi wabobevu wa Kitaifa na Kimataifa.



Gavana Mstaafu wa Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Prof. Florens Luoga akitoa mada wakati wa Mafunzo ya tatu ya Bespoke kwa Mawakili wa Serikali, yaliyofanyika Jijini Arusha.

KUELEKEA DIRA 2050 SERIKALI YAIMARISHA ULINZI WA WATOTO

- Na Rebecca Kwandu -



Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Zainab Katimba (Mb) akizungumza na watumishi wa Kikosi Kazi cha Ulinzi wa Mtoto Dhidi ya Biashara ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu mara baada ya kupokea taarifa ya utendaji kazi wa Kikosi Kazi hicho.

Ulinzi wa mtoto ni nguzo muhimu katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, inayolenga kujenga jamii salama isiyo na unyanyasaji wa kijinsia kwa watoto. Ili kuimarisha mapambano dhidi ya ukatili wa kingono na biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu, mwaka 2022 Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Sylvester Mwakitalu, chini ya kifungu cha 4A cha Sheria ya Huduma za Mashtaka, kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai Tanzania, alianzisha Kikosi Kazi cha Ulinzi wa Mtoto Dhidi ya Biashara ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu (AHTCP-TF).

Katika kuendeleza maono hayo, Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano wa taasisi za haki jinai ili kuhakikisha watoto wanalindwa dhidi ya ukatili na biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu.

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Zainab Katimba, alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kuimarisha mapambano dhidi ya ukatili wa kingono kwa watoto na usafirishaji haramu wa binadamu ili kuhakikisha watoto wanapata ulinzi unaostahili na haki zao zinalindwa kama sehemu ya kujenga Taifa imara.

Mhe. Katimba alisema Serikali itaendeleza juhudi hizo kupitia ushirikiano wa taasisi

mbalimbali za haki jinai, ikiwemo Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS), pamoja na wadau wa maendeleo, kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kuzuia, kuchunguza na kufikisha wahusika wa makosa hayo mbele ya sheria.

Mhe. Katimba aliyasema hayo alipotembelea Kikosi Kazi cha Ulinzi wa Mtoto Dhidi ya Biashara ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu (AHTCP-TF) kwa lengo la kujionea namna kinavyotekeleza majukumu yake. Katika ziara hiyo alipongeza kazi inayofanywa na Kikosi Kazi hicho kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kufichua na kuvunja mitandao ya kihalifu inayohusika na ukatili wa kingono kwa watoto na usafirishaji haramu wa binadamu.

"Kikosi kazi hiki kimeonyesha matokeo makubwa kwa kuvunja mitandao ya usafirishaji haramu wa binadamu, kuwakamata wahusika na kuwasaidia manusura kurejea katika jamii zao," alisema Mhe. Katimba.

Aidha, akizungumzia mafanikio yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwa Kikosi Kazi hicho, Mkuu wa Kikosi Kazi cha Ulinzi wa Mtoto Dhidi ya Biashara ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu, SACP Tulibake Kasongwa, amesema hadi kufikia Februari 2026 manusura 233 wameokolewa na kupatiwa huduma za kisaikolojia, kiafya na kijamii. Vilevile, manusura 85 walipatiwa nyumba salama, huku 17 waliokuwa raia wa Afrika Kusini, Burundi, Marekani, Indonesia na Rwanda wakisaidiwa kurejeshwa katika nchi zao.

SACP Kasongwa aliongeza kuwa manusura watano walipatiwa mafunzo ya ufundi stadi, ambapo wawili wamehitimu na kupatiwa mtaji wa kujikwamua kiuchumi. Pia, Kikosi Kazi kimefanikiwa kuwabaini watuhumiwa 20 wanaohusishwa na mitandao ya usafirishaji haramu wa binadamu, hatua inayodhihirisha mafanikio ya juhudi za Serikali katika kuvunja mitandao ya uhalifu uliopangwa.

Alieleza kuwa, Kikosi Kazi hicho hakikuanzishwa kwa lengo la kuchukua au kuingilia majukumu ya vyombo vya uchunguzi, bali kuunda timu ya wataalamu waliobobea katika masuala ya ulinzi na ustawi wa mtoto ili kuongeza ufanisi katika kushughulikia makosa hayo.

Sambamba na hayo, Kikosi Kazi cha Ulinzi wa Mtoto Dhidi ya Biashara ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu kilianzishwa kwa lengo la kuchunguza na kuvunja mitandao mikubwa ya kihalifu inayojihusisha na usafirishaji haramu wa binadamu pamoja na makosa ya unyanyasaji wa kingono, ili kung'oa mizizi ya uhalifu huo na kuimarisha usalama wa watoto katika jamii. Mbinu hiyo inalenga kushughulikia chanzo cha uhalifu badala ya kuwakamata wahusika wa matukio ya kawaida pekee.

Kupitia ushirikiano wa taasisi za haki jinai, Serikali inaendelea kujenga mazingira salama kwa watoto na kuhakikisha hakuna mtoto anayepoteza fursa ya kufikia ndoto zake kutokana na ukatili au usafirishaji haramu wa binadamu. Hatua hizi zinaifanya Tanzania kusonga mbele kuelekea kutimiza azma ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ya kujenga jamii salama, yenye haki, usawa na inayolinda utu wa kila mtoto.

OWMS YAJIPANGA UENDESHAJI WA MAJUKUMU YA KISHERIA

- Na Prisca Ulomi -



Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akiendesha kikao cha menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali cha kutathmini utendaji kazi wa Ofisi kilichofanyika Jijini Dodoma.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilifanya tathmini ya utendaji kazi katika kipindi cha nusu Mwaka wa Fedha 2025/26 na kujipanga kutekeleza majukumu yake katika kipindi cha mwezi Januari hadi Juni, 2026.

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi aliendesha kikao cha menejimenti cha kutathmini utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kilichofanyika jijini Dodoma kwa lengo la kuchambua taarifa ya utekelezaji ya Ofisi hiyo, kupanga mikakati mipya ya utendaji kazi ili kuhakikisha kuwa Ofisi hiyo inaendesha mashauri ya madai na usuluhishi kwa tija na ufanisi ndani na nje ya nchi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake.

“Kikao hiki ni cha kimkakati, lengo ni kujipanga kuendesha majukumu ya kisheria ya Ofisi ikizingatiwa kuwa kikao hiki kinafanyika kuelekea Siku ya kilele cha Wiki ya Sheria inayoadhimishwa kila mwaka mwanzoni mwa mwezi Februari,” alisisitiza Dkt. Possi.

Pia, Dkt. Possi aliongeza kuwa Ofisi imedhamiria kufungua Ofisi nyingine kwenye mikoa ya Katavi, Geita, Singida ili kusogeza huduma karibu na wananchi na aliwataka wajumbe wa menejimenti ya Ofisi hiyo kuendelea kutumia mifumo ya TEHAMA katika utendaji kazi.

Naye Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo akizungumza kwa niaba ya menejimenti ya Ofisi hiyo alieleza kuwa kwa kuwa mwaka mpya umeanza na Ofisi inaingia kipindi cha pili cha Mwaka wa Fedha, wajumbe wa menejimenti hiyo wataendelea kutekeleza majukumu kwa wakati.

Kikao hicho hufanyika mara moja kwa mwaka ili kuwapa muda wa kutosha wajumbe wa menejimenti wa Ofisi hiyo kufanya tathmini ya utendaji kazi na majukumu yaliyopangwa kutekelezwa katika kipindi cha mwaka husika.



Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo akifuatilia majadiliano ya kikao cha menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali cha kutathmini utendaji kazi wa Ofisi hiyo kilichofanyika jijini Dodoma.



Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kabla ya kikao cha kutathmini utendaji kazi wa Ofisi hiyo kilichofanyika jijini Dodoma. Kushoto ni Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo.

TANZANIA YANG'ARA CALC: BI REHEMA KATUGA AIBUKA MSHINDI WA AFRICA

- Na Michael Mhina -



Mkurugenzi wa Divisheni ya Urekebu wa Sheria, Tafiti na Mafunzo, na mwakilishi wa Afrika katika Baraza la Uongozi na Usimamizi la Chama cha Wataalamu wa Uandishi wa Sheria wa Jumuiya ya Madola (Commonwealth Association of Legislative Counsel (CALC), Bi. Rehema Katuga.

Mtanzania, Rehema Katuga kutoka Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria (OCPD), amechaguliwa kuwa mmoja wa wawakilishi wa Afrika katika Baraza la Uongozi na Usimamizi la Chama cha Wataalamu wa Uandishi wa Sheria wa Jumuiya ya Madola (Commonwealth Association of Legislative Counsel (CALC), kufuatia uchaguzi uliofanyika wakati wa Mkutano Mkuu wa chama tarehe 19 Julai 2026 nchini Singapore.

Ushindi huo unaipa Tanzania nafasi ya kushiriki katika chombo kinachosimamia uongozi na kufanya maamuzi ya kimkakati kuhusu maendeleo ya taaluma ya Uandishi wa Sheria katika nchi wanachama wa

Jumuiya ya Madola, huku ukiimarisha uwakilishi wa Katika uchaguzi huo, Bi. Katuga aliwashinda wagombea watatu kutoka Afrika, wakiwemo wawili kutoka Afrika Kusini na mmoja kutoka Namibia na akiwa mgombea pekee kutoka Tanzania.

Baraza la CALC linajumuisha wawakilishi wawili kutoka kila bara na lina jukumu la kusimamia shughuli na mwelekeo wa chama hicho.

Akizungumza baada ya kuchaguliwa, Bi. Katuga alisema CALC ni jukwaa muhimu linalowaunganisha wataalamu wa Uandishi wa Sheria kutoka nchi za Jumuiya ya Madola kwa lengo la kuimarisha ushirikiano

wa kitaaluma, kujenga uwezo na kuendeleza ubora wa Uandishi wa Sheria.

"CALC inalenga kuimarisha uwezo wa wataalamu wa Uandishi wa Sheria katika kuan- daa sheria bora zinazotekeleza sera za Serikali na kukidhi mahitaji ya maendeleo ya nchi wanachama, na kuhamasisha mafunzo, kubadilishana uzoefu, programu za mafunzo kwa vitendo, matumizi ya teknolojia na kuendeleza mbinu bora za Uandishi wa Sheria," alisema Bi. Katuga.

Alieleza nafasi hiyo itaiwezesha Tanzania na Afrika kwa ujumla kuimarisha ushirikiano na wataalamu wa Uandishi wa Sheria kutoka nchi nyingine za Jumuiya ya Madola, kubadilishana uzoefu na kutumia mbinu bora za kisasa katika kuandaa sheria.

Aidha, aliendelea kwa kusema kuwa atatumia nafasi hiyo kuimarisha mtandao wa wataalamu wa Uandishi wa Sheria barani Afrika, kukuza taaluma hiyo na kuchangia juhudi za kuboresha ubora wa sheria kupitia uandishi wenye weledi, uwazi na ufanisi.

Uwakilishi wa Tanzania katika Baraza la CALC unatarajiwa kuongeza ushiriki wa nchi katika majadiliano ya kimataifa kuhusu maendeleo ya taaluma ya Uandishi wa Sheria, pamoja na kupanua fursa za mafunzo, kujengea uwe o wataalamu, kubadilishana teknolojia na uzoefu, hatua zinazochangia kuimarisha mchakato wa uandaaji wa sheria nchini.



"Mwakilishi wa Afrika katika Baraza la Uongozi na Usimamizi wa Chama cha Wataalamu wa Uandishi wa Sheria wa Jumuiya ya Madola (CALC), Bi. Rehema Katuga (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya washiriki kutoka OCPD kwenye mkutano wa CALC uliofanyika nchini Singapore

SERIKALI YAJIPANGA KUREKEBISHA SHERIA ILI ZIENDE SAMBAMBA NA DIRA 2050

- Na Lela Muhaji -



Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera (Mb) akifungua Mkutano wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Watumishi uliofanyika Jijini Arusha.

Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera (Mb) alisema kuwa Serikali iko mbioni kufanya maboresho ya sheria mbalimbali ili ziende sambamba na malengo ya Dira Taifa 2050.

Dkt. Homera alitoa kauli hiyo wakati akifungua Mkutano wa Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali uliofanyika tarehe 28 Aprili, 2026 Jijini Arusha.

“Nimpongeze Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameanza vizuri na sasa tunaenda kurekebisha sheria mbalimbali ili ziweze kueandana na malengo ya kufikia Dira ya 2050”. alisema Mhe. Dkt. Homera.

Akizungumza katika Mkutano huo, Waziri wa Katiba na Sheria alieleza kuwa ni

muhimu kwa Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuendelea kujiendeleza kitaalamu na Kimaarifa ili waweze kuishauri vizuri Serikali na kuinua uchumi wa Taifa.

“Napenda kutoa rai kwenu mzidi kujiendeleza kitaaluma na kimaarifa ili muweze kulishauri vizuri Taifa letu hasa juu ya Sheria zipi zinapaswa kutungwa na kurekebisha kwa ajili ya kuchochea vizuri ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kweli kwa Wananchi wote.” Alisema Dkt. Homera.

Aidha, Dkt. Homera alimpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Menejimenti ya Ofisi kwa kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

"Nimshukuru Mhe. Rais kwa kukuteua tena kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali unaitendea haki nafasi hiyo, pia nikupongeze Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali na timu yako kwa maboresho makubwa uliyoyafanya katika Ofisi hii." Alisema Mhe. Dkt. Homera.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari akizungumza awali kabla ya kumkaribisha Mgeni Rasmi, alisema kuwa ili kufikia malengo ya Dira 2050 ni muhimu kwa Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakaongeza kasi katika maboresho ya Sheria mbalimbali.

"Wakati wenzetu wengine wanakuja, wakute tayari tumezifungamanisha sheria zetu na malengo ya Dira 2050 kwa kuzifanya rafiki na wezeshi kwa sekta na malengo mbalimbali." Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Katika hatua nyingine, Mhe. Johari alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna anavyoiwezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

"Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitarudia tena kumshukuru, kwa dhati kabisa ya moyo wangu, Rais wa Nchi yetu, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo Serikali yake imewezesha hayo kufanyika. Asante sana Mhe. Rais." Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Vilevile Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliwasisitiza Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuendelea

kufanya kazi kwa bidii na kuzingatia Nidhamu, Weledi na Uadilifu ili kuweza kufikia malengo ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Taifa kwa ujumla.

"Ni lazima kila mmoja wetu ajenge na kudumisha utamaduni wa uwajibikaji unaozingatia weledi, ubunifu katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali." Alisema Mhe. Johari.

Kwa upande wake, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Samwel M. Maneno aliwaeleza Watumishi juu ya umuhimu wa matumizi sahihi ya mifumo mbalimbali ya TEHEMA iliyoko katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuwawezesha katika kutekeleza majukumu yao kwa haraka na urahisi.

"Niwasisitize Watumishi juu ya matumizi ya Mifumo mbalimbali tuliyonayo kupitia mifumo hii tutaweza kutekeleza majukumu yetu kwa urahisi na ufanisi." Alisema Mhe. Maneno.

Mkutano wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Watumishi wa Ofisi, ulihusisha wasilisho kuhusu mafanikio ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Taarifa ya Utendaji kazi ya mwaka 2023/2024, Mpango Mkakati wa Ofisi, Muundo mpya wa Ofisi, Uzinduzi wa Tovuti ya Ofisi, Mifumo ya TEHAMA, Blueprint, Kipeperushi cha Je Wajua, pamoja na vitabu vinne vya Risk Management Framework, Risk Register, Risk Fraud Management Framework na Risk Fraud Register.



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari akizungumza katika Mkutano wa Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali uliofanyika Jijini Arusha.



Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wakifuatilia mada mbalimbali wakati wa Mkutano wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Watumishi uliofanyika Jijini Arusha.

DPP AWAPONGEZA MAWAKILI WA SERIKALI KWA KUFIKIA ASILIMIA 88 YA USHINDI WA MASHAURI

- Na Rebecca Kwandu -



Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Bw. Sylvester Mwakitalu akifungua Kikao Kazi cha Mkurugenzi wa Mashtaka, Menejimenti na Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kilichofanyika Jijini Arusha.

Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Bw. Sylvester Mwakitalu, aliwapongeza Menejimenti na Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS) kwa kuendelea kuimarisha utendaji kazi uliowezesha Ofisi kufikia kiwango cha asilimia 88 ya ushindi wa mashauri.

DPP Mwakitalu alitoa pongezi hizo wakati akifungua Kikao Kazi cha Mkurugenzi wa Mashtaka, Menejimenti na Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kilichofanyika tarehe 15 Julai, 2026, Jijini Arusha. Alisema mafanikio hayo yametokana na juhudi, weledi, uaminifu na kujituma kwa Mawakili wa Serikali, sambamba na ushirikiano mzuri na wadau mbalimbali wa mnyororo wa haki jinai.

Alieleza kuwa lengo la kikao hicho ni kufanya tathmini ya utendaji kazi wa Ofisi,

kubadilishana uzoefu, kujadili changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya mashtaka na kuweka mikakati ya pamoja ya kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Aidha, alisema kikao hicho kitatoa fursa kwa washiriki kutathmini mafanikio yaliyopatikana, kujifunza kutokana na changamoto zilizojitokeza na kuandaa mikakati madhubuti ya kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

Katika hotuba yake, DPP Mwakitalu alisema Mawakili wa Serikali ni nguzo muhimu katika mfumo wa haki jinai, kwani kiwango cha imani ya wananchi katika utoaji wa haki kinategemea namna wanavyotekeleza majukumu yao kwa weledi, uadilifu na kwa

kutumia ipasavyo ushahidi unaowasilishwa na vyombo vya uchunguzi.

Alisisitiza kuwa mafanikio ya Ofisi hayawezi kupatikana kwa kufanya kazi kwa kujitegemea, bali yanahitaji ushirikiano wa karibu na wadau wote wa mnyororo wa haki jinai, wakiwemo Jeshi la Polisi, Mahakama, taasisi za uchunguzi na wadau wengine wanaoshiriki katika utekelezaji wa haki.

DPP Mwakitalu pia aliwahimiza Mawakili wa Serikali kuendelea kujifunza na kujijengea uwezo ili kuendana na mabadiliko ya sheria,

Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia pamoja na mbinu mpya za uchunguzi na uendeshaji wa mashauri.

Akihitimisha hotuba yake, aliwataka washiriki watakaporejea katika vituo vyao vya kazi kuendeleza utamaduni wa kujisomea sheria, hukumu, machapisho ya kitaaluma na nyenzo nyingine za kisheria ili kuongeza umahiri wao, kuimarisha ubora wa huduma na kudumisha mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya mashtaka.



Mawakili wa Serikali wakifuatilia kwa umakini hotuba ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Bw. Sylvester Mwakitalu wakati akihutubia kwenye Kikao Kazi cha Mkurugenzi wa Mashtaka, Menejimenti na Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kilichofanyika Jijini Arusha.

DKT. POSSI: VIONGOZI NI TASWIRA YA TAASISI NA SERIKALI KWA JAMII

- Na Prisca Ulomi -



Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi, akizungumza na wajumbe wa menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati akifungua kikao cha faragha kwa viongozi hao kilichofanyika Jijini Dodoma.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliendesha mafunzo kwa viongozi wa taasisi hiyo na menejimenti ambayo yalifanyika Jijini Dodoma ambapo pamoja na mafunzo hayo viongozi hao walitathmini utendaji kazi wao wa kila siku, walipatiwa mafunzo ya uongozi ikiwemo usimamizi na mgawanyo wa majukumu, usimamizi wa muda, itifaki na ustaarabu.

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi alifungua mafunzo hayo na kuwaeleza wajumbe wa menejimenti ya Ofisi hiyo kuwa viongozi ni taswira ya taasisi na Serikali kwa ujumla ambapo aliwaeleza kuwa kiongozi yeyote awe Mkuu wa Idara au Mkuu wa

Kitengo atambue kuwa anabeba taswira ya taasisi anayofanyia kazi na Serikali kwa ujumla popote alipo. Hivyo ni muhimu kuzingatia sheria, taratibu, kanuni, maadili ya uongozi, mila na desturi za uongozi.

“Kila mmoja atambue wadhifa alionao na bendera anayopeperusha kwa niaba ya Serikali na kwa wale tunaowaongoza. Tuwe walezi kwa kuzingatia kuwa muda mwingi tupo mahali pa kazi kuliko familia zetu, watu tunaofanya nao kazi wafurahie kufanya kazi na wewe badala ya kukasirika, tujitathmini na kutafakari utendaji kazi wetu ili kuwa na matokeo mazuri mahali pa kazi na kujipa

muda wa kujisahihisha huku tukifanya kazi kwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni, tuwe wabunifu na tufanye ufuatiliaji wa majukumu,” alisisitiza Dkt. Possi.

Naye Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo alisema kuwa kikao hicho cha faragha na mafunzo hayo ni muhimu kwa wajumbe wa menejimenti wa Ofisi hiyo ili kupata muda wa kutathmini utendaji kazi na anaamini kuwa mafunzo hayo yataleta mabadiliko katika taasisi, kuwawezesha kuwafahamu na kuwasimamia vizuri wasaidizi wao, kumiliki kazi zao, kufanya maamuzi kwa wakati na kuzingatia muda katika utekelezaji wa majukumu.

Akitoa mada kuhusu uongozi na mgawanyo wa majukumu kwa wajumbe hao, Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uongozi, Bw. Kadari Singo, aliwapongeza viongozi wa Ofisi hiyo kwa kuandaa na kushiriki mafunzo hayo na ametoa rai kwao kujenga utaratibu wa kuwajenga wasaidizi wao ili wanapoondoka kwenye nafasi zao wawe na watu wa kuhakikisha mifumo inafanya kazi.



Bi. Alice E. Mtulo Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, akizungumza na Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa kikao cha faragha kilichofanyika Jijini Dodoma.

Aidha, Mhadhiri wa Chuo cha Diplomasia, ndugu Godwin Gonde Amani, aliwafundisha wajumbe wa menejimenti hiyo mada kuhusu itifaki na ustaarabu ambayo ilijikita kwenye masuala ya muonekano wa mtu, mavazi, mawasiliano, tabia, mienendo, matumizi ya akili ya kuzaliwa, kuheshimu mamlaka na madaraka ya kiongozi, kutambua, kujali na kuthamini uwepo wa kiongozi.

“Itifaki ni jambo muhimu Serikalini na katika uongozi kwa kuwa ni jambo nyeti linaathari chanya na hasi baina yako binafsi na mtu mwingine katika muonekano wa mavazi, salamu, mazungumzo na mawasiliano,” alisisitiza Mhadhiri Amani.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekuwa na utaratibu wa kuendesha mafunzo kwa viongozi wa Ofisi hiyo na kufanya kikao cha faragha kwa ajili ya kutathmini utendaji kazi na utekelezaji wa majukumu mara moja kwa mwaka.



Ndugu Kadari Singo Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uongozi, akitoa mada kuhusu Ugawaji wa Majukumu na Usimamizi wa Muda kwa Wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa kikao cha faragha kilichofanyika Jijini Dodoma.

OCPD YAUNGA MKONO KAMPENI YA TANZANIA 27 YA KIJANI

- Na Michael Mhina -



Watumishi wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria (OCPD) wakiwa katika picha ya pamoja katika kituo cha Afya cha Ilazo baada ya kukabidhiwa miti kwaajili ya kupanda kwenye makazi yao ili kuunga mkono kampeni ya #MtiWanguChallenge inayoratibiwa na OCPD ikishirikiana na TBC1

Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria (OCPD) ikiongozwa na Mkurugenzi wa Divisheni ya Urekebu wa Sheria, Utafiti na Mafunzo, Bi. Rehema Katuga aliyemwakilisha Mwandishi Mkuu wa Sheria, tarehe 27 Juni, 2026 ilishiriki zoezi la upandaji miti katika Kituo cha Afya cha Ilazo jijini Dodoma ikiwa ni kuunga mkono juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuhifadhi mazingira kupitia Kampeni ya 27 ya Kijani inayoratibiwa na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC).

Akizungumza na TBC wakati wa zoezi hilo, Bi. Katuga alisema OCPD inajivunia kuwa sehemu ya kampeni hiyo kwa kuwa inalenga kuifanya Dodoma kuwa ya kijani na kuimarisha utunzaji wa mazingira, huku

akisisitiza kuwa ofisi itaendelea kushiriki kikamilifu katika juhudi za uhifadhi wa mazingira.

"Sisi OCPD tunafurahi kuwa sehemu ya kampeni hii ambayo itasaidia kuifanya Dodoma kuwa ya kijani na kuimarisha mazingira" alisema Bi. Katuga.

Katika kuendeleza dhamira hiyo, Bi. Katuga aliitambulisha rasmi #MtiWangu Challenge, mpango unaowahamasisha watumishi wa OCPD kupanda miti majumbani kwao na kuhakikisha inastawi.

"Tunataka pia kuhamasisha watumishi wa OCPD katika kuifanya Dodoma ya kijani, hivyo kupitia hii challenge ya #MtiWangu watumishi wanapewa miti kwenda kuipanda"

majumbani na tutafanya ufuatiliaji ambapo mwakani watumishi ambao miti yao itakuwa imestawi vizuri watapatiwa zawadi nono". Alisisitiza Bi. Katuga.

Kwa upande wake, Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya cha Ilazo, Mathei Kauki, aliishukuru OCPD kwa kuchagua kituo hicho kwa ajili ya zoezi la upandaji miti, akieleza kuwa miti hiyo itakuwa na manufaa makubwa kwa wagonjwa.

"Miti ya matunda na miti ya vivuli iliyopandwa na OCPD kituoni hapa ina msaada mkubwa kwa wagonjwa ambapo itawawezesha kupata vivuli, matunda na upepo na hii italeta faraja kwao" alisema Kauki.

Kupitia ushiriki wake katika Kampeni ya Tanzania 27 ya Kijani pamoja na uzinduzi wa #MtiWangu Challenge, OCPD inalenga kuhamasisha utamaduni wa upandaji na utunzaji wa miti miongoni mwa watumishi wake na jamii kwa ujumla ili kuongeza mchango katika uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Kwa pamoja, OCPD na uongozi wa Kituo cha Afya cha Ilazo waliahidi kuisimamia na kuitunza miti yote iliyopandwa ili ikue na kustawi vizuri kwa manufaa ya wananchi wa sasa na vizazi vijavyo.



NAIBU MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AKAGUA MRADI WA UJENZI WA JENGO LA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI MTUMBA

- Na Ally Masaniga -



Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Samwel M. Maneno akikagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma.

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Samwel M. Maneno alifanya ziara ya kukagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali lililopo Mtumba Jijini Dodoma, lengo likiwa ni kujionea hatua zilizofikiwa pamoja na kuhakikisha kazi hiyo inakamilika kwa viwango vilivyokusudiwa na kwa wakati.

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali alifanya ziara hiyo tarehe 4 Septemba, 2026 ambapo alikagua maeneo mbalimbali ya mradi huo ikiwa ni pamoja na mifumo ya umeme na TEHAMA, eneo la maegesho ya magari, vyumba vya ofisi, na kumbi za mikutano.

Akizungumza mara baada ya ukaguzi huo, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali alieleza kuwa ukamilishaji wa jengo hilo utakuwa chachu kubwa katika kuboresha mazingira ya kazi kwa Mawakili na

Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, jambo litakaloongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za kisheria kwa Serikali na wananchi kwa ujumla.

Naye, Mhandisi Evance Mwingizi anayesimamia mradi huo kutoka SUMA JKT, amesema mradi huo umefikia asilimia 80, na kazi zinaendelea kulingana na mpango kazi uliowekwa.

Aidha, Mhandisi Mwingizi alieleza kuwa kazi zinazoendelea sasa ni pamoja na ukamilishaji wa kupaka rangi, kuweka vioo, kuweka milango, kusanikisha mifumo ya umeme na TEHAMA, pamoja na utengenezaji wa eneo la maegesho ya magari.

Kukamilika kwa Jengo hilo kutawasaidia Mawakili wa Serikali na Watumishi kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa kasi, umakini, na ufanisi mkubwa zaidi hivyo kurahisha upatikanani wa wa huduma za kisheria kwa wananchi.



Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Samwel M. Maneno akikagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma.

NAIBU DPP AHIMIZA USHIRIKIANO KATIKA KUDHIBITI UHALIFU WA KIFEDHA

- Na Rebecca Kwandu -



Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, Bi. Bibiana Kileo akifungua warsha kuhusu matumizi ya taarifa fiche za kifedha katika kufanya uchunguzi sambamba wa kifedha, iliyofanyika mkoani Pwani.

Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, Bi. Bibiana Kileo, amewataka Waendesha Mashtaka, Wachunguzi na Wapelelezi kuendelea kuimarisha ushirikiano baina ya taasisi zao kwa kufanya uchunguzi sambamba wa kifedha na kutumia ipasavyo ujuzi wanaoupata kama nyenzo muhimu katika mapambano dhidi ya uhalifu wa kifedha, hususan makosa ya utakatishaji fedha, ufadhili wa ugaidi na uhalifuwa kupangwa.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa warsha kuhusu matumizi ya taarifa fiche za kifedha katika kufanya uchunguzi sambamba wa kifedha, iliyofanyika tarehe 8 Mei, 2026 mkoani Pwani, Bi. Kileo alisema tathmini mbalimbali za kimataifa zilizopita zilioneshwa

kuwepo kwa mapungufu katika mifumo ya kushughulikia uhalifu wa kifedha nchini licha ya uwepo wa sheria madhubuti.

Bi. Kileo amesema ushirikiano uliopo kati ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Jeshi la Polisi unalenga kuziba mapengo hayo pamoja na kuimarisha kasi ya kushughulikia makosa ya utakatishaji fedha. Amefafanua kuwa tathmini hizo pia zilioneshwa udhaifu katika kudhibiti usafirishaji haramu wa fedha na ufadhili wa ugaidi, hali iliyochochea kuanzishwa kwa Kituo Jumuishi cha Kushughulikia Uhalifu wa Kifedha ambacho kimesaidia kuimarisha mapambano dhidi ya uhalifu huo.

Aidha, amesema mafunzo mbalimbali yanayoendelea kutolewa yamechangia kwa kiwango kikubwa kuimarisha uwezo wa kudhibiti uhalifu wa kifedha nchini, huku akizitaka taasisi hizo kuendelea kuimarisha mahusiano na ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yao.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Divisheni ya Makosa ya Udanganyifu, Utakatishaji Fedha na Rushwa, Bw. Christopher Msigwa,

amesema warsha hiyo inalenga kuongeza uelewa na kuimarisha mifumo ya uchunguzi katika nyanja za kifedha.

Warsha hiyo imewakutanisha maafisa kutoka taasisi mbalimbali zilizopo katika mfumo wa haki jinai zikiwemo; TAKUKURU, NPS, Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyama Pori Tanzania (TAWA), Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA).



Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, Bi. Bibiana Kileo akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa warsha kuhusu matumizi ya taarifa fiche za kifedha katika kufa ya uchunguzi sambamba wa kifedha, iliyofanyika mkoani Pwani.

OWMS YAWASILISHA TAARIFA YA UTEKELEZAJI KWA KAMATI YA BUNGE

- Na Prisca Ulomi -



Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi Alice E. Mtulo akiwasilisha taarifa ya majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Jijini Dodoma.

Katika juhudi za kuendeleza uwajibikaji na uwazi, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu yake mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwenye Ukumbi wa Bunge Jijini Dodoma, kwa lengo la kutathmini utendaji kazi, changamoto, na mafanikio ya ofisi hiyo katika kusimamia mashauri ya Serikali.

Akizungumza na wajumbe wa kamati hiyo pamoja na Viongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb), alisema kuwa ushirikiano kati ya Kamati ya Bunge, Wizara ya Katiba na Sheria, pamoja na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni kiungo muhimu katika kuhakikisha maslahi ya nchi

yanalindwa kupitia mifumo imara ya kisheria iliyopo nchini.

Dkt. Ndumbaro aliipongeza OWMS kwa kazi nzuri inayofanyika na kueleza kuwa imesaidia kuimarisha utendaji kazi kati ya Ofisi ya Wakili Mkuu katika kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi, hivyo kupelekea kuendesha mashauri ya serikali kwa ufanisi hatua iliyosaidia kuokoa fedha nyingi ambazo zitasaidia kutekeleza miradi ya maendeleo nchini.

Mhe. Dkt. Ndumbaro alieleza kuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ni daraja la kuhakikisha kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inapata rasilimali zote zinazohitajika ili kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa kuwa anatambua uzito wa majukumu iliyonayo.

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali alieleza kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itahakikisha inafanyia kazi maelekezo na ushauri uliotolewa na Kamati huku akiahidi kuendelea kufanyakazi kwa karibu na kamati, Wizara na taasisi zilizoko chini yake ili kuongeza chachu ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ili kufikia malengo iliyojiwekea katika kusimamia mashauri ya madai na usuluhishi.

"Tunatambua kuwa ushauri na maelekezo yanayotolewa na Kamati hii ni chachu ya mabadiliko ndani ya ofisi yetu, tunaahidi kuendelea kufanya kazi kwa karibu na Kamati pamoja na Wizara ili kuhakikisha majukumu yetu yanatekelezwa kwa wakati na kwa ubora unaostahili," alisema Bi. Mtulo.

Kuelekea Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Bi. Mtulo alieleza kuwa Ofisi itaendelea na usimamizi madhubuti na uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi ili kuhakikisha rasilimali za nchi zinalindwa, jambo ambalo litasaidia kuvutia wawekezaji wa sekta mbalimbali na uboreshaji wa miundombinu ili kuchochea ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii.

Bi. Mtulo alieleza kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, itaendelea kuimarisha mifumo ya ndani ya TEHAMA na kuendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wa kada zote ili kuhakikisha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inaendana na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.



Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi Alice E. Mtulo akiwasilisha taarifa ya majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Jijini Dodoma.

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Zainab Katimba (Mb) akifafanua jambo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, wakati taasisi zilizoko chini ya Wizara hiyo zilkiwasilisha majukumu yao kwa Kamati hiyo katika Ukumbi wa Bunge, Jijini Dodoma.



OCPD NA AFISI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR ZAJENGEANA UWEZO MASUALA YA UANDISHI WA SHERIA

- Na Carine Senguji -



Menejimenti ya Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria (OCPD) na viongozi kutoka Afisi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar wakiwa katika kikao cha kujengeana uwezo na kubadilishana uzoefu kuhusu Uandishi wa Sheria, Jijini Dodoma.

Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria (OCPD), ikiongozwa na Kaimu Mwandishi Mkuu wa Sheria, Bi. Rehema Katuga, ilipokea ujumbe kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa lengo la kujengeana uwezo kwenye masuala ya uandishi wa sheria na ujenzi wa mfumo wa uandishi wa sheria, jijini Dodoma.

Bi. Rehema, wakati wa ukaribisho alisema kuwa kuanzishwa kwa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria kumerahisisha upatikanaji wa sheria kwa wananchi na hii inasaidia katika upatikanaji wa haki.

"Tokea kuanzishwa kwa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria imerahisisha upatikanaji wa sheria kiurahisi kwa wananchi kwa kuwezesha kutoa toleo la urekebu wa sheria ambapo toleo la mwisho lilitolewa 2002, lakini pia imerahisisha upatikanaji wa sheria kwa lugha ya kiswahili na kiingereza kulingana na mahitaji," alisema Bi. Rehema.

Bi. Rehema aliendelea kwa kueleza kuwa kabla ya kutoa sheria kwa wananchi huwa

zinapitia hatua za uhakiki ubora kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanapata sheria zilizo bora bila makosa yoyote.

"Kubwa ambalo tumefanya kama ofisi ni kuwa na kitengo cha uhakiki ubora kama unavyojua mlaji wa mwisho wa sheria ni mwananchi na kitengo kina jukumu la kuhakiki ubora wa sheria na tathmini ya sheria ili kubaini sheria zilizotungwa na bunge zinatimiza lengo la kutungwa kwakwe na kama kuna changamoto za uandishi wanaweza kuzishughulikia," alieleza Kaimu Mwandishi Mkuu wa Sheria.

Bi. Rehema alieleza kuwa OCPD ipo katika hatua za ujenzi wa mfumo wa Uandishi wa Sheria ambao utawezesha 56 TOLEO LA 2 kutatua changamoto wakati wa uandishi.

"Kwa sasa tupo katika hatua za kutengeneza mfumo wa uandishi wa sheria ili kuweza kutatua changamoto ambazo zinajitokeza wakati wa uandishi, ambapo itatusaidia kudumisha viwango vya uandishi wa sheria na kupunguza makosa yanayojitokeza wakati wa uandishi."

Aliongeza.

Kwa upande wake Mkuu wa Divisheni ya Uchambuzi wa Sheria na Miswada kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Bw. Saleh Mubarak alishukuru kwa mapokezi mazuri kutoka OCPD

"Tunashukuru kwa mapokezi haya mazuri na tunatarajia kujifunza mengi haswa kwenye kutengeneza mfumo kwani na sisi tupo katika hatua za kutengeneza mfumo wetu utakaorahisha utekelezaji wa majukumu yetu," alisema Bw. Saleh.

“KATIKA UTEKELEZAJI WA DIRA 2050, TUNA MATARAJIO MAKUBWA NA MAWAKILI WA SERIKALI”

- Na Lela Muhaji -



Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Zainab A. Katimba (Mb) akizungumza wakati wa kufunga Mafunzo ya Bespoke kwa Mawakili wa Serikali, Jijini Arusha.

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Zainab A. Katimba alisema kuwa, Serikali ina matarajio makubwa na Mawakili wa Serikali katika utekelezaji wa miradi mingi ya kimkakati itakayoliwezesha Taifa kutekeleza na kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Mhe. Katimba aliyasema hayo, alipokuwa mgeni rasmi wakati wa kufunga msimu wa tatu wa Mafunzo ya Bespoke kwa Mawakili wa Serikali, yaliyofanyika Jijini Arusha kuanzia tarehe 15 hadi 17 Julai, 2026.

Mhe. Katimba alisema kuwa, Serikali inatarajia kuwa na Mawakili wa Serikali wenye uwezo wa kuona mbali, kufikiri kimkakati, kutumia sheria kama nyenzo ya maendeleo, na kuhakikisha kuwa kila uamuzi wa Serikali unaimarisha uchumi,

unalinda maslahi ya Taifa na unaongeza imani ya wananchi kwa taasisi za umma.

“Tunahitaji Mawakili wa Serikali watakaohakikisha kila mkataba unalinda maslahi ya Taifa, unaongeza za thamani ya edha za umma, unaepusha migogoro, na unachangia maendeleo endelevu ya nchi yetu.” Alisema Mhe. Katimba.

Aidha, Mhe. Naibu Waziri aliwataka Mawakili wa Serikali kuyatumia maarifa waliyoyapata katika kuendea kuboresha utendaji kazi wao ikiwemo kutoa ushauri wa Kisheria, kupekua na kusimamia mikataba, kushughulikia mashauri kuimarisha ushirikiano na taasisi nyingine za Serikali na namna wanavyochangia utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

"Nina imani kubwa kuwa ninyi mliopo hapa mtakuwa sehemu ya kizazi hicho cha Mawakili wa Serikali kitakachoiwezesha Tanzania kufikia matarajio makubwa ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050." Alisema mhe. Katimba.

Kwa upande wake, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Samwel M. Maneno akizungumza wakati akimkaribisha mgeni rasmi alisema kuwa, Mawakili wa Serikali wamepata fursa ya kujadili na kujifunza masuala mbalimbali ya kimkakati kwa lengo la kuimarisha nafasi ya Mawakili wa Serikali katika kuchangia utekelezaji wa Dira ya Taifa 2050.

"Tunaamini maarifa na ujuzi walioupata kupitia mafunzo haya utawawezesha Mawakili wa Serikali kutekeleza majukumu yao kwa weledi, ubunifu na ufanisi zaidi katika kulinda na kutetea maslahi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania." Alisema Mhe. Maneno,

Vilevile, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali alieleza kuwa mafunzo ya Bespoke kwa Mawakili wa Serikali yalijikita katika maeneo muhimu yanayohusu usimamizi wa majadiliano na mikataba ya kimkakati, usuluhishi wa migogoro, ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP), usimamizi wa vihatarishi vya kisheria (Legal risk management), pamoja na matumizi ya Akili Unde (Artificial Intelligence) katika taaluma ya sheria.



Mhe. Maneno alitumia fursa hiyo, kuwasisitiza Mawakili wa Serikali kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, wakati wa Ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mawakili wa Serikali (TPBA) kwa mwaka 2026, katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

Aidha, aliwataka Mawakili wa Serikali kuendelea Kusoma na Kutafakari kwa kina Kitabu cha Falsafa ya Sheria ya Mama Samia (Mama Samia Doctrine of Law) ili kuelewa dira ya uongozi na maendeleo ya Taifa, pamoja na kuongeza kasi na ufanisi katika uchakataji wa masuala ya kisheria, hususan upekuzi na uandaaji wa mikataba, bila kuathiri ubora wa kazi na kwa kuzingatia kikamilifu sheria, kanuni, miongozo na maslahi ya Taifa.

Mhe. Maneno alieleza kuwa Kauli mbiu ya mafunzo ya Bespoke kwa Mawakili wa Serikali 2026, *"Repositioning State Attorneys for Strategic Legal Leadership in Realizing Tanzania Development Vision 2050,"* imeendelea kuwakumbusha Mawakili wa Serikali wajibu wao wa kujiendeleza kitaaluma ili waendeleo kuwa nguzo muhimu katika kusimamia utawala wa sheria, kulinda rasilimali za umma, na kutoa ushauri wa kisheria unaochochea maendeleo endelevu ya Taifa.

Mawakili wa Serikali kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa (RS & LGAs) walishiriki Mafunzo ya Bespoke 2026 yaliyofanyika kwa siku 3 kuanzia tarehe 15 hadi 17, 2026 Jijini Arusha.

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Zainab A. Katimba akipokea tuzo kutoka kwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Samwel M. Maneno wakati wa kufunga Mafunzo ya Bespoke kwa Mawakili wa Serikali, Jijini Arusha.

“MIONGOZO YA MAAMUZI YA KUSHTAKI NA UTAIFISHAJI MALI ILETE TIJA KATIKA UTOAJI HAKI” – NAIBU DPP

- Na Rebecca Kwandu -



Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, Bi. Bibiana Kileo akikata utepe kuashiria uzinduzi wa Miongozo ya Maamuzi ya Kushtaki, Utaifishaji na Urejeshaji Mali pamoja na Mpango wa Kurejesha, Kutaifisha na Kusimamia Mali katika hafla iliyofanyika Jijini Arusha.

Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, Bi. Bibiana Kileo, alisema miongozo iliyohuishwa ya Maamuzi ya Kushtaki, Utaifishaji na Urejeshaji Mali pamoja na Mpango wa Kurejesha, Kutaifisha na Kusimamia Mali inapaswa kuleta tija, kuongeza ufanisi na kuboresha ubora wa utekelezaji wa majukumu katika taasisi za haki jinai.

Bi. Kileo aliyasema hayo tarehe 23 Juni, 2026 Jijini Arusha wakati wa hafla ya uzinduzi wa miongozo hiyo, ambapo aliwashukuru wadau mbalimbali walioshiriki kikamilifu katika mchakato wa kuiboresha na kuihuisha. Alieleza kuwa maboresho yaliyofanyika yametokana na uzoefu wa utekelezaji wa miongozo ya awali na hitaji la kuimarisha usimamizi wa masuala ya utaifishaji, urejeshaji na usimamizi wa mali zinazotokana na uhalifu.

Alisema miongozo hiyo itasaidia kutatua changamoto zilizokuwa zikijitokeza katika utekelezaji wa majukumu hayo na kuleta mfanano wa utendaji kazi miongoni mwa watendaji. Aidha, amewataka viongozi na watendaji wote kuhakikisha miongozo hiyo inatekelezwa kikamilifu na haitabaki kuwa nyaraka za kuwekwa kabatini bila kutumika.

Akizungumzia dhamira ya Serikali, Bi. Kileo alisema Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kuwekeza katika kuboresha mfumo wa haki jinai kupitia maboresho ya sera, miundombinu na mazingira ya kazi ili kuwezesha utoaji wa huduma bora na haki kwa wananchi.

Alisisitiza umuhimu wa kufanya tathmini ya utekelezaji wa miongozo hiyo baada ya muda maalum ili kupima mchango wake katika kuimarisha utendaji kazi na kufikia matokeo yaliyokusudiwa.

“Miongozo hii itakuwa na maana zaidi ikiwa italeta mabadiliko chanya katika usimamizi wa mali zinazotokana na uhalifu, kuongeza kasi ya utendaji na kuhakikisha haki inaonekana kutendeka kwa manufaa ya taifa letu.” Alisema Bi. Kileo.

Sambamba na hayo, Bi. Kileo alieleza umuhimu wa kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu sheria zinazohusu utaifishaji wa mali ili kuongeza uelewa wa jamii na kuimarisha ushirikiano katika mapambano dhidi ya uhalifu.

WAKILI MKUU WA SERIKALI ASHIRIKI UZINDUZI WA KAMATI ZA USHAURI WA KISHERIA NGAZI YA MKOA NA WILAYA

- Na Prisca Ulomi -



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari akitoa msaada wa Sheria bila malipo kwa mwananchi wakati wa Kliniki ya Sheria Bila Malipo Mkoa wa Dar es Salaam iliyofanyika kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja Jijini Dar es Salaam.

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi aliwaongoza watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kushiriki Uzinduzi wa Kamati ya Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa na Wilaya na Kliniki ya Sheria bila malipo katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya uzinduzi wa kamati hizo, Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Possi Dkt. Possi alibainisha kuwa uzinduzi wa kamati hizi na Kliniki za Msaada wa Kisheria bila malipo ni mkakati wa Serikali kuhakikisha kuwa huduma za kisheria hazibaki mijini bali zinawafikia mpaka wananchi wa ngazi ya chini ambao wengi ni wa vijijini.

Alieleza kuwa uwepo wa msaada wa kisheria bila malipo utasaidia wananchi kujua haki zao kabla ya kukibilia mahakamani kwa kuwa migogoro mingi itaweza kutatuliwa kwenye ngazi ya

jamii bila kuhitaji mchakato mrefu wa kimahakama unaoweza kupelekea shauri kuchukua muda mrefu mahakamani hasa kwa wananchi wasio na uwezo wa kulipa mawakili binafsi.

Dkt. Possi alimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza Johari kwa kuratibu na kuzindua Kamati ya Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa na Wilaya katika Mkoa wa Dar es Salaam na kuisitiza kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itaendelea kushirikiana kwa karibu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na mamlaka za mikoa ili kuhakikisha maslahi ya Serikali na haki za wananchi zinalindwa.

Akizungumza katika hotuba yake wakati wa uzinduzi wa kamati hiyo, Mgeni rasmi ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Albert Chalamila, aliwataka

Mwakili wa Serikali kutoa elimu na ushauri wa kisheria kwa wananchi watakaohudhuria Kliniki ya Sheria kwa kutumia lugha nyepesi inayoeleweka kwa urahisi na wananchi.

“Katika mkoa huu kuna changamoto nyingi za kisheria kutokana na ukubwa wa mji na mwingiliano wa kibiashara na kijamii, hivyo muwasikilize wananchi na kuwaelimisha kwa lugha nyepesi na rahisi yenye kueleweka,” alisema Mhe. Chalamila.

Aidha, Mhe. Chalamila alieleza kuwa uwepo wa kamati hizo utasaidia kupunguza mashauri au migogoro dhidi ya Serikali, kutoa huduma za ushauri wa kisheria na kutatua changamoto mbalimbali za kisheria zinazowakabili wananchi, kuwawezesha Mwakili wa Serikali kusimamia utawala wa sheria na kupunguza malalamiko ya kisheria kutoka kwa wananchi.

Vilevile, Mkuu wa Mkoa alitoa rai kwa wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam na maeneo ya jirani kujitokeza kwa wingi katika kliniki hiyo ili waweze kupata huduma za ushauri wa kisheria bure.

“Nitoe wito kwa wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam mjitokeze kwa wingi kupata huduma hii ya ushauri wa kisheria inayotolewa bure na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,” alisema Mhe. Chalamila.

Awali, akitoa neno la utangulizi kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Samwel M. Maneno alisema kuwa kuzinduliwa kwa Kamati ya Ushauri wa Kisheria na Kliniki ya Sheria katika Mkoa wa Dar es Salaam ni mwendelezo wa juhudi na nia ya dhati ya Serikali za kusogeza huduma za kisheria karibu na wananchi.

“kwa namna ya kipekee niwaashukuru sana wananchi waliojitokeza na kuungana nasi katika uzinduzi wa Kamati hii,” alisema Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Sambamba na hilo, Mhe. Maneno ameeleza kuwa Kliniki ya Sheria iliyozinduliwa itajikita katika kutoa huduma elekezi na wezeshi kwa wananchi, kutoa elimu ya kisheria kwa wananchi na kushughulikia changamoto mbalimbali za kisheria zinazowakabili wananchi katika maeneo yao.

Hizi ni Kamati zenu Mhe. Mkuu wa Mkoa na Wakuu wa Wilaya, niwaombe kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itashirikiana pamoja nanyi na naomba mztumie katika kuwasaidia wananchi kutatua kero zao,” alisema Mhe. Maneno.

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, alisema kuwa kupitia Kamati za Ushauri wa Kisheria zinazoendelea kuzinduliwa katika maeneo mbalimbali nchini Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inategemea kuwafikia wananchi wengi zaidi hususani maeneo ya vijijini.

“Nitoe wito kwa Mwakili wa Serikali kujitoe kwa Weledi katika kusikiliza malalamiko ya wananchi na kuyatafutia ufumbuzi kwa umahiri mkubwa.” Alisema Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Hafla ya Uzinduzi wa Kamati ya Kisheria na Kliniki ya Sheria bila malipo kwa Wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Seikali akiwemo, Mkurugenzi Mashtaka, Bw. Sylvester Mwakitalu, Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam Bw. Abdul Rajabu Mhinte, pamoja na Wakuu wa Wilaya wa Wilaya za Mkoa wa Dar es Salaam.

Kliniki ya Sheria bila malipo kwa wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam ilizinduliwa tarehe 16 Februari, 2026 na iliendelea hadi tarehe 22 Februari, 2026 kwa wananchi wa mkoa huo kupata huduma mbalimbali za kisheria zilizokuwa zinatolewa na Mwakili wabobevu.



Mhe. Albert Chalamila Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, akizungumza na wananchi wakati akizindua Kamati za Ushauri wa Kisheria Ngazi ya Mkoa na Wilaya na Kliniki ya Sheria Bila Malipo Mkoa wa Dar es Salaam kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam



Dkt. Ally Possi, Wakili Mkuu wa Serikali (aliyeketi kulia) akizungumza na Mkurugenzi wa Taifa wa Mashtaka, ndugu Sylvester Mwakitalu kabla ya uzinduzi wa Kamati za Ushauri wa Kisheria Ngazi ya Mkoa na Wilaya na Kliniki ya Sheria Bila Malipo Mkoa wa Dar es Salaam uliofanyika kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.

OCPD NA MIKAKATI YA MATUMIZI YA TEKNOLOJIA KATIKA UANDISHI WA SHERIA

- Na Carine Senguji -



Mwandishi Mkuu wa Sheria Bw. Onorius Njole, akitoa hotuba kuhusu mipango ya Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria kwenye kutengeneza mfumo itakayorahisisha masuala ya uandishi wa sheria wakati wa ufunguzi wa kikao cha kwanza cha baraza la Ofisi hiyo.

Katika miaka ya hivi karibuni, serikali imeanza kufanya mageuzi makubwa katika mfumo wa kutunga na kusimamia sheria nchini, hususan katika eneo la Uandishi wa Sheria Ndogo zinazotungwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mageuzi hayo yameibua maswali mengi kutoka kwa wadau wa sheria, wataalamu wa utawala wa umma na hata wananchi wa kawaida.

Mwandishi Mkuu wa Sheria nchini, Bw. Onorius Njole, alieleza kwa kina sababu za serikali kuingilia kati Uandishi wa Sheria Ndogo za Halmashauri, mafanikio yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwa ofisi yake pamoja na mipango ya baadaye ya kuboresha mfumo wa sheria nchini.

Njole alisema, Serikali iliona umuhimu wa

kuingilia kati suala la uandishi wa sheria ndogo katika halmashauri baada ya kuibuka kwa malalamiko mengi kuhusu baadhi ya sheria hizo kukiuka Katiba au kuwa na athari kwa maisha ya wananchi.

Alieleza kuwa, Sheria ni jambo nyeti katika maisha ya kila mwananchi kwa sababu zinaweza kuathiri moja kwa moja shughuli za kila siku za watu. Kwa mujibu wa Bw. Njole, mtu au taasisi inapokuwa na mamlaka ya kutunga sheria bila usimamizi madhubuti, kuna uwezekano wa kutokea matumizi mabaya ya mamlaka hayo.

“Sheria ni maisha ya kila mtu. Mtu akiamua leo kukuharibia maisha yako, anaweza kufanya hivyo kwa kutunga tu sheria ambayo ikianza kutumika maisha yako yanabadilika moja kwa moja,” alieleza Bw. Njole.

Aidha, alifafanua kuwa, sheria zinaweza kuathiri shughuli mbalimbali za kiuchumi kama biashara, huduma au ajira.

“Unaweza kuwa unafanya biashara ya shule, biashara ya bajaji au shughuli nyingine yoyote. Lakini mtu akiamua kukutoa katika mstari, anaweza kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wake, na ghafla unajikuta uko nje ya mfumo,” aliongeza.

Kutokana na hali hiyo, serikali imeweka mkazo mkubwa kuhakikisha Uandishi wa Sheria unazingatia misingi ya haki, usawa na uadilifu ili kuzuia uwezekano wa sheria kutumiwa kuonea au kuumiza makundi fulani ya jamii.

SHERIA KUKIUKA KATIBA

Moja ya sababu kubwa zilizochoea serikali kuanzisha mfumo mpya wa kusimamia Uandishi wa Sheria Ndogo ni malalamiko yaliyokuwa yakitolewa bungeni kuhusu baadhi ya halmashauri kutunga sheria zinazokiuka Katiba, kwani kabla ya mfumo mpya kuanzishwa, halmashauri zilikuwa na uhuru wa kuandaa sheria ndogo kisha kuziwasilisha kwa mamlaka husika kwa ajili ya kupitishwa. Hata hivyo, kutokana na uhaba wa wataalamu wa sheria katika baadhi ya halmashauri, mara nyingi sheria hizo zilikuwa na kasoro za kisheria

“Unakuta halmashauri imetengeneza sheri- andogo lakini sheria ndogo hiyo inakiuka Katiba au sheria nyingine za nchi. Hii ilisababisha kuwapo malalamiko mengi,” alieleza Bw. Njole.

Changamoto hiyo imeonekana zaidi katika Halmashauri ambazo hazikuwa na Wanasheria ambapo katika baadhi ya maeneo, alisema hata walimu au watumishi wa kawaida walikuwa wakipewa jukumu la kuandaa sheria ndogo licha ya kutokuwa na utaalamu wa kisheria. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria ilianzisha mfumo maalum wa kusaidia Halmashauri kuandaa Sheria Ndogo kwa kutumia mifano maalum ya sheria (templates).

Bw. Njole alieleza kuwa, OCPD imekusanya maeneo yote muhimu ambayo halmashauri hutunga Sheria Ndogo yakiwemo mazingira, mifugo, ushuru na shughuli nyingine za kiuchumi. Baada ya kufanya uchambuzi, walitengeneza mfumo wa mfano wa Sheria Ndogo ambayo halmashauri zinaweza kutumia kama mwongozo.

“Tumetengeneza ‘templates’ za sheria ndogo na kuziweka katika mfumo wa mtandao wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Halmashauri zinaweza kuzitumia kama mwongozo wa kuandaa sheria zao,” alifafanua Bw. Njole.

Kwa kutumia mfumo huo, halmashauri zinaweza kuandaa rasimu ya sheria kwa kufuata muundo uliowekwa kisha kuwasilisha kwa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa ajili ya uhakiki na kupitishwa.

TIJA YA TEKNOLOJIA

Bw. Njole alieleza kuwa, matumizi ya teknolojia katika mchakato huo yamesaidia kupunguza muda na gharama zilizokuwa zinatumiwa hapo awali ambapo alieleza kuwa zamani mchakato wa kupitisha sheria ndogo ulikuwa mrefu na wenye hatua nyingi za kiutawala. Kwa mfano, kama Halmashauri ya Nzega ingeandaa sheria ndogo ilipaswa kuwasilisha kwanza kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI (sasa iko chini

Ofisi ya Waziri Mkuu), kisha TAMISEMI ingeipeleka kwa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria. Baada ya kufanyiwa uchambuzi, sheria hiyo ingerudishwa tena TAMISEMI kabla ya kurejeshwa kwa halmashauri husika. Katika baadhi ya maeneo, sheria hizo zilipaswa pia kupitia kwa Mkuu wa Mkoa kabla ya kufika katika ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria.

“Utaratibu huu ulikuwa una chukua muda mrefu sana. Lakini sasa kila kitu kinafanyika mtandaoni, hivyo kuharakisha mchakato,” alieleza.

Katika mahojiano hayo, Bw. Njole alieleza kuwa mchakato wa kutunga sheria si rahisi kama wengi wanavyodhani kwa kuwa baadhi ya sheria zinaweza kuchukua muda mrefu sana kukamilika kutokana na umuhimu wake na idadi ya wadau wanaohusika.

“Mchakato wa kutunga sheria ni mrefu. Kuna sheria nyingine zinachukua hadi miaka kumi kukamilika,” alieleza na kutolea mfano Sheria ya Wanyamapori ambayo alisema ilichukua muda mrefu kukamilika kutokana na ushiriki wa wadau wengi wa ndani na nje ya nchi.

Alieleza kuwa sheria zinazohusu rasilimali za taifa mara nyingi huhitaji ushirikishwaji mpana ili kuhakikisha zinazingatia maslahi ya taifa na wadau wote wanaohusika.

MAFANIKIO

Tangu kuanzishwa kwa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria mwaka 2025, mafanikio kadhaa yamepatikana katika kuboresha mfumo wa sheria nchini ambapo moja ya mafanikio makubwa ni kuchapishwa kwa toleo jipya la Urekebu wa Sheria (Revised Edition) la mwaka 2023, ambapo Bw. Njole alieleza kuwa kabla ya hapo toleo la mwisho lilitolewa mwaka 2002, zaidi ya miaka 20

iliyopita. Kwa mujibu wa sheria, toleo hilo linapaswa kutolewa kila baada ya miaka 10 ili kuunganisha marekebisho yote yaliyofanywa katika sheria mbalimbali.

“Revised edition inaweka pamoja sheria na marekebisho yake yote ili iwe rahisi kwa watu kuisoma na kuielewa,” alieleza.

Mafanikio mengine ni kutafsiriwa kwa sheria zote za Tanzania kwa lugha ya Kiswahili. Bw. Njole alieleza kuwa, kwa muda mrefu sheria nyingi zilikuwa zinaandikwa kwa lugha ya Kiingereza, jambo ambalo lilikuwa changamoto kwa wananchi wengi. Kwa mujibu wake, mchakato wa kutafsiri sheria ulianza mwaka 2023 na kukamilika mwaka 2025.

“Tumetafsiri jumla ya sheria kuu 444 kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili. Hii si kazi ndogo kwa sababu baadhi ya sheria zina kurasa 200 hadi 300,” alieleza.

Bw. Njole alieleza kuwa hatua hiyo itarahisisha wananchi wengi kuelewa sheria na kushiriki katika mijadala ya kisheria.

Mageuzi mengine muhimu ni kwamba sasa miswada mipya ya sheria inaandikwa kwa lugha ya Kiswahili, hapo awali sheria nyingi zilikuwa zinaandikwa kwa Kiingereza kwa sababu wataalamu wengi walipata elimu yao kwa lugha hiyo, lakini sasa serikali imeamua kutumia Kiswahili ili kuwapa wananchi fursa ya kuelewa sheria zinazowaongoza.

“Kwa sasa sheria mpya zinaandikwa kwa Kiswahili. Hii ina maana kila Mtanzania anaweza kuisoma na hata kuikosoa,” alisema.

Akizungumzia matumizi ya teknolojia mpya kama akili unde (AI) katika Uandishi wa Sheria, alieleza kuwa Tanzania bado iko nyuma kidogo katika eneo hilo ukilinganisha na baadhi ya nchi ambazo tayari zimeanza

kutumia mifumya akili unde kusaidia katika uchambuzi wa sheria na maandalizi ya rasimu za sheria, Hata hivyo, changamoto kubwa ni kwamba Uandishi wa Sheria ni sehemu tu ya mchakato mzima wa kutunga sheria.

“Mchakato mzima wa kutunga sheria unahusisha taasisi nyingi, likiwemo Baraza la Mawaziri. Ili kutumia mifumo ya kisasa kama AI, mnyororo mzima wa taasisi lazima uwe tayari,” alieleza. Aliongeza kuwa, kama sehemu moja ya mfumo itatumia teknolojia lakini nyingine zikaendelea kutumia nyaraka za karatasi, ufanisi wa mfumo huo hautakuwa mkubwa.

Aidha, Bw. Njole aliendelea kusesitiza kuwa, kwa siku zijazo, ofisi yake ina mpango wa kuhakikisha kila mkoa nchini unakuwa na mwandishi wa sheria kutoka katika Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, hatua itakayosaidia kutoa huduma za haraka kwa taasisi mbalimbali zinazohitaji ushauri wa kisheria. Mbali na serikali za mitaa, anasema taasisi nyingi za serikali zinahitaji huduma za uandishi wa sheria ndogo mara kwa mara.

Kutokana na tahmini ya jumla, OCPD imejipanga kuunga mkono juhudi za Serikali kwa vitendo katika kuendana na kasi ya teknolojia kwa kuweka mifumo thabiti ya TEHAMA itakayosaidia utolewaji mzuri wa huduma za uandishi wa sheria na kuwafikia wataanzania wote kwa wakati na ufanisi mkubwa.



Watumishi wa OCPD wakiwa katika Kikao cha Kwanza cha Baraza la Wafanyakazi Jijini Dar es Salaam.

“SHERIA INA THAMANI PALE INAPOBADILISHA MAISHA YA WATU”

- Na Lela Muhaji -



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari akizungumza wakati wa Uzinduzi wa Kitabu cha Falsafa ya Sheria ya Mama Samia, uliofanyika Jijini Dar es Salaam.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari alisema kuwa, Sheria zinapaswa kutumika kama nyenzo ya kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kufungua fursa, kuongeza uwajibikaji, kuvutia uwekezaji, kuongeza mapato ya Serikali, kuboresha elimu na afya.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliyasema hayo, wakati wa Uzinduzi wa Kitabu kipya kiitwacho **"Falsafa ya Sheria ya Mama Samia: Utekelezaji wake katika Mageuzi ya Kiuchumi na Kijamii"**, ulioratibiwa na Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania na kufanyika katika Ukumbi wa Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Julai 10, 2026.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisisitiza kuwa, thamani ya Sheria hupimwa kwa uwezo wake wa kuboresha maisha ya wananchi, kuvutia uwekezaji, kuimarisha uwajibikaji na kuongeza ufanisi wa utoaji huduma kwa Wananchi.

Aidha, Mhe. Johari alieleza kuwa, wazo la kuandika kitabu hicho lilitokana na tafakuri ya kina kuhusu nafasi ya sheria katika kuchochea maendeleo, ambapo waandishi wa Kitabu hicho walitaka kujibu maswali muhimu kuhusu namna marekebisho ya sheria, mabadiliko ya sera na maboresho ya taasisi yalivyochangia kuleta matokeo chanya katika uchumi na ustawi wa jamii.

"Kitabu hiki hakikuandikwa kwa lengo la kusifu tu mazuri yaliyofanyika, bali hii ni kazi ya uchambuzi wa kitaaluma inayotumia ushahidi, takwimu na nyaraka rasmi kuchunguza kama mageuzi ya kisheria na kisera yaliyofanyika tangu Machi mwaka 2021 yanaonesha mfumo unaoweza kueleweka, kupimwa na kujadiliwa kitaaluma." Alisema Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Aidha, Mhe. Johari alifafanua kuwa, lengo kuu lilikuwa kuhamisha mjadala kutoka kwenye kauli za jumla kwenda kwenye ushahidi wa kisayansi kwa kuangalia matokeo halisi ya marekebisho ya sheria na sera kwa wananchi.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, alisema kitabu hicho kinaonesha katika kipindi cha Awamu ya Sita kumekuwa na mwelekeo mpya wa kutumia sheria, sera, taasisi na mifumo ya utekelezaji kujenga mazingira ya maridhiano, uwekezaji, uwazi, haki, utoaji huduma bora na maendeleo ya wananchi.

"Ndiyo maana tuliona ni muhimu kuuweka mwelekeo huu katika maandishi ili uwe rejea kwa watunga sera, wasomi, watafiti na wadau wengine wanaotaka kuelewa nafasi ya sheria katika maendeleo ya taifa," alisema.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali alieeza kuwa kwa mujibu wa majukumu ya kikatiba ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ushauri wa kisheria haupaswi kuishia katika tafsiri ya sheria pekee, bali unapaswa kusaidia Serikali kufanya maamuzi yanayolinda maslahi ya taifa, kupunguza migogoro, kuvutia uwekezaji na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

"Sheria nzuri zinapaswa kuwa wazi, zenye mantiki, zinazotekelezeka na zinazotabirika, huku zikitoa mazingira rafiki kwa ukuaji wa uchumi na kuimarisha taasisi za umma." Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Katika hatua nyingine Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kusimamia ubora wa utungaji wa sheria, usimamizi wa mikataba ya Serikali, matumizi ya mifumo ya kidijitali katika huduma za kisheria pamoja na kujenga uwezo wa mawakili wa Serikali ili waendane na mabadiliko ya uchumi, teknolojia na mazingira ya kimataifa.

"Sheria ina thamani pale inapoboresha maisha ya watu, kuvutia uwekezaji, kuongeza mapato ya Serikali, kuboresha elimu na afya, kupanua upatikanaji wa nishati, kulinda taarifa binafsi, na kupunguza migogoro." Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Vilevile, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alitoa pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake ambao umekuwa chachu kwa maendeleo ya nchi.

"Napenda kutumia nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuongoza nchi kwa mwelekeo wa maridhiano, mageuzi, ustawi na maendeleo." Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Sambamba na hilo, Mhe. Johari aliwapongeza na kuwashukuru waandishi, wahakiki, wahariri, Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania, Wizara ya Katiba na Sheria, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, na wadau wote waliofanikisha kupatikana kwa kitabu hicho.

Kitabu cha Falsafa ya Sheria ya Mama Samia kinakusudia kuwa rejea muhimu sana kwa Serikali, Wasomi, Watafiti, Mawakili, Sekta Binafsi na wadau wengine katika kuendeleza mjadala kuhusu nafasi ya sheria kama nguzo ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.



Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhe. Hemed Suleiman Abdullah (katikati) akimkabidhi Mwandishi Mkuu wa Sheria Bw. Onorius Njole (kulia) Kitabu cha Falsafa ya Sheria ya Mama Samia, katika halifa ya Uzinduzi wa Kitabu hicho iliyofanyika Jijini Dar es Salaam.

UENDESHAJI WA MASHAURI YA JINAI MAHAKAMANI KWA MFUMO WA KIFICHO

- Na Renatus Mkude -

Katika mfumo wa utoaji haki, mashauri mengi mahakamani husikilizwa kwa njia ya wazi ili jamii iweze kuona na kuelewa jinsi haki inavyotendeka. Ndiyo maana kuna msembo maarufu wa kisheria unaosema *"haki haipaswi tu kutendeka, bali pia ionekane inatendeka."* Hata hivyo, kuna mazingira maalum ambapo mahakama hulazimika kusikiliza mashauri kwa kificho ili kulinda maslahi ya wahusika au usalama wa taifa.

Uendeshaji wa mashauri kwa mfumo wa kificho ni utaratibu unaotumiwa na

mahakama kusikiliza baadhi ya kesi bila kuruhusu watu wengine wasiokuwa wahusika kuhudhuria, wakiwemo wakati mwingine wanahabari au ummaa kwa ujumla. Hatua hii huchukuliwa pale ambapo taarifa zinazojadiliwa mahakamani ni nyeti au zinaweza kuathiri faragha, usalama au heshima ya wahusika endapo zitajulikana hadharani.

Kwa kawaida, Jaji au Hakimu anaweza kuamua kuwa shauri zima lisikilizwe kwa kificho au sehemu fulani tu ya ushahidi ipokelewe kwa njia hiyo. Hali hii hutokea pale ambapo kuna ushahidi wenye taarifa nyeti, siri za kitaifa au maelezo binafsi yanayohitaji kulindwa.

Maana ya sikilizaji wa Mashauri kwa kificho

Kwa ufupi, usikilizaji wa mashauri kwa kificho ni utaratibu wa kimahakama unaoruhusu kesi kusikilizwa bila uwepo wa umma. Ni wahusika wa shauri pekee kama vile mahakama, waendesha mashtaka, mawakili wa utetezi, mashahidi na wahusika wa kesi ndio huruhusiwa kuwepo. Kwa mujibu wa Wex definition team, Cornell Law School, Legal Information Institute 2023, "[in camera proceedings](#)" ni utaratibu ambapo mahakama husikiliza shauri au sehemu ya ushahidi bila uwepo wa umma au wanahabari.

Nje ya mahakama, dhana hii inaweza pia kufanana na mikutano ya ndani ya taasisi au kampuni ambapo masuala nyeti kamataarifa za fedha, masuala ya wafanyakazi au mbinu za biashara hujadiliwa bila uwepo wa watu wa nje.

Historia ya mfumo huu

Mfumo wa kusikiliza mashauri kwa kificho umeanza kutumika tangu zamani katika nchi nyingi duniani kama vile Uingereza, Marekani na India. Awali ulitumiwa zaidi kulinda haki na utu wa watu, hasa wahanga wa makosa nyeti.

Kadri mifumo ya haki ilivyokuwa ikiendelea kuboreshwa, utaratibu huu ulianza pia kutumika kama njia ya kulinda mashahidi na wahanga wa uhalifu. Lengo lake lilikuwa kuzuia taarifa nyeti zisisambae kwa umma na hivyo kulinda usalama na faragha ya wahusika.

Kwa kiasi kikubwa, utaratibu huu ulipata nguvu kupitia mikataba ya kimataifa na kikanda kama vile Mkataba wa **Kimataifa wa Haki za Kisiasa na Kiraia (ICCPR)** 1966 Ibara ya 2(2),(3b), 10(1)(3),14(4) na Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu Ibara ya 3, 4 na 5 inayolenga kulinda haki za binadamu. Mikataba hiyo ilisisitiza haki ya mtu kulindwa utu wake, kusikilizwa kwa haki na kuepuka udhalilishaji hadharani. Misingi hiyo pia ilisababisha kuwepo kwa mikataba maalum inayolinda makundi kama wanawake na watoto.

Hali ilivyo Nchini Tanzania

Nchini Tanzania, chini ya Ibara 12 na 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalinda haki na usawa mbele ya sheria pamoja na heshima ya utu wa kila mtu. Kwa ujumla, kanuni ya msingi ni kwamba mashauri yote yanapaswa kusikilizwa katika mahakama za wazi ili jamii iweze kushuhudia utoaji haki.

Hata hivyo, sheria zimeweka utaratibu wa kusikiliza baadhi ya mashauri kwa kificho pale inapobidi. Mashauri hayo yanaweza kujumuisha makosa ya kujamiana, mashauri ya watoto, ushahidi wa wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu, pamoja na mashauri ya nidhamu katika taasisi mbalimbali.

Katika baadhi ya kesi, mahakama inaweza kutoa amri maalum kuruhusu shauri kusikilizwa kwa kificho endapo itaona kuwa kuna sababu za msingi za kufanya hivyo.

Sheria na Kanuni Zinazosimamia Utaratibu huu

Usikilizaji wa mashauri kwa kificho unategemea misingi ya sheria mbalimbali nchini. Miongoni mwa sheria hizo ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (Sura ya 20), Sheria ya Ushahidi (Sura ya 6), Sheria ya Ugaidi, Sheria ya Mahakimu pamoja na Sheria ya Mtoto.

Mbali na sheria hizo, zipo pia kanuni na miongozo mbalimbali ya kitaaluma kama vile miongozo ya Jaji Mkuu kuhusu mashauri ya watoto na miongozo ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuhusu uchunguzi na uendeshaji wa baadhi ya makosa kama vile ubakaji.

Katika mfumo wa haki jinai, taasisi kadhaa hushiriki katika mnyororo wa kushughulikia mashauri yanayoweza kusikilizwa kwa kificho. Taasisi hizo ni pamoja na Mahakama, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Jeshi la Polisi, Idara ya Ustawi wa Jamii na Magereza.

Mahakama ndiyo yenye mamlaka ya mwisho ya kuamua kama shauri lisikilizwe kwa kificho, lakini utekelezaji wake unategemea pia ushirikiano wa taasisi nyingine katika mfumo wa haki jinai.

Sambamba na hayo mfumo wa kusikiliza mashauri kwa kificho una faida kadhaa: Kwanza, hulinda utu na faragha ya wahusika, hasa wahanga wa uhalifu. Pili, husaidia kulinda usalama wa siri za nchi. Tatu, huongeza ulinzi wa mashahidi na kupunguza uwezekano wa kushawishiwa au kutishwa ili kupotosha ushahidi.

Aidha, mfumo huu huzuia mjadala wa mapema wa kesi au hukumu kabla ya mahakama kutoa uamuzi wake.

Hata hivyo, mfumo huu pia una changamoto. Baadhi ya watu wanaona kuwa unaweza kupunguza uwazi katika utoaji haki kwa sababu umma hauwezi kufuatilia mwenendo wa kesi hizo. Pia, wanafunzi na wanazuoni wa sheria hukosa fursa ya kujifunza kutokana na kutoruhusiwa kuhudhuria katika uendeshaji wa mashauri hayo.

Changamoto nyingine ni kwamba jamii inaweza kukosa nafasi ya kupata elimu ya kisheria kupitia kesi hizo, tofauti na mashauri ya wazi ambayo huonekana kama darasa kwa umma.

Hitimisho

Katika ulimwengu wa sasa unaozidi kuboresha mifumo ya haki jinai, suala la ulinzi wa mashahidi na wahanga wa uhalifu limekuwa muhimu sana. Usikilizaji wa mashauri kwa kificho ni moja ya njia zinazosaidia kufanikisha lengo hilo.

Hata hivyo, ni muhimu kuhakikisha kuwa mfumo huu unatumiwa kwa uangalifu ili usipunguze uwazi katika utoaji haki. Tanzania inaweza kuendelea kujifunza kutoka nchi nyingine zilizoendeleza mfumo huu ili kuboresha zaidi mifumo yake ya haki jinai.



WAKILI MKUU WA SERIKALI AKAGUA MRADI WA UJENZI WA JENGO LA OWMS, DODOMA - Na Prisca Ulomi -



Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (wa pili kushoto) akipatiwa maelezo na mkandarasi wa SUMA JKT na Kanali Saul Chiwanga kuhusu maendeleo ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali lililopo Mji wa Serikali, Mtumba, Jijini Dodoma.

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi alikagua mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali unaoendelea kujengwa kwenye mji wa Serikali, Mtumba Jijini Dodoma ambao umefikia kiwango cha asilimia 73.

Dkt. Possi alimtaka mkandarasi, SUMA JKT na mshauri elekezi, TBA kuhakikisha kuwa jengo hilo linakamilika kwa kuzingatia viwango na ubora unaotakiwa ili liweze kutumika kwa muda mrefu.

Pia, alimwelekeza mkandarasi kuwa kisima cha maji ya ardhi kilichochimbwa kitunzwe ili maji yake yaweze kutumika wakati wa msimu wa kiangazi na matumizi mbalimbali ikiwemo utunzaji wa mazingira ili kuifanya Dodoma kuwa ya kijani.

“Nategemea kupata jengo lenye ubora na viwango vinavyotakiwa ili liweze kutumika kwa muda mrefu kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wananchi na kuongeza tija na ufanisi katika mnyororo wa utoaji haki nchini,” alisisitiza Dkt. Possi.

Pia, aliongeza kuwa tunahitaji jengo liishe mapema mwaka huu ili tuhamie Dodoma kwa kuwa Ofisi hii inafanya kazi kwa karibu na Mahakama ya Tanzania ambayo tayari imehamia Dodoma.

Dkt. Possi aliambatana na Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, wakilishi wa mkandarasi, Meneja Ujenzi Kanda ya Mashariki wa SUMA JKT, Kanali Saul Chiwanga na wakilishi wa mshauri elekezi, Kaimu Meneja Miradi wa TBA, ndugu Daniel Nkruma.

SERIKALI NA MIKAKATI YA KUPAMBAN NA UTAKATISHAJI FEDHA

- Na Carine Senguji -



Mkurugenzi Msaidizi Divisheni ya Uandishi wa Sheria, Bi. Chresencia Mathayo akitoa mafunzo kwa Mawakili Caption wa Serikali kuhusu Sheria ya Fedha ya Mwaka 2026, iliyoanza kutumika Julai, 2026.

Li kupunguza matumizi ya fedha taslimu na kuziba mianya ya utakatishaji wa fedha haramu, Serikali imeweka utaratibu wa malipo kwa njia za kidijitali katika miamala mbalimbali nchini.

Utaratibu huo umewekwa kupitia marekebisho ya Sheria ya Miamala ya Kielektroniki, Sura ya 442 na kutungwa kwa Amri ambayo inabainisha miamala inayopaswa kufanyika kwa njia ya kidijitali, kwa mujibu wa Amri hiyo, mtu yeyote anayefanya au kupokea malipo katika miamala iliyobainishwa anapaswa kutumia njia ya kielektroniki.

Akizungumza wakati wa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali kuhusu mabadiliko yaliyotokana na Sheria ya Fedha ya mwaka 2026, Mkurugenzi Msaidizi wa Divisheni ya Uandishi wa Sheria kutoa Ofisi ya

Mwandishi Mkuu wa Sheria (OCPD), Bi. Chresencia Mathayo alisema hatua hiyo inalenga kujenga mfumo wa malipo ulio salama na unaoweza kufuatiliwa kwa urahisi hivyo kusaidia kuziba mianya ya utakatishaji wa fedha haramu nchini.

“Matumizi ya njia za kidijitali katika miamala yanarahisisha ufuatiliaji wa malipo, yanaongeza usalama wa fedha na yatasaidia kuziba mianya inayoweza kutumika katika utakatishaji wa fedha haramu, ukwepaji wa kodi na vitendo vingine vya uhalifu wa kifedha,” alisema Bi. Chresencia.

Kwa mujibu wa Amri hiyo, njia zinazotambuliwa kuwa za kidijitali zinajumuisha fedha kwa simu, uhamisho wa fedha kupitia benki, kadi za malipo, mashine za malipo (POS), huduma za benki kwa njia

ya mtandao au simu pamoja na mifumo ya malipo ya Serikali.

Bi. Chresencesia alieleza kuwa Amri hiyo imebainisha miamala yote ambayo inapaswa kufanyika kidijitali.

“Miongoni mwa miamala ambayo ni lazima kufanyika kwa njia ya kidijitali ni pamoja na malipo ya ada za shule, malipo ya nauli kwenye vyombo vya usafiri (mabasi ya mwendokasi, madaraja, vivuko, tekisi mtandao, mabasi ya masafa marefu, usafiri wa anga na reli), huduma kwenye maduka makubwa (supermarket), huduma za malazi na chakula kwenye mahoteli na migahawa, huduma za kitalii, malipo ya kupangisha au kuuza jengo, shamba au kiwanja, malipo ya uuzaji na ununuzi wa magari na malipo yanayofanyika kupitia vyama vikuu vya ushirika na Vyama vya Ushirika vya Mazao na Masoko (AMCOS) katika mazao ya kimkakati,” alisema Bi. Chresencia.

Mkurugenzi Msaidizi wa Divisheni ya Uandishi wa Sheria OCPD, aliendelea kwa kusema kuwa sambamba na hatua hiyo, Kanuni za Utoaji wa Leseni za Biashara zimerekebishwa pia ili maombi ya leseni

mpya na maombi ya kuhuisha leseni kwa wafanyabiashara wote yaambatishwe na uthibitisho wa matumizi ya mfumo au kifaa cha kupokea malipo kwa njia ya kidijitali, ikijumuisha Lipa Namba au TANQR

“Kwa wafanyabiashara wote ambao bado hawana njia za malipo ya kidijitali watashindwa kuhuisha leseni zao za biashara pindi muda wake unapoisha mpaka pale watakapokuwa na njia za malipo ya kidijitali, hatua hii inalenga kuhakikisha kuwa miamala katika biashara hizo inapitia katika mifumo rasmi ya kifedha,” aliendelea Bi. Chresencia.

Bi. Chresencia alisema maboresho hayo hayalengi tu ukusanyaji wa mapato, bali pia kupunguza gharama na hatari zinazotokana na matumizi ya fedha taslimu, ikiwemo gharama za kutunza na kusafirisha fedha pamoja na hatari ya wizi na upotevu wafedha.

Mabadiliko hayo yameanza kutumika rasmi Julai 1, 2026, hivyo wananchi, wafanyabiashara na watoa huduma wanahimizwa kujiandaa na kutumia njia rasmi za malipo ya kidijitali katika miamala iliyobainishwa.



Mwakili wa Serikali wakipatiwa mafunzo ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2026, Jijini Dodoma

BUNGE LAPITISHA MUSWADA WA SHERIA NA 2 WA MWAKA 2026

- Na Ally Masaniga -



Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari akiwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na.2) ya Mwaka 2026 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 02) Bill, 2026), Jijini Dodoma.

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limepitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2026 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 02) Bill, 2026), tarehe 2 Septemba, 2026 katika Mkutano wa Nne, Kikao cha Sita cha Bunge kilichofanyika Bungeni Jijini Dodoma.

Akizungumza wakati wa kuwasilisha Muswada huo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari alisema kuwa Muswada unakusudia kufanya maboresho katika Sheria kuu Saba.

"Malengo ya marekebisho haya ni kuboresha utekelezaji wa masharti ya sheria husika na kuzifanya sheria hizi ziendane na wakati na kuleta tija kwa wananchi."
Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Aidha, Mwanasheria Mkuu alizitaja Sheria zilizofanyiwa marekebisho ni pamoja na Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Sura ya 116, Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287, Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288 na Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa, Sura ya 61.

Mhe. Johari aliendelea kueleza kuwa Sheria ya Mamlaka ya Nchi Katika Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 449, Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, Sura ya 138, Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283 nazo zimejumuishwa katika Muswada huo.



Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari (watatu kushoto) katika picha ya pamoja na Viongozi wa Jamii ya Wafugaji mara baada ya Kikao cha Bunge Jijini Dodoma.

Katika hatua nyingine, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema kuwa Serikali itaendelea kufanya maboresho katika Sheria mbalimbali ili kuhakikisha kuwa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inatekekelezwa ipasavyo.

“Kwa Niaba ya Serikali, niliahidi Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali itaendelea kufanya maboresho ya sheria ili kuhakikisha kuwa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050

iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu inatekekelezwa ipasavyo.” Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mara baada ya Bunge kupitisha Muswada huo, ulipelekwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kusainiwa na kuwa Sheria kamili za nchi.

“LENGO LETU NI KUREJESHA TABASAMU KWA WANANCHI”- MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

- Na Ally Masaniga -



Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari akizungumza katika hafla ya kukabidhi magari kwa Kampuni ya SEMA Limited iliyofanyika katika Viwanja vya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, Manispaa ya Singida.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari alishiriki hafla ya kukabidhi magari kwa Kampuni ya SEMA Limited iliyofanyika katika Viwanja vya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, tarehe 22 Aprili, 2026.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema kuwa, zoezi hilo la kukabidhi magari ni matokeo ya Kliniki ya Kisheria bila malipo iliyofanyika kuanzia tarehe 19 hadi 25 Aprili, 2025 katika Viwanja vya Stendi ya zamani Manispaa ya Singida, Mkoa wa Singida.

Aidha, Mhe. Johari alieleza kuwa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilipokea lalamiko la Bw. Lameck Muyanzi (Meneja wa Karakana wa Sustainable Environment Management Action (SEMA) aliyelalamikia Kampuni ya TAOMTRA Limited (Hussein

Mjili na Getruda Agripa Mwashambwa Dalali wa Mahakama) kwa kukamata magari matano (5) ya Kampuni ya SEMA na kuyauza magari husika isivyo halali.

“Tulipokea lalamiko kutoka Kampuni ya SEMA na nilikabidhi kwa watalamu kwa ajili ya kulishughulikia na matokeo yake ndio haya mnayaona leo hapa.” Alieleza Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, alisema kuwa Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Ofisi ya Upelelezi Mkoa wa Singida pamoja na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Mkoa wa Singida, ilifanya jitihada za kuyarejesha magari hayo kwa kampuni ya SEMA.

“Dhumuni kubwa la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kutatua changamoto za wananchi katika hali ya kawaida ili kuipinguzia Mahakama mzigo.” Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Vilevile, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alieleza kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea na utaratibu wa kutembelea maeneo mbalimbali nchini na kutatua kero mbalimbali za kisheria zinazowakabili wananchi.

“Tutaendelea kuwasaidia wananchi kutatua kero zao za kisheria na kuwarejeshea tabasamu wananchi kama alivyoagiza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.” Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mkuu wa Wilaya ya Singida Mhe. Godwin Gongwe alimpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi kubwa anayoifanya ya kutatua changamoto mbalimbali za kisheria zinazowakabili wananchi hususani wa Mkoa wa Singida.

“Tunakupongeza sana Mhe. Hamza Johari kwa kazi kubwa unayoifanya sisi Singida tunakuona kama ni Alama ya Haki.” Alisema Mhe. Gondwe.

Awali akitoa neno la utangulizi Mkurugenzi wa Divisheni ya Uratibu na Ushauri wa Kisheria Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Bi. Neema J. Ringo alizishukuru Taasisi mbalimbali zilizoshiriki katika kushughulikia lalamiko hilo na kuweza kulitua na kuwezesha Kampuni ya SEMA kurejeshewa magari yaliyokuwa yameshikiliwa na Kampuni ya TAOMTRA Limited.

“Tunavishukuru vyombo mbalimbali vya Serikali vilivyohusika katika kutatua suala hili, Serikali ilifanya kazi kama timu na mafanikio tumeyaona.” Alisema Bi. Ringo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Kampuni ya SEMA Bw. Ivo Manyako alimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Watendaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushughulikia changamoto iliyokuwa inawakabili na kufanikisha kurejeshewa magari ya Kampuni ya SEMA yaliyokuwa yanashikiliwa na Kampuni ya TAOMTRA Limited.

“Kwa niaba ya Kampuni ya SEMA tunakushukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kulibeba suala hili na kulitua kwa Weledi, na pengine kwa Weledi huo ndio uliomfanya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu kukuteua tena kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.” Alisema Bw. Manyako.

Kampuni ya SEMA Limited ilifanikiwa kurejeshewa jumla ya magari manne (4) ambayo ni Toyota Land Cruiser S/Wagon lenye namba za usajili T465 AED; Isuzu Winch lenye namba za usajili T418 AED; Isuzu Tipa lenye namba za usajili T423 AED na Land Rover 101 Station Wagon lenye namba za usajili T412 AED. Aidha, walalamikiwa walitakiwa kulipa kiasi cha Shilingi 27,750,000 kufidia gari moja lililokuwa limeharibiwa.

UTAIFISHAJI WA MALI: SILAHA MUHIMU KATIKA KUPAMBANA NA BIASHARA YA DAWA ZA KULEVYA

- Na Juma Mahona -



Gari lililotaifaishwa ambalo limetokana na uhalifu wa kubeba Dawa za Kulevya.

Mapambano dhidi ya biashara ya dawa za kuleva hayaishii kwa kuwakamata nakuwafikisha wahalifu mahakamani pekee, bali pia kuhaakikisha hawafaidiki na mali walizotumia au walizozipata kutokana na uhalifu. Utaifishaji wa mali huvunja uwezo wa mitandao ya kihalifu kwa kuwaondolea wahalifu rasilimali wanazotumia kuendesha shughuli zao, huzuia uhalifu kujirudia na kuimarisha utekelezaji wa haki. Ndiyo maana Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu sura 256 iliyofanyiwa marejeo 2023 inaruhusu Mahakama kuamuru mali zilizotumika kutendea uhalifu au mali zilizopatikana kwa njia ya uhalifu zitaifishwe kuwa mali ya Serikali.

Mfano mzuri wa utekelezaji wa sheria hiyo ni shauri namba 27973/2025 lililohusu watuhumiwa watatu waliokamatwa

wakisafirisha dawa za kulevya aina ya bangi kutoka Afrika Kusini kuingia Tanzania. Katika shauri hilo, Mahakama iliamuru kutaifishwa kwa lori aina ya mercedes benz lililotumika kusafirisha dawa hizo pamoja na fedha ambao ni mazalia ya uhalifu zilizopatikanakutokana na mauzo ya matunda yaliyokuwa yametumika kuficha dawa hizo.

Safari ya shauri hili ilianza tarehe 7 Agosti 2023 katika mpaka wa Tunduma, Mkoa wa Songwe. Mafisa wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) waliwakamata Constantine Onesmo Msuya, Henry Samson Hao na Innocent Gervas Mwanja wakiwa wameingia nchini kutoka Afrika Kusini kwa kutumia lori aina ya Kusini kwa kutumia lori aina ya Mercedes Benz Axor Truck. Kwa nje, lori hilo lilionekana

kubeba mzigo wa kawaida wa matunda aina ya tufaa (apples) na peasi (pears), lakini uchunguzi uliofanyika ulibaini kuwa ndani yake kulikuwa na pakiti 77 za bangi.

Baada ya uchunguzi wa Mkemia Mkuu wa Serikali, ilithibitika kuwa dawa hizo zilikuwa aina ya bangi yenye uzito wa kilogramu 81.3. Pia, maafisa walikamata simu tano za mkononi pamoja na maboksi 901 ya matunda yaliyokuwa ndani ya lori hilo.

Ili kuhakikisha mali hizo hazihamishwi wala kupotea wakati kesi ikiendelea, upande wa Jamhuri uliomba Mahakama ya Wilaya ya Momba itoe amri ya zuio. Mahakama ilikubali ombi hilo tarehe 17 Agosti 2023. Kutokana na matunda hayo kuwa yanaharibika kwa haraka, Mahakama iliruhusu yauzwe kwa mnada wa hadhara. Mauzo hayo yalizalisha shilingi milioni 15.8 ambazo zilihifadhiwa katika akaunti maalumu ya Serikali iliyoko Benki Kuu ya Tanzania zikisubiri uamuzi wa mwisho wa Mahakama.

Shauri la msingi Mahakama ya Hakim Mkazi Mkoa wa Songwe, Vwawa. Katika hatua hiyo, washitakiwa waliachiliwa huru. Hata hivyo, Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) hakuridhika na uamuzi huo alikata rufaa katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Mbeya.

Tarehe 18 Julai 2025, Mahakama Kuu ilibatilisha uamuzi wa Mahakama ya chini na kuwatia hatiani washitakiwa wote watatu kwa kosa la kusafirisha dawa za kulevy. Kila mmoja alihukumiwa kifungo cha miaka 30 jela. Hukumu hiyo iliipa nafasi Ofisi ya

Taifa ya Mashtaka kuendelea na hatua nyingine muhimu ya kuomba mali zilizotumika na zilizotokana na uhalifu huo kuomba Mahakamani zitaifishwe kwa mujibu wa Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu.


Katika maombi hayo, upande wa Jamhuri uliieleza Mahakama kuwa lori hilo lilikuwa chombo kilichotumika kutekeleza uhalifu (instrumentality of crime), huku fedha zilizotokana na mauzo ya matunda zikiwa mali zilizotokana na uhalifu (proceeds of crime). Serikali pia iliomba simu tano za mkononi zitaifishwe kwani zilitumika kuratibu shughuli za mtandao huo wa biashara ya dawa za kulevy.

Baada ya kuchambua ushahidi, Mahakama ilibaini kuwa kulikuwa na ushahidi wa kutosha kuthibitisha kuwa lori pamoja na fedha hizo zilihusika moja kwa moja na uhalifu huo. Tarehe 27 Aprili 2026, Mahakama ya Hakim Mkazi Mkoa wa Songwe iliamuru lori aina ya Mercedes Benz Axor Truck pamoja na shilingi milioni 15.8 zitaifishwe kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mujibu wa sheria, baada ya kupita siku 30 za kukata rufaa bila pingamizi lolote, mali hizo hukabidhiwa rasmi kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha kwa niaba ya Serikali.

Shauri hili linaonesha kuwa mapambano dhidi ya uhalifu hayaishii kwenye hukumu za kifungo pekee. Utaifishaji wa mali ni hatua muhimu inayowanyang'anya wahalifu faida walizotarajia kupata kutokana na uhalifu wao. Kwa kufanya hivyo, sheria inalinda maslahi ya umma, kuimarisha utekelezaji haki na kutuma ujumbe kwamba uhalifu haulipi.

SEKTA YA SHERIA NI MIUNDOMBINU LAINI KUFIKIA DIRA 2050

- Na Prisca Ulomi -



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Dkt. Franklin Rwezimula akizungumza na wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati akifungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi hiyo uliofanyika Jijini Dodoma.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Dkt. Franklin Rwezimula alieleza kuwa sekta ya Sheria sio sekta ya huduma, isipokuwa ni mojawapo ya miundombinu laini kufikia utekelezaji wa Dira ya Taifa 2050.

Naibu Katibu Mkuu aliyasema hayo wakati akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kilichofanyika Jijini Dodoma.

“Kumekuwa na mtazamo kuwa Sekta ya Sheria inahusika na utoaji wa huduma pekee ila ukweli ni kwamba Sekta hii ni miundombinu muhimu ya kufanikisha utekelezaji wa majukumu na hivyo taifa kujitelea maendeleo,” alisema Dkt. Rwezimula.

Pia, aliipongeza OWMS kwa kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali ndani na nje ya nchi kwa ufanisi na weledi na amewakumbusha kuwa lengo la kuwa na Baraza hilo mahali pa kazi ni kuwawezesha wafanyakazi kushauri menejimenti na kushirikiana katika kutekeleza majukumu.

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi alisema kuwa katika kipindi cha mwezi Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliendesha jumla ya mashauri 10,400 ya madai ambapo kati ya mashauri hayo, mashauri 642 yalikamilika na OWMS ilishinda mashauri 563 sawa na asilimia 88%.

“Ushindi huu wa uendeshaji wa mashauri kwa niaba ya Serikali na taasisi zake ni dhahiri kuwa OWMS imeitendea haki Serikali,” alisema Dkt. Possi.

Akizungumza wakati wa salamu za utangulizi, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo alisema kuwa OWMS inawashirikisha wafanyakazi katika majadiliano ya pamoja ya utekelezaji wa majukumu.

Katika hatua nyingine, Dkt. Rwezimula alizindua Mkakati wa Mawasiliano wa OWMS (**OSG Communication Strategy**) ambapo Mkakati huo utaiwezesha Ofisi hiyo kuwa na mwongozo wa kufanya mawasiliano ya kimkakati baina ya Ofisi hiyo, wadau na wananchi, kuchambua na kuainisha njia za mawasiliano, ukusanyaji wa mrejesho na namna ya kufanyia kazi ili OWMS iweze kutumia lugha nyepesi na rahisi kuwasiliana na wadau na wananchi kwa ujumla.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Dkt. Franklin Rwezimula (aliyesimama katikati) akikata utepe kuzindua Mkakati wa Mawasiliano wa Ofisi ya Wakili Mkuu Serikali (OSG Communication Strategy) baada ya kufungua Mkutano wa Braza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali uliofanyika Jijini Dodoma. Anayeshuhudia kushoto kwake ni Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Dkt. Franklin Rwezimula (aliyesimama kulia) akipokea zawadi kutoka kwa Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Ally Possi baada ya kufungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi hiyo uliofanyika Jijini Dodoma.

OFISI YA AG NA NDOTO YA KUWA CHACHU YA KUFIKIA MALENGO YA DIRA 2050

- Na Lela Muhaji -



Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari akisisitiza jambo wakati wa Ufunguzi wa Kikao cha Baraza la Wafanyakazi kilichofanyika Jijini Arusha.

Malengo ya Dira ya Taifa 2050, pamoja na mambo mengine yanalenga kuwa na Utumishi wa umma unaowajibika, hivyo matarajio ni kuwa na utumishi wa umma unaofanya kazi kwa ufanisi, uwajibikaji, uadilifu, uwazi na wenye kupambana na rushwa. Dira hiyo ni ndoto ya Ofisi ya Mkuu wa Serikali katika kuona haya yote yanaafikiwa.

Akizungumza namna ya kufikia lengo hilo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Hamza S. Johari, alisema kuwa Ofisi yake imejipanga kufanya maboresho katika Sheria mbalimbali ili kuweza kufikia malengo hayo ya Dira 2050.

"Tutahakikisha kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inakuwa chachu ya kufikia malengo ya Dira 2050, yanalenga kuwa na Utumishi wa umma unaowajibika, hivyo Matarajio ni kuwa na Utumishi wa Umma unaofanyakazi kwa ufanisi, uwajibikaji, uadilifu, uwazi na wenye kupambana na rushwa. Ni dhahiri kuwa kuwa Mabaraza ya wafanyakazi kwetu ni nyenzo muhimu kwa ustawi wa watumishi, taasisi na Taifa katika kufikia malengo ya DIRA 2050." Alisema.

Katika kukamilisha hilo, Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amewawezesha kwa Rasilimali na vitendea kazi mbalimbali

vinavyowawezesha Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutekeleza Majukumu yao kwa urahisi.

Hivyo Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni jukumu lao kutumia vema muda wa kazi kwa kutekeleza majukumu yake kwa bidii na weledi, ili kuiwezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuendelea kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na kisheria, kupitia utoaji wa huduma za kisheria kwa ubora unaotakiwa na ufanisi na tija inayotarajiwa kwa wadau mbalimbali.

Pia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeeleza mafanikio yake kuwa katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya Mikataba ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa 2,324 ilifanyiwa upekuzi kati ya mikataba 2,000 iliyokuwa imepangwa kufanyiwa upekuzi ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 16 ya utekelezaji.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanikiwa kufanya upekuzi wa Hati za

Makubaliano (Memorandum of Understanding) 396 kati ya 600 iliyokuwa imepangwa ambapo ni sawa na asilimia 66 ya utekelezaji.

Mikataba iliyofanyiwa upekuzi ilihusisha masuala ya ununuzi na ujenzi na ukarabati wa majengo, utoaji huduma za jamii kama vile ujenzi wa shule, hospitali na barabara, huduma za kitaalam, na ununuzi wa bidhaa.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilipokea jumla ya maombi ya ushauri 1,897 kutoka kwenye Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na wadau wengine.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanikiwa kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Kamati za Kudumu za Ushauri wa Kisheria za Mikoa na Wilaya kwa kuzindua na kuendesha Kliniki bure za Ushauri wa Kisheria katika Mikoa ya Manyara, Simiyu na Dar es Salaam na Wilaya zake.



Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Samwel M. Maneno akizungumza wakati wa Ufunguzi wa Kikao cha Baraza la Wafanyakazi kilichofanyika Jijini Arusha

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuunganisha Mfumo wa OAG-MIS na Mifumo ya Kesi (Case Management Systems) ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Mahakama ya Tanzania. Kwa upande wa Wafanyakazi Serikali imeboresha mazingira na maslahi ya Watumishi, yanayowawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Katika kukamilisha Dira 2050, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekuwa karibu na Mahakama kutokana na kutambua mchango mkubwa inayotoa katika jukumu la utoaji haki nchini ikiwa ni utekelezaji wa Ibara ya 107A (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika kutekeleza wajibu huo, Mawakili wamekuwa kiungo muhimu baina ya wananchi na Mahakama katika kuichambua na kuitafsiri haki na sheria. Hivyo Mawakili wana nafasi kubwa katika kuhakikisha jukumu la utoaji haki linatekelezwa kwa ufanisi na Mahakama.

Wakiwa wao ndio maofisa wa Mahakama wamekuwa wakisaidia Mahakama kutekeleza jukumu la utoaji haki nchini kwa kutoa tafsiri sahihi za sheria ili

kuisaidia Mahakama itende haki na kuhakikisha wananchi wanapatiwa haki zao wanapokwenda Mahakamani au kwenye vyombo vingine vya kisheria.

Jambo hili halifanyiki pale shauri linapokuwa linaendelea pekee bali hata wa utekelezaji wa hukumu.

wakati Haya yote yamekuwa yakifanywa katika harakati za kusimamia haki, kwa kuwa wanatambua jukumu lao ni kubwa zaidi ya kuwawakilisha wateja kutokana na kuwa walinzi wa haki.

Katika kutekeleza Dira 2050 katika utoaji wa haki, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imekuwa ikiendesha Kliniki za msaada wa kisheria katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

Mwaka 2023 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilianzisha Kamati za Ushauri wa Kisheria katika ngazi za mikoa na Wilaya ili kurahisisha ufikiwaji wa huduma za ushauri wa kisheria kwa wananchi.

Miongoni mwa majukumu ya Kamati hizo ni kusaidia wananchi kupata haki zao mahali ambako haki hizo zinaweza kupatikana ili kupunguza malalamiko ya wananchi dhidi ya Serikali na kulazimika kutembea umbali mrefu kutafuta haki zao.



Baadhi ya Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiwa katika Kikao cha Barazala Wafanyakazi Kilichofanyika Jijini Arusha.

MCHANGO WA OCPD KATIKA MCHAKATO WA KUTUNGA SHERIA NCHINI

- Na Carine Senguji -



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari akiwasilisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Jijini Dodoma.

Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, pamoja na majukumu mengine, iliendelea kuandaa miswada ya sheria baada ya kupokea Drafting Instructions kutoka Wizara mbalimbali. Katika kipindi cha Januari hadi Julai 2026, Ofisi iliandaa na kushughulikia miswada saba (7) kupitia vikao vya majadiliano na wadau.

Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali Zinazohamishika wa mwaka 2026

Muswada huu ulilenga kuweka mfumo wa usimamizi wa maslahi katika dhamana za mikopo ya mali zinazohamishika, kuanzisha Masijala ya usajili wa maslahi hayo na kuweka haki na wajibu wa wahusika. Uliwasilishwa katika Kamati ya Baraza la Mawaziri ya Katiba, Sheria na Bunge tarehe 28 Januari 2026 kupitia Hati ya Kamati (KB) Na.

1/2025-26, na kusomwa kwa Bungeni tarehe 6 Februari 2 kusomwa mara ya pili na Bunge lijalo.

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2026

Muswada huu ulipendekeza marekebisho katika sheria 18 na uliwasilishwa katika KB tarehe 28, Januari kupitia Hati ya Kamati KB Na. 4 na 5/2025-26, kabla ya kusomwa kwa mara ya kwanza Bungeni tarehe 6 Februari 2026

Miongoni mwa marekebisho hayo yalikuwa katika Sheria ya majin a ya Biashara, Sura ya 213, kifungu cha 21, kuhusu upatikanaji wa taarifa za umiliki manufaa; Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80, vifungu vya 15A, 15B

15D, 15E na 33A, kuhusu uchunguzi wa ajali za ndege, AAU, usiri wa taarifa, mgongano wa maslahi na usalama wa ndege; Sheria ya Kampuni, Sura ya 212, vifungu vya 133 namanufaa wa kampuni za ndani na 438, kuhusu taarifa za hisa na manufaa wa kampuni za ndani na za kigeni.

Pia, Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20, kifungu cha 4, ilipendekezwa kurekebisha ili kuwezesha makosa ya jinai yanayotokana na masuala ya ajira kushughulikiwa kwa wakati, huku vifungu vya 15 na 16 vikijumuisha dawa za kulevya katika hali ya yabisi na kimiminika.

Marekebisho mengine yalihusu Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, kifungu cha 85(1) kuhusu lugha ya sheria ndogo; Sheria ya Usimamizi wa Mahakama, Sura ya 237, kifungu cha 7; Sheria ya Magereza, Sura ya 58, vifungu vya 62A na 81A kuhusu programu za urekebishaji wa wafungwa na msaada baada ya kuachiwa; Sheria ya Usimamizi wa Maabara Binafsi za Afya, Sura ya 136, kifungu cha 13; na Sheria ya Alama za Biashara na Huduma, Sura ya 326, vifungu vya 16A, 16B na 26, kuhusu ulinzi na usajili wa alama.

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kilimo wa mwaka 2026

Muswada huu ulipendekeza marekebisho katika Sheria Nne: Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura ya 249; Sheria ya Tasnia ya Mkonge, Sura ya 30; Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sura ya 251; na Sheria ya Tasnia ya Chai, Sura ya 275. Uliwasilishwa katika KB tarehe 25 Juni 2026 kupitia Hati ya Kamati (KB) Na. 8/2025-26 na kusomwa kwa mara ya kwanza tarehe 26 Juni 2026.

Miongoni mwa marekebisho hayo, kifungu cha 6 cha Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura ya 249 kilipendekezwa kurekebisha ili kuipa Bodi mamlaka ya kutoa miongozo na

kutatua migogoro kati ya wakulima na wafa- nyabiashara. Katika Sheria ya Tasnia ya Mkonge, Sura ya 376, vifungu vya 5 na 22 vilipendekezwa kurekebisha kuhusu mamlaka ya Waziri kutunga kanuni za uchakataji, usafirishaji na uhifadhi wa mkonge. Kwa Sheria ya Tasnia ya Chai, Sura ya 275, vifungu vya 2, 3 na 4, Jedwali la Kwanza na la Pili vilipendekezwa kurekebisha ili kufuta Wakala wa Maendeleo ya Wakulima wa Chai Tanzania na kuhamishia majukumu yake kwa Bodi.

Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa mwaka 2026

Muswada huu ulipendekeza kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto na kuhamisha mali, madeni na watumishi wa Bodi ya Pareto kwenda Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko. Lengo lilikuwa kupunguza taasisi zenye majukumu yanayofanana, kuimarisha uratibu na matumizi ya rasilimali za umma. Uliwasilishwa katika KB tarehe 25 Juni 2026 kupitia Hati ya Kamati (KB) Na. 9/2025-26 na kusomwa kwa mara ya kwanza tarehe 26 Juni 2026.

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 02) wa mwaka 2026

Muswada huu ulipendekeza marekebisho katika Sheria Saba: Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Sura ya 116; Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287; Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288; Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa, Sura ya 61; Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Maliasili, Sura ya 449; Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, Sura ya 138; na Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283.

Marekebisho muhimu yalihusu kifungu cha 7A cha Sura ya 116 kuhusu uwekezaji wa Tume; kifungu cha 25 kuhusu ushirikishwaji

wa Tume katika upangaji wa matumizi ya ardhi; na kifungu cha 61 kuhusu adhabu. Katika Sura ya 287, kifungu cha 38, na Sura ya 288, vifungu vya 25 na 27, muda wa viongozi wa serikali za mitaa ulipendekezwa kuoanisha na muda wa viongozi wakuu Sura ya 288, vifungu vya 25 na 27, muda wa viongozi wa serikali za mitaa ulipendekezwa kuoanisha na muda wa viongozi wakuu.

Aidha, Sura ya 61, kifungu cha 4 kilihusu idadi ya vikao vya Baraza la Usalama la Taifa; Sura ya 449, kifungu cha 11 kuhusu wigo wa utatuzi wa migogoro ya rasilimali asilia; Sura ya 138, vifungu vya 6, 49, 50 na 62 kuhusu ada, thamani ya soko na udhibiti wa taaluma ya uthamini; na Sura ya 283, vifungu vya 111 na 116 kuhusu kuondoa mifugo miongoni mwa vitu vinavyoweza kutaifishwa baada ya kutiwa hatiani.

Muswada huu ulipitishwa na KB tarehe 25 Juni 2026 kupitia Hati ya Kamati (KB) Na. 6/2025-26, na kusomwa kwa mara ya kwanza Bungeni tarehe 26 Juni 2026.



Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2026

Muswada huu ulilenga kufanya marekebisho katika Sheria 26 za kodi na zisizo za kodi, ikiwemo viwango vya kodi, tozo na ada, kuchochea ukuaji wa uchumi na kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Ulisomwa kwa mara ya kwanza tarehe 16 Juni 2026 na, baada ya kufanyiwa marekebisho, ulisomwa mara ya pili na tatu na kupitishwa kuwa Sheria tarehe 25 Juni 2026.

Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Fedha za Serikali wa mwaka 2026

Muswada huu uliidhinisha matumizi ya Serikali kwa mwaka 2026/2027. Baada ya kupitia taratibu zote, ulipitishwa na Bunge tarehe 25 Juni 2026 kuwa Sheria ya kuidhinisha matumizi ya shilingi trilioni 62, bilioni 334, milioni 193, elfu 227 na mia nane kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2027.

Kwa ujumla, miswada hiyo saba ilionesha mchango wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria katika kuandaa na kuboresha sheria ili kuendana na mahitaji ya kiuchumi, kijamii, kiutawala na kisheria ya nchi, huku ikizingatia maelekezo ya Wizara na maamuzi ya Kamati ya Baraza la Mawaziri na Bunge.

Mwandishi Mkuu wa Sheria
Bw. Onorius Njole akifafanua hoja
mbalimbali katika Kikao cha Kamati ya
Kudumu ya Bunge, Utawala,
Katiba na Sheria Jijini Dodoma.

UTAWALA WA SHERIA ILI KUFIKIA MALENGO YA DIRA YA TAIFA 2050

- Na Lela Muhaji -



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari (Katikati) mstari wa mbele, katika picha ya pamoja na Viongozi wa Taasisi za Kisheria na Wakufunzi wa Mafunzo ya Bespoke yaliyofanyika Jijini Arusha.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari aliwataka Mawakili wa Serikali kuhakikisha wanasimamia Utawala wa Sheria sambamba na kuishauri Serikali ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa 2050.

Wito huo aliutoa wakati akizungumza kwenye hafla ya mafunzo ya tatu ya 'Bespoke' kwa Mawakili wa Serikali, yalioandaliwa na kuratibiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yaliyoanza Julai 15, 2026 na kuhitimishwa Julai 17, 2026 katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano Arusha (AICC) Jijini Arusha.

Mhe. Johari alitumia fursa hiyo kuwaeleza Wanasheria wa Serikali umuhimu wa matumizi ya utaalamu wao katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya 2050.

"Ninawakumbusha washiriki wote kuwa, mnatakiwa kutambua katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa 2050, Taifa linahitaji zaidi utaalamu wetu wa Sheria" Mwanasheria mkuu wa Serikali alisema

Katika utekelezaji wa Dira hiyo, Mhe. Johari aliwakumbusha Mawakili wa Serikali kutambua umuhimu wa nafasi yao, ambapo aliwaelezea kuwa utekelezaji wake unategemea kwa kiwango kikubwa uwezo wa Mawakili wa Serikali, pamoja na kuwa na mifumo ya kisheria itakayokwenda sambamba na kasi ya maendeleo na mabadiliko yanayoendelea nchini na duniani kote.

"Imani yetu ni kuwa, Dira hii itatekelezwa kwa kiwango kilichokusudiwa kwa kupitia Sheria bora, Sera madhubuti, mikataba yenye tija, Mifumo bora ya utawala wa sheria sambamba na taasisi zenye uwezo wa kutafsiri malengo ya maendeleo kuwa matokeo yanayoonekana kwa manufaa ya Taifa lote kwa ujumla." Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Katika hatua nyingine, aliwataka Mawakili wa Serikali kuzingatia matumizi ya teknolojia ambayo yamebadilisha kwa kiasi kikubwa, utoaji wa huduma za kisheria ikiwemo matumizi ya Akili Mnemba (AI) na utoaji wa matumizi ya Ushahidi wa Kielektroniki.

"Mapinduzi ya teknolojia yamebadilisha kwa kiasi kikubwa, namna ambavyo huduma za kisheria zinaendelea kutolewa nchini na duniani kwa ujumla, hivyo katika mazingira haya, Mawakili wa Serikali na maafisa sheria hawawezi kuendelea kutekeleza majukumu yao ya kazi kwa kutumia mazoea ya zamani". Alisema Mhe. Johari.

Vilevile, Mhe. Johari aliwataka Mawakili wa Serikali kuendelea kufanya kazi kwa kuzingatia Uadilifu, Weledi, Uwajibikaji, Uzalendo na Nidhamu ili waweze kutoa ushauri wenye ubora, tija na Mikataba yenye manufaa kwa Taifa.

"Wananchi wanatarajia kuona rasilimali za umma zikilindwa kwa wivu mkubwa. Wananchi wanatarajia kuona Sheria zikitumika kama nyenzo ya maendeleo ya kufikia malengo ya Dira ya Taifa 2050." Alisema Mhe. Johari.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali alitoa wito kwa Mawakili wa Serikali kuyatumia mafunzo wanayopata kama fursa ya kujifunza, kubadilishana uzoefu, kujenga mitandao ya kitaaluma, kuibua suluhisho za changamoto zinazowakabili Mawakili hao.

Katika mafunzo hayo kulikuwa na Gavana Mstaafu wa Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Prof. Florens Luoga ambaye aliwasilisha mada kuhusu *"Nafasi ya Kimkakati ya Mawakili wa Serikali katika kufikia Dira ya Taifa 2050,"*. Kwenye mada hiyo alieleza mengi kuhusu nafasi waliyonayo Mawakili wa Serikali katika kufanya maboresho mbalimbali ya Kisheria ili kuweza kutimiza malengo ya Dira 2050.

"Wakili wa Serikali ana nafasi kubwa katika kuchangia maendeleo ya nchi na kulinda maslahi ya Taifa, kwakuwa ushauri wa kisheria anaoutoa ni kichocheo katika mageuzi ya kiuchumi." Alisema Prof. Luoga.

Akizungumza wakati wa kumkaribisha Mgeni rasmi Mhandishi Mkuu wa Sheria, Bw. Onorius Njole alitumia nafasi hiyo kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuwezesha kufanyika kwa mafunzo hayo muhimu kwa Mawakili wa Serikali ambayo anaamini yataleta mabadiliko katika utekelezaji wa majukumu yao.

Pia Mkurugenzi wa Uratibu na Huduma za Sheria, Bi. Neema Ringo akielezea faida za mafunzo hayo alisema yatasaidia kuwawezesha Mawakili wa Serikali kupata uzoefu katika nyanja mbalimbali za kisheria, ambapo alieleza kuwa wakufunzi mahiri watawasilisha mada mbalimbali kwa Washiriki wa Mafunzo ya Bespoke.

Mafunzo ya Bespoke kwa Mawakili wa Serikali yalifunguliwa Julai 15 na kufikia tamati Julai 17, 2026 Jijini Arusha ambapo Mawakili wa Serikali walipata wasaa wa kujifunza masuala mbalimbali ya kisheria na kiuchumi kutoka kwa Wakufunzi wabobevu wa Kitaifa na Kimataifa.

MAWAKILI WA SERIKALI WABEBA MATUMAINI YA TANZANIA KATIKA DIRA YA TAIFA 2050

- Na Lela Muhaji -



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akipokea Kitabu cha Falsafa ya Sheria ya “Mama Samia” kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari wakati wa Ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa TPBA uliofanyika Jijini Arusha.

Kwa takribani wiki moja, Jiji la Arusha liligeuka kuwa kitovu cha mijadala mikubwa kuhusu mustakabali wa sekta ya sheria nchini, huku mamia ya Mawakili wa Serikali kutoka taasisi mbalimbali za umma wakikutana kujadili namna taaluma yao inavyoweza kuendelea kuwa nguzo muhimu katika safari ya Tanzania kuelekea Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Wiki hiyo haikuwa tu mkusanyiko wa wataalamu wa sheria, bali ilikuwa jukwaa la kutafakari nafasi ya sheria katika kujenga uchumi imara, kulinda rasilimali za taifa, kuimarisha utawala bora na kuhakikisha maendeleo ya nchi yanakwenda sambamba na misingi ya haki na usawa.

Katika kipindi hicho, Mawakili wa Serikali walishiriki matukio mbalimbali muhimu ikiwemo Mkutano Mkuu wa Mwaka

wa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania (TPBA), Msimuwa Tatu wa Mafunzo ya Bespoke kwa Mawakili wa Serikali pamoja na uzinduzi wa Kitabu cha Falsafa ya Sheria ya Mama Samia.

Kwa ujumla, wiki ya Mawakili wa Serikali jijini Arusha imeacha ujumbe mmoja mkubwa, kwamba safari ya Tanzania kuelekea Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 haihitaji tu uwekezaji, miundombinu na teknolojia, bali pia inahitaji mfumo madhubuti wa sheria unaosimamiwa na wataalamu wenye weledi, uzaalendo na maono.

Kutoka kwenye mijadala ya kitaaluma, mafunzo ya kujenga uwezo, uzinduzi wa kitabu cha falsafa ya sheria kauli za viongozi wakuu wa nchi, Arusha imekuwa jukwaa lililoonyesha wazi kuwa Sekta ya Sheria ina

nafasi muhimu katika kulinda rasilimali za taifa kusimamia maendeleo na kuhakikisha Tanzania inafikia malengo yake ya muda mrefu kwa misingi ya haki na utawala wa sheria.

Kalamu ya Mwanasheria ni Silaha ya Maendeleo

Miongoni mwa matukio yaliyovuta hisia zaidi ni ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Chama cha Mawakili wa Serikali uliofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Julai 13, 2026.

Katika hotuba yake, Mhe. Dkt. Samia aliwataka Mawakili wa Serikali kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu, weledi na uzalendo, akisisitiza kuwa wao ni walinzi muhimu wa rasilimali za taifa kupitia taaluma yao.

Mhe. Dkt. Samia alisema kalamu ya mwanasheria ikitumika kwa usahihi inaweza kuzuia hasara kabla haijatokea, kulinda mikataba ya Serikali kabla haijawa mzigo kwa wananchi na kusaidia viongozi kufanya maamuzi yenye manufaa kwa taifa.

“Nawataka Mawakili wa Serikali kuendelea kuwa walinzi wa rasilimali za taifa kwa kutoa ushauri wa kisheria kwa usahihi, uzalendo, uaminifu na kutanguliza mbele maslahi ya taifa,” alisema Dkt. Samia.

Kwa mujibu wa Rais Samia maendeleo ya taifa hayawezi kutenganishwa na sheria bora na wataalamu wenye uwezo wa kuzisimamia kwa manufaa ya wananchi.

Serikali yapokea Matokeo ya Maboresho

Katika hotuba yake, Mhe. Dkt. Samia pia aliipongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hatua mbalimbali zilizochukuliwa katika kuimarisha mifumo ya upekuzi wa mikataba, urekebu wa tafsiri za

sheria, utoaji wa msaada wa kisheria pamoja na kliniki za sheria kwa wananchi.

Alisema hatua hizo zimekuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha utekelezaji wa shughuli za maendeleo na kuongeza ustawi wa wananchi.

Mhe. Rais pia alieleza kuridhishwa kwake na juhudi za kutafsiri sheria kwa lugha ya Kiswahili, akisema hatua hiyo itasaidia wananchi wengi kuelewa sheria, haki zao, wajibu wao na mipaka ya mamlaka ya Serikali.

“Hatua hii ni muhimu kwa sababu mwananchi anapoelewa sheria anaelewa haki zake, wajibu wake na mipaka ya uhuru wake. Huu ndiyo msingi wa utawala wa sheria,” alisema.

Sheria na Dira ya Taifa 2050

Kila kikao katika wiki hiyo ilikuwa nafasi ya Sekta ya Sheria katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Mhe. Dkt. Samia alisema Tanzania inahitaji mfumo washeriaunaoweza kuwahamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika kujenga uchumi wa kisasa, shindani, jumuishi na unaotegemea maarifa pamoja na ubunifu.

Alieleza kuwa matarajio ya taifa kwa miaka 25 ijayo yanahitaji sheria zinazowezesha uwekezaji, biashara, ubunifu na matumizi ya teknolojia huku zikilinda maslahi ya wananchi.

Chama cha Mawakili wa Serikali Chajivunia Mafanikio

Akizungumza katika mkutano huo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye pia ni Mlezi wa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania (TPBA), Mhe. Hamza Johari, alisema chama hicho kimeendelea kukua na kuwa jukwaa muhimu la kubadilishana uzoefu wa

kitaaluma na kujenga uwezo wa wanachama wake.

Alisema kupitia chama hicho, Mwakili wa Serikali wameendelea kuimarisha maadili ya kazi, ushirikiano wa kitaaluma na mchango wao katika taasisi mbalimbali za umma.

“Chama bora cha kitaaluma ni kile kinachosaidia Serikali kufikia malengo yake na siyo kuitikisa au kuiyumbisha Serikali” alisema Mhe. Johari.

Alieleza kuwa miongoni mwa malengo ya mkutano huo ni kujadili maendeleo ya chama, sekta ya sheria kwa ujumla na kufanya uchaguzi wa viongozi wa chama hicho.

Kitabu kinachoeleza Falsafa ya Sheria ya Mama Samia

Mafanikio mengine yaliyotajwa katika mkutano huo ni uzinduzi wa Kitabu cha Falsafa ya Sheria ya Mama Samia.

Kwa mujibu wa Mhe. Johari, kitabu hicho kinaeleza kwa kina namna maboresho yaliyofanyika katika sekta ya sheria yalivyosaidia kuleta mabadiliko katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini.

Alisema kitabu hicho kinaonesha jinsi Serikali ya Awamu ya Sita iliv yotumia sheria, sera, taasisi na mifumo ya utekelezaji kujenga mazingira ya maridhiano, uwekezaji, uwazi, haki na maendeleo ya wananchi.

Mafunzo ya Bespoke yalivyochochea Ujenzi wa Taifa

Baada ya mkutano mkuu, macho ya washiriki yalielekezwa kwenye Msimu wa Tatu wa Mafunzo ya Bespoke kwa Mwakili wa Serikali uliofanyika Julai 15 hadi 17, 2026.

Baada ya mkutano mkuu, macho ya washiriki yalielekezwa kwenye Msimu wa Tatu wa Mafunzo ya Bespoke kwa Mwakili wa Serikali uliofanyika Julai 15 hadi 17, 2026.

Akifungua mafunzo hayo, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Zainab Katimba, alisema Serikali ina matarajio makubwa kwa Mwakili wa Serikali katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati na kufanikisha Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Alisema taifa linahitaji mawakili wenye uwezo wa kufikiri kimkakati, kuona mbali na kutumia sheria kama nyenzo ya maendeleo badala ya kuiona kama chombo cha kutatua migogoro pekee.

“Tunahitaji Mwakili wa Serikali watakaohakikisha kila mkataba unalinda maslahi ya taifa, unaongeza thamani ya fedha za umma, unaepusha migogoro na unachangia maendeleo endelevu,” alisema Mhe. Katimba.

Aliwahimiza washiriki kutumia maarifa waliyojifunza kuboresha ushauri wa kisheria, usimamizi wa mikataba, uendeshaji wa mashauri na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Teknolojia na Akili Mnemba Zabadili utojai wa Huduma za Kisheria

Katika mafunzo hayo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza Johari alisisitiza umuhimu wa Mwakili wa Serikali kuendana na kasi ya maendeleo ya teknolojia.

Alisema mapinduzi teknolojia yamebadilisha namna huduma za kisheria zinavyotolewa duniani, hivyo mawakili hawawezi kuendelea kufanya kazi kwa kutumia mifumo na mazoea ya zamani.

Mhe. Johari alitaja matumizi ya Akili Mnemba (Artificial Intelligence) ushahidi wa kielektroniki na mifumo ya kidijitali kuwa sehemu ya mabadiliko ambayo wataalamu wa sheria wanapaswa kuyaelewa na kuyatumia katika kazi zao za kila siku.

Kwa upande wake, Naibu Mwanasheria Mkuu, Mhe. Samwel M. Maneno alisema mafunzo hayo yamewapa washiriki fursa ya kujadili masuala mbalimbali ya kimkakati

yatakayosaidia kuimarisha nafasi ya Mawakili wa Serikali katika utekelezaji wa Dira ya Taifa 2050.

“Tunaamini maarifa na ujuzi walioupata utawawezesha kutekeleza majukumu yao kwa weledi, ubunifu na ufanisi zaidi katika kulinda na kutetea maslahi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,” alisema.



Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Samwel M. Maneno akizungumza wakati wa Mafunzo ya Bespoke kwa Mawakili wa Serikali, yaliyofanyika Jijini Arusha.

Sauti *ya* Sheria

TOLEO LA 2 — MACHI - SEPTEMBER, 2026



Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
Mji wa Serikali - Mtumba
S.L.P 630, Dodoma - Tanzania
info@oag.go.tz www.oag.go.tz
+255 26 2961941



Ofisi ya Taifa ya Mashtaka
20 Barabara ya Mashtaka
S.L.P 1733, Njedengwa Dodoma
dpp@nps.go.tz
www.nps.go.tz
+25526 2963634



Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali
10 Barabara ya Kivukoni
S.L.P 71554, 11101,
Dar es Salaam
info@osg.go.tz I www.osg.go.tz
+255 22 2127384



Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria
Mtaa wa Tambukareli
Jengo la PSSSF -Kambarage
S.L.P 438, Dodoma - Tanzania
info@ocpd.go.tz
www.ocpd.go.tz

**UTEKELEZAJI WA DIRA 2050
MCHANGO WA SEKTA YA SHERIA
KATIKA KUJENGA TANZANIA MPYA**



oagtanzania



oag_tz



oagtanzania



Mwanasheria Mkuu TV



omashtaka



Ofisi ya_taiya ya_mashtaka



Mashtaka TV



Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali



osgtanzania



osgtanzania



Wakili Mkuu TV



www.ocpd.go.tz



+255 262 961 949



@ocpd_tanzania



@ocpd_tz



@ocpd_tanzania

